**5 NOVEMBA, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Tano – Tarehe 5 Novemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

**na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2021**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Benaya Luka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINDA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo siku ya kipekee, siku maalum iliyopatikana kwa maamuzi yako makubwa kwa nia njema kabisa ya kuisimamia Serikali, kwa maneno hayo kwa dhati kabisa nakupongeza wewe na kwa kweli umeonesha kwamba yanapofikia mambo haya mazito *your very serious*, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru pia mimi Benaya Kapinga, hivi karibuni umenipeleke kwenye Kamati hii nzito, Kamati ya *LAAC*, kwa hiyo, nakushukuru kwa uteuzi napata nafasi ya kuisaidia nchi yangu lakini kuona namna gani Watumishi tuliowapa dhamana wanavyokwenda kutuvuruga, wanavyokwenda kuharibu rasilimali ambazo Seirkali imeziweka kwa ajili ya kusaidia nchi. Kwa hiyo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, nitajielekeza katika maeneo mawili, matatu. Ripoti za Mkaguzi zimetuonesha kuna mapungufu makubwa kwenye utekelezaji wa maagizo na mapendekezo. *CAG* anasema katika Taasisi za Serikali

hizi hususan Halmashauri kuna shida kubwa ya kutekeleza maagizo yanayotolewa. Kwa nini maagizo yanatolewa, au mapendekezo yanatolewa, *CAG* anapofanya ukaguzi anakutana na vitu tofauti tofatui, anaona dosari tofauti tofauti, ndipo inafikia hatua ya kutoa mapendekezo ili kuondoa hizo dosari. Pia Bunge linapoona kuna dosari hizo ndiyo linakuja kutoa maagizo. Sasa inapofika huyu anayeagizwa hatekelezi yale maagizo inakasirisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa zinasema mwaka uliotangulia walitoa maagizo zaidi ya Elfu Kumi, kati ya hayo ni maagizo 3,511 tu ndiyo yaliyotekelezwa. Sasa najiuliza wewe ni mwalimu, kule chuo ulikuwa unatoa *assignment* mwanafunzi harejeshi, unatoa *assignment,* hivi mwisho wa siku si unajua hatua inayofuata? Nami napendekeza hapa kwa taasisi ama Halmashauri ambazo hazitekelezi haya maagizo kwanza zinaonesha kiburi, jeuri. Kwa nini zinafanya hivyo? Nia ni moja tu Halmashauri za namna hii ni kuzichukulia hatua kali ikiwemo kuziondosha mezani, hakuna haja kuendelea baadhi ya Halmashauri hapa naambiwa zina hoja hizi miaka Kumi, zina hoja hizi miaka saba, kila zinaitwa mezani, zinapigwa maneno zinaondoka, kesho tena…

Mheshimiwa Spika, kwa kweli jambo hili linonesha kupunguza hadhi ya Bunge ambayo inatoa maagizo. Sasa tusikubaliane nalo tuchukue hatua kubwa ikiwemo kuzifukuza hizi Halmashauri na kama zitarejea basi hatua kali zidi ichukuliwe dhidi ya Halmashauri hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee pia suala la upotevu wa mapato, taarifa zinasema kuna upotevu mkubwa sana wa mapato ya Serikali, yako maeneo tofauti tofauti

ambayo yanayosababisha upotevu wa mapato ya Serikali ikiwemo wakati wa makusanyo, pia wakati wa matumizi. Katika wakati wa makusanyo, ziko Halmashauri hazipeleki fedha benki, hapa taarifa inasema katika mwaka wa ukaguzi zaidi ya Bilioni 20 hazikupelekwa benki, sasa najiuliza hizi fedha zilienda wapi? Hawa watu wanafahamu sheria iko wazi, ukikusanya ndani ya muda fulani unatakiwa upeleke fedha benki. Sasa kwa vile wanayo mikakati yao na namna yao, Serikali imeanzisha utaratibu mzuri wa makusanyo kupitia *POS*, inafika baadhi ya sehemu hizo *POS* zinazimwa, baadhi ya hizo *POS* zinakusanya fedha hazionekani, baadhi ya hizo *POS* zinakusanya fedha mtu mmoja ana-*ID* zaidi ya mbili. Nia hapo ni mbaya sana, nia ovu ya kutaka kutumia hizi fedha za Serikali, sasa Bilioni 20 hazipelekwi benki zinaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunaambiwa Bilioni 33.9 hazikukusanywa kabisa, kwenye maeneo ya ushuru wa mazao, kodi za pango, mauzo ya viwanja, leseni za vileo, sokoni, pamoja na ushuru wa hoteli hazikusanywi. Sasa hapa ni mipango inayofanywa na baadhi ya hawa watumishi, wanafanya mipango wanachukua kidogo cha chini cha juu wanamwachia Serikali inapata hasara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana tuweke maazimio hapa makali, ya kuwataka Wakurugenzi hawa watekeleze Sheria na Kanuni za Fedha, muda mfupi huu wanapokusanya hizi fedha wazifikishe benki na ambaye hajapeleka hizi fedha benki hatua kali ichukuliwe, ikiwemo pia na kumfunga, kwani wezi hawafungwi? Huyu mtu ambaye hapeleki fedha benki kwa maksudi.

Mheshimiwa Spika, nasema nakushukuru kwa sababu ninashuhudia pale tunapofanya mahojiano na Maafisa Masuuli, sababu zingine unaona ni za kawaida mno haifai kabisa. Kwa sababu naona kengele ya kwanza imenigongea na sijui tunachangia dakika ngapi ni dakika Tano ama dakika Kumi? Naona kengele imenigongea Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Imegonga ya kwanza, kwa hiyo wewe malizia.

**MHE. BENAYA L. KAPINDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Eneo lingine ambalo linatupotezea fedha nyingi ni eneo la uwekezaji. Taarifa hapa imesomwa na Wenyeviti wetu wametuambia, uwekezaji huu kwa baadhi ya Halmashauri wanaufanya na wamelenga kupeleka kwenye maeneo hasa mawili, stendi na soko. Imejidhihirisha maeneo hayo baadhi ya Halmashauri hayana tija. Ningeshauri Sana soko na stendi zijengwe kwenye maeneo labda ya Miji mikubwa na halmashauri za Majiji lakini kule Vijijini tuwe na stendi za kawaida sana ambazo hazina sababu ya kutumia fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, mfano Jiji la Mbeya walikopa fedha kujenga soko la Mwanjelwa, zaidi ya Mabilioni yamewekwa pale na taarifa ya *CAG* inatuambia deni lile linatakiwa lirejeshwe kufikia 2033, Halmashauri inapaswa kurejesha kila mwaka zaidi ya Shilingi Bilioni Mbili lakini mapato halisi ya pale Halmashauri ni Shilingi Milioni 750 hadi Shilingi Milioni 850, sasa watapata wapi fedha hizo zaidi ya Bilioni na kidogo ili kurejesha benki, tena benki ya kibiashara, hiyo hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya miradi hii wakati mwingine inafanyika pasipo kufanyika kabisa wanaita

tathmini na upembuzi yakinifu, lakini cha zaidi kile kinaitwa *project plan* - andiko la kibiashara, andiko la kibiashara ndiyo litaonesha mradi huu hapa utakaa kwa namna gani, utatoa faida kiasi gani mpaka mwaka gani, sasa watu wanakwenda wanaweka tu mradi pale hawajafanya chochote wanaleta Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ninaomba hapa kwamba tusikubali kuruhusu mradi wowote pasipokuwa na tathmini, upembuzi yakinifu wa eneo hilo. Lakini tusikubali kuanzisha mradi pasipo kuwa na hili andiko la kibiashara ambalo litatuonesha faida na muda wa kupata faida huo mradi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee pia miradi iliyotelekezwa. Taarifa ya *CAG* inatuambia kwamba ipo miradi ya zaidi ya Bilioni 41.5 imetelekezwa kwa muda mrefu. Miradi hii ukiwauliza Maafisa Masuuli wanasema hii miradi ni ya nguvu za wananchi, mwananchi anapoibua mradi maana yake kaona tatizo anataka kuondokana na lile tatizo, kwa hiyo, hii miradi ni muhimu kuliko hata haya masoko na vingine. Mwananchi kaona hapa tuna shida ya zahanati anaona hapa kuna shida, jambo hili tuitake Serikali itenge fedha nyingi najua inatenga fedha lakini iongeze zaidi fedha ili miradi hii iliyoanzishwa na wananchi ikamilike na lengo la kuanzisha ile miradi kwa wananchi litimie kuliko ilivyo sasa tunawavunja moyo sana wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano mmoja.

**SPIKA:** Utamalizia na huo mfano.

**MHE. BENAYA L. KAPINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika Halmashauri yangu kuna ujenzi wa

zahanati, zahanati ile imejengwa toka mwaka 1995 imepauliwa mpaka leo ipo hivyo hivyo, yaani imeisha kupauliwa. Sasa ukiona eneo inapotolewa huduma utalia, ni kibanda tu kamepigwa bati hapo ndipo wanakotolea huduma, hapa kuna jengo nzuri, fedha imeenda pale, tena wanasema wananchi walikuwa wanachota maji mbali kweli toka mwaka 1995 hadi leo zahanati ya Kilanga Juu Kata ya Mbuje, lakini Maafisa hawa Masuuli wapo, Afisa Mipango yupo miaka inaenda, miaka inaenda hawaoni hata sababu ya kukamilisha ile miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii miradi kama nilivyosema Serikali ipeleke fedha nyingi pia hata Halmashauri zenyewe kuliko kuanzisha miradi mingine ikamilishe hiyo miradi iliyopo. Ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge wakati Mheshimiwa Benaya akichangia nikawa najiuliza sijui na mimi nisimame hapa kama Mheshimiwa Nicodemas Maganga alivyokuwa anajitetea jana. Amelitaja hapa Jiji la Mbeya, ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran ajiandae. *(Makof/Kicheko)*

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi kwanza kabisa nianze kukupongeza wewe kwa namna ambavyo umeliendesha Bunge hili na kuendelea kuwapa Wabunge nguvu zaidi na kuendelea kuliheshima Bunge, kwa dhati ya moyo wangu ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwanza kabisa niseme naunga hoja taarifa zote za Kamati ambazo ziko hapa mezani ambazo ni Kamati ya *PAC, LAAC* pamoja na *PIC* ambayo Mimi ni Mjumbe huko. Nitachangia katika maeneo mawili, nitachangia kwenye asilimia Kumi za Halmashauri pamoja na Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nikianza na asilimia Kumi ya mapato ya Halmashauri naona kabisa nia ya dhati kabisa ya Serikali kwanini waliweka kuwepo na asilimia Kumi hii ya Halmashauri. Lengo kubwa ilikuwa ni kuhakikisha wanampa mwananchi huyu nguvu kumuwezesha katika uchumi wake ikiwa ni sambamba ya kuendelea kumpa madaraka ya yeye kuendelea kujisimamia kama ambavyo Serikali yoyote inapaswa kufanya duniani kote.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu nataka kum-*quote* kidogo ambaye alishakuwa Rais wa Marekani Thomas Jefferson, anasema hivi, ''*The purpose of the Government is to enable the people of a Nation to live in safety and happiness. Government exists for the interests of the governed, not for the Governors*''. Akiwa na maana kwamba Serikali yoyote duniani maslahi yake kwanza ni kuwaridhisha wale ambao wanawatawala na siyo wale ambao watawaliwa. Tafsiri yake, viongozi wote wa Serikali na wasimamizi wote ambao wamepata dhamana cha kwanza kabisa jukumu lao ni kuhakikisha wanalinda maslahi ya wananchi ambayo sisi wao tunawatumikia au kwa lugha nyingine kama ni Serikali ambao tuseme wanawatawala.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo nataka nirejee kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, nitasoma mambo kadhaa. Kwenye sura ya Sita ya Ilani ya Chama

cha Mapinduzi, ukurasa wa 161 ukienda kwenye ukurasa wa 174 unasema hivi, kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi katika hali iliyoshirikishi, Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka ijayo imetarajia kufanya yafuatayo:-

(i) Kuimarisha mifumo ya taasisi na uwezo wa Viongozi na Watendaji wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda Vijijini kusikiliza na kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi kwa wakati na haki na uadilifu. Aidha, kupokea na kusikiliza na kuwahudumia wananchi wanaotembelea ofisi hizo kwa weledi hekima na busara;

(ii) Kufanya mapitio ya Sheria za Tawala za Mikoa na Sheria za Serikali za Mitaa ili kuendana na uboreshaji wa mifumo ya utoaji huduma kwa wananchi;

(iii) Kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha makusanyo ya mapato katika vyanzo vilivyopo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;

(iv) Kuimarisha Serikali za Mitaa ili ziendelee kuwa chombo cha kuwapa wananchi uwezo na sauti ya kuamua kushiriki kwa karibu katika shughuli za maendeleo, mwisho na mengine yanaendelea;

(v) Kusimamia kikamilifu suala la utawala bora ndiyo hapa ambapo watu wamekula hela hapa, narudia, kusimamia kikamilifu suala la utawala bora, uadilifu, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasimali za umma pamoja na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mamlaka hizo, itekelezwe kwa kiwango kinachokusudiwa

kuhakikisha kuwa ubora wa miradi unalingana na thamani ya fedha iliyotumika.

Mheshimiwa spika, kwenye ripoti ya *CAG* inaonesha kwamba kwenye asilimia kumi zipo halmashauri kwamba kwenye asilimia kumi zipo asilimia 155 nchini hazikuweza kurudisha yale marejesho, bilioni 47.5. Bilioni 47.5 zote hizi cha kwanza, zimepora mamlaka ya wananchi ambazo ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema; 'kwamba mtawala yeyote anapokuwepo kwenye madaraka lazima ahakikishe anawapa nguvu wale ambao wao wamemuweka madarakani'. Hizi bilioni 47.5 zimepotea ziko kwenye mifuko ya watu, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sio najiuliza na ni wazo langu katika maazimio ambayo wenyeviti wa Kamati wanaweza wakachukua. Nikaona tu; kwa mfano TAMISEMI wangeamua kwamba waweke dirisha maalum linaloshughulikia mikop tu, labda tuchukulie kwamba afisa maendeleo wao wamekuwa na shughuli nyingi na hawana huo utaalam wa kusimamia hizi fedha. Hizi fedha ambazo zimepotea bilioni 47.5 ni katika kipindi cha mwaka mmoja tu 2021/2022, bilioni 47.5.

Mheshimiwa Spika, nikachukulia mfano, wako vijana wengi mtaani ambao hawajaariwa ambao ni *bankers, accountant*, pamoja na wachumi. Tufanye kama TAMISEMI, ingeamua kuajiri kwa kutumia fedha hizi hizi ambazo ni za Serikali, zimeliwa toka kwenye mifuko ya watu au zimepotea kwa uzembe ambao unasababisha na wataalam wetu kutokuvaa, kuzimiliki zile fedha kwamba ni fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi nikawa najiuliza, kwenye mabenki yetu, *CRDB, NMB* na benki zingine zilizopo hapa hapa nchini, hao ambao ni wataalam wa kusasanya mikopo wametoka nje wapi? Si wamesoma hapa hapa ni ma-*banker* wamesoma hapa hapa nchini kwetu mbona wana huo utaalam wa kukusanya mikopo? Kuna mwananchi yeyote amekopa hela benki anaweza akala fedha? Sasa kwanini sisi Serikali isitenge dirisha kuwaajiri wataalam, wahasibu, wachumi, ma-*banker* wakasaidia kutoa elimu, kukusanya fedha hizi na fedha hizi zirudi?

Mheshimiwa Spika, nikaweka hesabu ya kawaida tu kwa mfano TAMISEMI, waamua kumuajiri *graduate* ambaye amemaliza *degree* yake ya uchumi, uhasibu *whatever* ambaye anaweza kusimamia vizuri mikopo, waanze kwa kumlipa mshahara wa Shilingi laki saba, wakaajiri watu watatu kwenye halmashauri 84, nikapata kwamba wakiwaajiri watoto watatu kwa mwezi watakuwa wanawalipa milioni 2,100,000, ukichukua milioni 2,100,000 katika halmashauri 184 tutapata milioni 386,400,000. Nikaweka kwamba tufanya kwa miaka mitano ya majaribio, hii ambayo tunatekeleza ilani utakuta hawa vijana umewalipa bilioni 1.932; lakini unaona kwa mwaka mmoja hela zimepotea bilioni 47.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tafsiri yake tungeweze kuajiri vijana watatu tu, ambao ni uhasibu, *banker* na mchumi wanakaa yaani wao kitengo chao ni *special* kusimamia mikopo tu ya asilimia 10, katika kipindi cha miaka hiyo mitano ambayo tumeweka tungeweza kuwalipa bilioni mbili. Tafsiri yake ni kwamba tungeweza kuokoa hela.

Mheshimiwa Spika, lakini bado nikapiga hesabu, ukiwaajiri vijana hao kwenye halmashauri 184 utaajiri vijana wakitanzania wasiopungua 520. Kwa hiyo pia tungekuwa tume-*solve* changamoto ya ajiri. Hata hivyo, kama wangesimamia kwa ufanisi, zile hela zingekuwa zinazunguka; maana yake kama mwaka huu watu walikopeshwa bilioni moja, mwaka huu halmashauri ikakusanya tena bilioni moja vikundi vitapata, nikatolea tu mfano, mfano nikachukulia halmashauri yangu. Labda halmashauri yangu sisi labda mwaka huu wa fedha tulipata bilioni 1.7, kwa hiyo ni milioni 170; tukivigawia vikundi vitano wangeweze kupata milioni 34 kwenye kila kikundi. Tafsiri yake milioni 34 hii ingekuja na mwaka mwingine siwangekusanya? Milioni 34 ingekuja na vikundi vingine na wakati huo mapato yaongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hayo ni mapendekezo yangu kwa wenyeviti wa kamati, kwamba ipo haja ya kuona hili. Lakini wakati tunaendelea kuona ipo hoja ya kuona hivi hawa waliohusika na jambo washughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na benki ya kilimo. Benki ya kilimo, pamoja kwamba mwaka wa nyuma kuna kiwango cha pesa ambazo walipewa kama bilioni 208, lakini walikuwa wanaomba waongezewe mtaji angalau bilioni 760. Ni kweli, mimi ninatamani waongezewe hicho kiwango cha fedha ili kuleta tija kwa wananchi wetu ambao ni wakulima; na tukiangalia nchi hii kwa kiwango kikubwa wazalishaji wakubwa ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, pia nataka niseme, watu hawa wa Benki ya Kilimo pamoja na kwamba mnataka

kuongezewa fedha na Waziri wa Kilimo upo hapa, pamoja hatukushauri tunakusimamia muda huu, tunaomba kuona mnapotaka kuwaongezea fedha hizi tuwape, zikalete tija kweli kwa wananchi, zifike kule kwa wananchi ambao tunawakusudia. Ni kweli tunaona kuna benki ya kilimo, lakini kuna wakati jamani kule vijijini hatuona sana tija hii ya benki ya kilimo mwananchi wa kawaida hakopesheki, mwananchi wa kawaida kule kijijini hapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano mzuri tu pamoja naongelea Benki ya Kilimo. Miezi miwili iliyopita tulipata ruzuku ya mbolea, tukaambiwa Wabunge tukatoe taarifa kwamba Serikali inatuletea mbolea, ni kweli mbolea imekuja. Cha kushanga sasa hivi tunavyoongea tumebakiwa na wiki mbili tu msimu wa mvua urudi wananchi vijijini waanze kulima mpaka sasa mbolea hazijafika vijijini, mpaka muda huu mbolea bado na sehemu zingine mbolea imeenda ya aina moja tu.

Mheshimiwa Spika, sasa tunajiuliza wakati mwingine mnapotuomba Wabunge tuwasaidie kuwapikishia hiki tuona na tija ili wakati mwingine tunapokuja hapa; kwamba kama tuliwasaidia kuwapitishia hizi fedha au ndio mnaomba tuwapendekezee kama sisi Bunge maazimio yetu, tuone na mambo ambayo yanafanana na mambo hayo. Kama ni Benki ya Kilimo imewezeshwa imfikie kweli mkulima, lisionekane tu lipo kundi la mapapa hawa ambao wao tu ndio wana-*grub* na kuchukua wao tu lakini mwananchi wa kawaida yule ambaye ndiye mzalishaji halisi, yule ambaye mpaka sasa hivi analima kwa jembe la mkono, yeye ambaye sasa hivi kununua mfuko mmoja tu wa *DAP* ni changamoto, amekopeshwa,

mwananchi huyu ambaye bado hata mbegu yenyewe kununua ni shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunategemea Benki ya Kilimo ndiye huyu tumkusudie apate. Wakati mwingine ukiwauliza watu wa Wizara wanasema Benki ya Kilimo kazi yake si kufungua matawi huko vijijini na sehemu zingine zingine kwenye wilaya kwa sababu hawafanyi *transaction*.

Mheshimiwa Spika, mimi ninajiuliza, kwani Mheshimiwa Rais, Mama Samia anaishi kwenye halmashauri zote 184? Si anaishi Ikulu hapa Chamwino na Dar es Salaam? Lakini mbona miradi yote akitoa inafikia halmashauri zote 184? Kote anapeleka. Kwa hiyo, kaeni na benki Dar es Salaam, *whatever,* wekeni kwenye kanda lakini tunachotaka huduma zifike. *Whether* mtatafuta mawakala wakufikisha hizi huduma kwa wananchi *or* mtaunda vikundi, lakini tunataka mkulima wa kawaida, yaani tunaongelea mkulima wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, na katika hili nimuombe Mheshimiwa Waziri Bashe, twende nikakukutanishe na wakulima wa kawaida huko vijijini ili tunapoongea muwasilize wenyewe kwa masikio yao, hawapati mikopo.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja zote za kamati ambazo ziko mezani, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, Mhesimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kuwapongeza Kamati zote tatu zilizotuletea ripoti zao hizi pamoja na ripoti ya *CAG*. Kwa kweli wamekaa na kuchambua na wametulea vitu ambavyo tunaweza kujadili asubuhi hii ya leo. Naunga mkono hoja za kamati zote tatu.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza kwenye kipengele ambacho kinahusu fedha za dharura ambazo zinatumiwa na halmashauri pale ambapo kunatokea majanga, maafa na maradhi ya mlipuko.

Mheshimiwa Spika, inapotokea maradhi ya mlipuko hayana dakika wala saa; lakini wanapoomba vibali halmashauri Wizara husika inachelewa sana kutoa majibu ya vibali vile na hapo inasababisha wavunje sheria kwa kutumia fedha ambazo hazikuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa, ili kuepusha isiwe kichaka cha upotevu wa fedha nyingi cha kutumia kipengele cha kwamba maradhi ya mlipuko au majanga na maafa Wizara iandae aidha, kitengo maalum au wahusika maalum ambao watapokea barua na watafanyia kazi kwa haraka kwa dharura iliyojitokeza ili kuepusha matumizi ambayo hayakuidhinishwa na au kuwa, kama nilivyosema mwanzo, kuwa kichaka cha utumiaji wa fedha za umma bila matarajio yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hapa inakuja hoja, je tusubiri kibali cha matumizi au tuachie watu wafe? Sasa inapokuja hoja kwamba tuwaachie watu wafe ndipo halmashauri na wahusika kutumia fedha bila kupata

kibali. Hili suala lina hoja nzito kwa sababu huwezi kuwaacha watu wakafa wakati fedha unazo lakini fedha hizo ni madhumuni ya watu walewale ambao unatakiwa kuwaoongoza lakini wakifa wote unaomuongoza nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikijielekeza kwenye mchango wangu kuna ripoti ya *CAG* kuna hasara ya shilingi takriban milioni 56 ambazo wamelipwa watumishi hewa, watumishi waliostaafu, watumishi waliokufa na watumishi ambao hawapo kazini kabisa. Hapa ni upotevu mkubwa wa fedha za umma ambazo zinahitaji fedha zile zielekezwe katika kutumia fedha hizi katika mambo mengine ambayo yanahusu maendeleo ya nchi, ya wananchi na watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, nikiunganisha hapo hapo kwenye suala la watumishi, kwenye ripoti ya *CAG* kuna madeni ambayo yanahusu bilioni 160 ambayo hawajalipwa watumishi, pamoja na milioni 96 ambazo ni posho na mengine haya kwa ajili ya watumishi ikiwemo uhamisho, likizo na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumishi hawa ndio tunawategemea wasimamie fedha zetu, watumishi hawa ndio tunategemea wakakwamue maendeleo ya wananchi na wasimamie fedha na maendeleo ya wananchi. Lakini tunapowavunja moyo na kuwakatisha tamaa, malimbikizo mengine yanafika miaka kumi, mitano, sita mpaka mtumishi anakufa mrithi wake anakufa fedha hizi anapewa nani? Anakuja kupokea mtu ambaye hausiki kabisa hajamsaidia lolote yule mtumishi aliyetumia nguvu zake.

Mheshimiwa Spika, ukiwahoja halmashauri ni mkakati gani ambao wameweka kulipa watumishi hao mabilioni haya wanatenga fedha kidogo sana ambazo kwa kutenga fedha hizo inaweza ikachukua muda mrefu, takriban miaka kumi hajamaliza madeni.

Mheshimiwa Spika, tutafute hatua za haraka na dharura ili kuhakikisha tunapunguza angalau nusu ya madeni ya watumishi wetu ili watumishi hawa wasitumie fursa hii ya kuhujumu kwa sababu hawalipwi likizo, uhamisho, mishahara, na matibabu. Sasa ili wasihujumu, wasifiche mapato wafanya kazi zao kwa weledi na kwa uaminifu na wao stahiki zao zinatakiwa zilipwe kwa wakati. Wajibu unaendana na haki. Sasa, sasa, ili atekeleze wajibu wake mtumishi apate haki zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea. Kuna uvujaji mkubwa wa mapato katika halmashauri ambako hawakusanyi mapato kutoka kwenye vyanzo vingi, na hapa kuna upotevu mkubwa wa fedha za Serikali na fedha za umma. Kwa mfano kuna ushuru wa mazao, chanjo na machinjio ambako zaidi ya bilioni 14 hazikukusanywa kwenye baadhi ya halmashauri; tumeikuta katika ripoti ya CAG.

Mheshimiwa Spika, huu uvujaji wa mapato au kutokukusanya mapato kunaitia hasara kubwa Serikali, kwa sababu haya mapato tunayotaka kuyakusanya ndiyo tunatakiwa tuwalipe watumishi, tulipe vikundi, kufanyia shughuli nyingine za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiongezea hapo hapo kwenye ukusanyaji wa mapato, mfano ukusanyaji unaohusiana

na kilimo, mifugo na uvuvi ndani ya halmashauri watenge *percent* ambayo itasaidia kuendeleza zile sekta, tuziziachie Wizara peke yake. Kule kuna uvuvi, kilimo, ufugaji, zitengwe fedha kwaajili ya kuongeza majosho, kusaidia uboreshaji wa kilimo na mabwawa. Hii ni kwa sababu ndio ushuru wa kilimo chenyewe au uvuvi na mifugo yenyewe. Kuonekane basi kuna faida kuendeleza kile kilimo katika ile halmashauri kwa sababu wanachukua fedha kutoka kwao hayo ni maoni kwa sekta zinazohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelea, kuhusu mfuko wa wanawake, vijana na wenye ulemavu, hili ni takwa la kisheria kupeleka 4:4:2, lakini baadhi ya halmashauri hawafikishi hiyo asilimia kwa hivyo vikundi, na inasababisha sasa kuzorota kwa ile azma ya Serikali ya kumkomboa mwananchi kiuchumi na kupunguza umaskini wa kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hii mifuko kuna takriban bilioni 47.01 hazijakusanywa kwenye mamlaka 155, bilioni 47 hazijakusanywa kwenye mamlaka 155.

Mheshimiwa Spika, hapa inabidi tutafakari na tujiulize; kweli fedha hizi zitapatikana? Waliohusika na kupewa hiyo mikopo wapo? Hivyo vikundi viko? Uhakiki umefanyika ili kuhakikisha vikundi hivi viko hai na vinafanya uzalishaji? Kama vinafanya uzalishaji na havirejeshi mikopo basi ni suala letu sisi wahusika kufuatilia hiyo mikopo. Lakini kama baadhi ya vikundi havipo ni kwamba tuna haja sasa ya kuhakikisha fedha hizi zinakwenda kwa walengwa husika ambao wana miradi mahususi ya uzalishaji ili fedha hizi zirudi zikasaidie wengine katika kujikwamua na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano halmashauri badala ya kuwapa fedha wahakikishe vile vikundi wanavipa ujuzi kwanza ndipo baadaye wanavipa vifaa na vitendea kazi. Wavisimamie ili kuhakikisha wao wenyewe wananufaika lakini na Serikali fedha zake zinarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo kuna baadhi ya halmashauri hawapeleki ile asilimia 40 na asilimia 60 kwenye miradi ya maendeleo. Hili ni takwa la kisheria, inatakiwa fedha ziende kama ilivyotakiwa ili kuimarisha miradi ya kiuchumi na miradi mingine ya kijamii katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikimalizia la mwisho nakuja kwenye uhaba wa watumishi, uhaba wa watumishi umejitokeza katika sehemu nyingi za halmashauri zetu. Hapa nitoe rai. Halmashauri itenge fedha za kusomesha na kuwajengea uwezo wale watumishi waliopo, wasisubiri tu uajiriwe na Serikali kuu ilete kwa sababu wao wana fedha na wana watumishi. Kwa mfano, kwenye sekta ya hesabu na sekta ya mambo ya kimtandao *(TEHAMA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta hizi mbili ndiyo zinachangia sana kwenye uvujaji na upotevu wa mapato katika halmashauri, tukiweka wataalam, halmashauri ikiwa na mpango mkakati wa kusomesha watu wake wale wale walio ndani ofisini kuwajengea uwezo watu wa hesabu na *TEHAMA* hakutakuwa na upotevu na ubadhirifu mkubwa wa fedha wataweza kuweka hesabu zao sawa na kujua wanafanya nini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, nampongeza Mheshimiwa Rais, anajitahidi sana kuhangaika huku na kule kutafuta fedha kwa ajili ya wananchi wetu. Ni wajibu wetu sisi tumuunge mkono kuhakikisha fedha hizi zinatumika ipasavyo ili kuwaletea wananchi wetu maendeleo, na kuwapunguzia upungufu na umaskini wa kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata nyumbani kama unahangaika kuomba, kukopa, unachuna uso unakwenda kwa ajili ya watoto wako, lakini watoto wakawa wanaharibu, hawatumii ipasavyo roho yako inanyonga, inaumia na inachukia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwaunge mkono viongozi wetu wote waliopo madarakani kwa kuhakikisha kwamba tunawasaidia katika kuokoa fedha na katika kuwasaidia wananchi kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru na naunga mkono hoja zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Sillo Barani, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kupata nafasi niweze kuchangia katika hoja ambazo ziko mbele yetu. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi kwamba kuna miradi mingi inaendelea katika majimbo yetu

pamoja na huduma za jamii. Nikupongeze pia wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuongeza Bunge letu vizuri na tunakupongeza kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nipongeze wenyeviti na makamu wenyeviti na wajumbe wa kamati hizi tatu, kwa maana ya *PIC, PAC* pamoja na LAAC kwa kuchambua taarifa hizi, ripoti ya *CAG* pamoja na uwekezaji wa mitaji ya umma katika taasisi ya mashirika mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza kwanza kwenye kamati ya *PIC*, uwekezaji wa mitaji ya umma. Faida ambayo inatarajiwa kupata na Serikali katika utendaji huu ni gawio, mchango wa asilimia 15, marejesho kutoka *TTMS,* yaani mtambo unaosimamia masuala nchini riba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliyoishia Juni 30, 2021, kwa upande wa gawio, malengo ambayo *TR* aliweka kwa kukusanya ilikuwa ni Shilingi bilioni 408.4, lakini makusanyo halisi ni Shilingi bilioni 308 sawa na ufanisi wa asilimia 76.3. Tukienda kwa upande wa michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi, Msajili wa Hazina aliweka lengo la kukusanya Shilingi bilioni 395.4, lakini makusanyo halisi ni Shilingi bilioni 202.2, sawa na ufanisi wa asilimia 51 ya lengo. Kwa upande wa marejesho kutoka *TTMS,* malengo kwa mwaka wa fedha huu uliyoishia Juni 2021 ilikuwa ni Shilingi bilioni 15, lakini makusanyo halisi ni Shilingi bilioni 10.3 sawa na ufanisi wa asilimia 68.3.

Mheshimiwa Spika, picha inayoonekana hapa ni kwamba kwa ujumla mwenendo wa mapato yasiyokuwa ya kodi, yanayotokana na uwekezaji huu uliofanywa na Serikali, yamepungua sana kwa mwaka huu wa fedha

uliyoishia Juni 2021. Vilevile tukumbuke kwamba fedha hizi ni sehemu ya bajeti zetu, maana mapato yote haya yanaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali *(consolidated fund)*. Kwa hiyo, tunapokuwa hatufanikishi bajeti zetu ni kwa sababu ya usimamizi usioridhishisha kwa baadhi ya taasisi au mashirika ambako Serikali imewekeza. Matokeo haya yanaonyesha dhahiri kwamba baadhi ya taasisi ambazo Serikali zetu imewekeza kodi za wananchi hayasimamiwi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya *PAC* kusomwa ukurasa wa 22 inazungumzia taasisi kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi. Bodi ya Wakurugenzi ni chombo kikuu cha uamuzi katika taasisi na mashirika ya Umma. Kwa hiyo, unapokosa chombo cha maamuzi pale ambapo Serikali imewekeza, unatarajia nini? Lazima utarajie matokeo haya ambayo hakuna mahusiano yaliyofika hata asilimia 80. Kwa hiyo, kutokufikia malengo haya ni kwa sababu kuna maamuzi ambayo yalitakiwa yafanyike, hayakufanyika. Hata wanaofanya biashara binafsi, kama ndani ya mwaka mzima hakuna kikao kinachokaa kufanya maamuzi, unatarajia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, suala la Bodi ni la msingi sana. Lazima kuwe na *checks and balance*. Kwa hiyo, naomba sana wale wanaohusika na uteuzi wa Bodi, wateuliwe Wajumbe wa Bodi wenye weledi katika taasisi hizi na mashirika ambapo Serikali imewekeza. Taasisi hizi zikifanya vizuri, haitaishia kupata gawio asilimia 15 ya mapato ghafi na marejesho haya, lakini yatapata faida ambayo pia italipa kodi ya mapato. Kwa hiyo, mashirika haya yakiboreshwa katika misingi hii yataongeza Mapato ya Taifa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na Bajeti Kuu ya Serikali. Kwa hiyo, naomba sana

kwa kweli jambo hili tulichukilie kwa uzito mkubwa sana kwa upande wa Serikali maana ni kwa faida ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)*. Nampongeza sana Mwenyekiti na timu yake nzima kwa kazi kubwa waliyofanya, wamepitia Taarifa ya *CAG,* imeonyesha madudu ambayo tumeyaona. Taarifa ya *CAG* inasema, Serikali imepata hasara ya Shilingi bilioni 68.73 ambayo ilisababishwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* kuchelewa kuwalipa Wandarasi. Taarifa inasema, kusimama kwa ujenzi wa vihenge unaotekelezwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi *(NFRA)* wakati Mkandarasi ameishalipwa Dola za Marekani 33.4 sawa na karibu Shilingi bilioni 76.8; taarifa inaendelea kusema, malipo ya Dola za Marekani milioni 153.43 yalifanywa na *TANESCO* kwa *SYMBION* ambayo takriban ni Shilingi bilioni 350; taarifa hii inasema, fedha hizi ni nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, leo Waheshimiwa Wabunge tunalia hapa miradi ya barabara kwenye majimbo yetu, nishati ya umeme haipo, lakini kuna wenzetu ambao wamepewa dhamana ya kusimamia fedha za Umma, wanazichezea. Naomba sana wenzetu wenye dhamana hizi wawe na uchungu na Watanzania. Wawe wanatembea vijijini kuona hali halisi ya maisha ya Watanzania. Tukumbuke hizi ni kodi za Watanzania. Tunakaa Bunge hapa miezi mitatu tunapanga bajeti, halafu watu wachache wanakaa wanachezea fedha za Umma. Jambo hili linaumiza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna miradi mingi ya kimkakati inataka fedha, tuna upungufu wa kibajeti, tunataka

fedha, tuna upungufu wa watumishi wa Afya, Elimu katika maeneo yetu, tunataka fedha; tuna deni la Serikali, tunataka fedha tulipe; Watanzania wana shida ya maji katika maeneo mbalimbali; tuna shida ya nishati ya umeme vijijini, lakini wapo wenzetu wameamua kucheza na fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge toka Bunge hili limeanza, inatia uchungu sana pale ambapo fedha za Umma zinachezewa. Kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwachukulia hatua wote waliohusika na ubadhirifu huu wa fedha za Umma. Sisi ni wawakilishi wa wananchi, tunaelewa uhalisia ulioko kwa wananchi kule. Kuna msemo wa Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwamba mihemo ya mgonjwa anajua anayelala naye. Sisi ndio tunalala na wananchi wetu. Kwa hiyo, naomba Wenyeviti wa Kamati, pamoja na maazimio ambayo wameweka, basi tuongeze yetu kwamba lazima waliochezea fedha za Umma wachukuliwe hatua za kisheria na kikanuni za kiutumishi ili liwe fundisho kwa wengine kwa miaka mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kila mwaka katika taarifa za CAG makosa yanajirudia kwa taasisi hizo hizo, na watu wapo tu. Jambo hili halikubaliki, sisi kama Wabunge lazima tusimame na kuwatetea Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache, nashukuru kwa kunipa fursa na ninaunga mkono hoja zote tatu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia na ninaunga mkono hoja zote tatu za Kamati. Vilevile nakushukuru wewe kwa kutuongoza vizuri Wabunge na kutuwezesha kufanya kazi zetu vizuri na kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lina mchanganyiko wa Wabunge wazuri wenye weledi mkubwa sana. Pia naomba nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuifungua nchi kuitafutia fedha na pia kubwa, ku-*control* uchumi wa nchi yetu ambao umeweza kuhimili mfumuko *(inflations rate)* ambao upo duniani kwa sasa hivi. Nchi yetu imeweza ku-*control,* kwa mfano tu wa haraka haraka, duniani huko nchi iliyotutawala, Uingereza mpaka Septemba *inflations rate* yao, wao wali-*target* 2% ya *infations rate,* lakini mpaka Septemba, 2022 wamekuwa na *inflations rate* ya *10.1 percent* kwa maana ya *two digits*.

Mheshimiwa Spika, kwa uwezo wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan wa ku-*control* uchumi wetu, sisi tumeendelea kuwa katika *single digit* ya uchumi wetu kwa maana ya kudhibiti kwa mfano mafuta, kupeleka ruzuku, pia lingine kubwa kuweka ruzuku ya mbolea kwa wakulima. Kwa hiyo, tunamshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, wetu.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye hili la mbolea kabla sijaenda kwenye mada, tunaishukuru sana Serikali baada ya kuiomba kuweka kituo cha ununuzi wa mbolea Namtumbo ambacho kilikuwa Songea Mjini. Watu wa Namtumbo walikuwa wanatembea kilometa nyingi kwenda kufuata mbolea. Serikali ilisikia na imefungua kituo Namtumbo Mjini. Hata hivyo, bado haitoshi, tunaomba mbolea za ruzuku ziende vijijini kwa wakulima kama ilivyokuwa hapo nyuma. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itafakari ione jinsi gani inaweza ikasaidia kwenye hili.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hussein Bashe.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Vita na Wabunge wote, siyo rahisi kwa Serikali kufungua vituo vya kuuzia mbolea katika kila kijiji katika nchi yetu. Vituo vya kuuzia mbolea ya ruzuku vitafunguliwa katika *centers* ambazo hapo awali biashara ya mbolea ilikuwa inafanyika na kwa Wakala ambaye atafikia vigezo tunavyoviweka vya udhibiti ili tusirudie matatizo yaliyotokea 2014, 2015, 2016 ambapo ruzuku haikumsaidia mkulima, bali iliwasaidia Mawakala na Wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba kama una *concern* ya eneo, wasiliana na Wizara, tutali-*evaluate* eneo hilo, kwa

sababu unaweza ukapeleka kijijini gharama ya kusafirisha na ku-*supply* mbolea kule kijijini, mantiki yote ya ruzuku ikawa imekufa na wala isiwepo bila sababu yoyote. Kwa hiyo, tutafungua katika maeneo ambayo awali mbolea ilikuwa inauziwa na *distribution* tutendelea kuiongeza kadri ambavyo inawezekana.

**SPIKA:** Mheshimiwa, kabla sijamwuliza Mheshimiwa Vita Kawawa kama anaipokea taarifa hiyo, nadhani jambo la msingi ni kwamba mbolea isogezwe kwa wakulima. Hilo ndilo jambo la msingi. Sasa hoja ya kila Kijiji ni namna Mheshimiwa Mbunge anavyojenga hoja yake, lakini hoja ni kwamba maeneo ambayo wakulima ni wengi, mashamba ni makubwa, mbolea isogee kwao ili kuwapunguzia mzigo wa kusafiri umbali mrefu kwenda kufuata mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Vita Kawawa, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, kuipokea ni ngumu kweli. Napokea maelekezo yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sasa nirudi kwenye hoja. Taarifa ya CAG imetueleza kwamba baada ya kufanya tathmini, fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 185, kulikuwa na Shilingi bilioni 838 hazikupelekwa kwenye miradi ya maendeleo na pia matumizi ya kawaida. Pia imejitokeza taarifa ya CAG inasema, kuna Halmashauri 39 zilipokea fedha za makisio ya bajeti zilizohidhinishwa ziada Shilingi bilioni 74.38 kama 8% ya makisio yaliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, hapa utakuta kwamba kuna halmashauri zimepata zaidi ya makisio yao ya bajeti ambayo yaliidhinishwa na Bunge lako Tukufu, lakini kuna halmashauri ambazo zimepata upungufu. Sasa ushauri wangu hapa ni kwamba, siyo vyema kwa Watumishi wa Serikali ambao wana *disburse* fedha hizi wakazigawa halmashauri. Halmashauri nyingine zinapendelewa, nyingine zinanyimwa fedha. Tutoe kulingana na tulivyoidhinisha kwenye Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unasema katika ukurasa wa nane wa kwenye kishikwambi kwamba, Kamati imeona kuwa dosari hizo hazikutokea kwa bahati mbaya na ishara ya mkakati maalum unaoratibiwa na baadhi ya Watumishi wa Umma wasiokuwa na uadilifu kwa lengo la kuwa na upendeleo, udanganyifu na ubadhirifu. Katika hili, naomba Serikali na sisi Bunge katika maazimio yetu tusimamie ili Wizara ya Fedha ihakikishe inatoa fedha sawa kwa wote kama walivyoidhinishiwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Wizara ya Fedha itueleze katika eneo hili ambalo kuna baadhi ya halmashauri zimeongezewa fedha za ziada nje ya bajeti iliyoidhinishwa imelifuatitia kama kweli fedha hizo za ziada zilizotoka nje ya bajeti zilifanya kazi gani huko katika halmashauri zilikopelekwa? Suala la tatu, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe azimio lake kwamba, Bunge lifanye uchunguzi ili kubaini iwapo fedha zilizotolewa zaidi, au nje ya bajeti haikuwa na viashiria vyovyote vya upendeleo, udanganyifu au ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati iliendelea kusema halmashauri nyingi hufanya manunuzi kwa dharura bila

kuzingatia mipango ya manunuzi kwa mradi wa mwaka. Wote tunafahamu kuna Sheria ya Manunuzi, lakini ukitazama shida iliyojitokeza hapa kubwa ni kwa sababu mfumo huu wa *force account,* ni mzuri lakini lazima tukubaliane kuwe na kiwango maalum cha fedha za miradi itakayofanyika kwa huu mfumo wa *force account*. Tukiacha mradi wa fedha, Shilingi milioni 800, Shilingi bilioni moja, Shilingi bilioni mbili, ukaendeshwa kwa mfumo huu wa *force account* peke yake, ndiyo shida hizi zitaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nini kinatokea? Kinachotokea ni kwa kwamba Watumishi wa Halmashauri ndio wanaonunua vifaa na wanatafuta fundi. Sasa hapa kwenye ununuzi wa vifaa mradi unaanza; wakati ukiwa kwenye msingi, Watumishi wa Halmashauri, Idara ya Manunuzi inanunua vifaa vyote vya mwanzo mpaka msumari wa bati, mpaka rangi inanunuliwa kwa mara moja. Ukitazama kiuhalisia kwenye *tender* au kwa Wakandarasi wanaofanya kazi hizi, huwa wanapewa fedha kulingana na kazi waliyoaifanya. Sasa pale wanaponunua vifaa vyote kwa mara moja, kwa maana nyingine wanaweza wakanunua vifaa vile kwa *interest* yao ya *ten percent* au wapate ziada, wana-*inflate rate* za bei na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaponunua vifaa vyote vile kwa pamoja, inapofika mradi umefikia mwishoni, fedha zimekwisha na kuna vitu vya msingi vinatakiwa, wanakosa fedha za kuzifanya. Kwa mfano, kwangu Namtumbo yaliyotokea Waziri Mkuu alipokuja kuangalia na kuona milango iliyokuwa chini ya kiwango, kwa sababu fedha zote zimekwisha, hawana fedha za

milango, wanaenda kuchukua fundi wa Mwembeni kutengeneza mlango, ndiyo yaliyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile siyo hayo tu, ukiondoa hiyo, baadaye wameingia tena kula hata mbegu yenyewe. Kwangu Namtumbo kule kuna mradi ulikuwa wa kutengeneza vyoo vya zahanati zetu tano. Wameenda kununua *cement* 1,200 lakini zilizoshushwa ni *cement* 600, na 600 nyingine zimeshuka huko njiani. Pia wameenda ku-*order* milunda 800 ya kutengenezea vyoo. Unatengeneza vyoo vya shimo ili uweke milunda ufunike! Milunda ya nini kwenye vyoo? Milunda haikuletwa, fedha zimelipwa toka mwaka 2021. Waziri Mkuu anakuja ndiyo wamestuka, wameenda kuleta milunda 800 wameilundika. Waziri Mkuu akastukia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la *force account* nalo tunasema lazima tuliangalie. Hayo makosa yataendelea kuwepo, lazima tuwe na *limit* ya fedha kwa ajili ya Miradi ya *force account*. Miradi mikubwa ya fedha nyingi lazima itumike na Wakandarasi. Tukubali, tusikatae, mradi wa bilioni na zaidi hauwezi kutumiwa tu na fundi. Lazima tuangalie hilo pia. Vilevile kuepusha gharama. Kwa mfano, yaliyotokea kwangu Namtumbo kwenye hospitali ya Wilaya, fundi yule kashamaliza kazi yake, hakuna fedha za kuweza kurekebisha ile milango. Tunamlazimisha sasa *technician* aliyesimamia atengeneze kwa gharama yake. Ingelikuwa kazi ile inafanywa na Mkandarasi, kuna fedha zinabakizwa pale, hapewi miezi sita. Kama kuna dosari, anarekebisha.

Mheshimiwa Spika, sasa hili la *force account* ndiyo hasara yake hiyo. Pia *force account* fundi hela zote zile hazilipiwi kodi. Anapopewa Mkandarasi, analipa kodi;0

analipa *service levy* kwenye Halmashauri na pia analipa *TRA*. Hela nyingi kwa ajili ya *force account* kwa fundi tu hailipwi, Serikali hai-*collect,* inatoa tu, lakini ikimpa Mkandarasi, Serikali pale inatoa na inakusanya kodi.

Mheshimiwa Spika, leo hii mradi wa bilioni nne kwangu unajengwa na shule ya wasichana wanapewa mafundi wa kawaida. Pale Serikali haitakusanya na halmashauri haikusanyi, lakini *on top of that* wana-*inflate rate* ya vifaa vile.

**SPIKA:** Sekunde 30, malizia.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wana-*inflate rate* ya vifaa, gharama inakuwa kubwa, matokeo yake *CAG* anakuja kuona hayo, kwa hiyo, haya yataendelea kuonekana kutokana na watumishi wasiokuwa waadilifu. Nakubaliana kabisa watumshi wote ambao pia, hawakuwepo, shida wanayoipata Kamati zetu hizi wakiwaita, unakuta waliokuwepo sasa hivi wanakwambia mimi nina miezi miwili sikulifahamu hili. Kwa hiyo, tunaomba wale wote waliokuwepo mwaka huo 2021, waitwe watoe majibu kutokana na hoja za *CAG* na hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Erick James Shigongo ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Ripoti ya *CAG,*

lakini na ripoti za Kamati hizi. Kwanza nakupongeza sana kwa uamuzi uliochukua kutoa siku zote hizi tuweze kujadili ripoti na haya mambo ya Kamati. Nakupongeza kwa sababu hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo umenuia kulisaidia Taifa na kumsaidia Mheshimiwa Rais. Naamini tutakapokuwa tunafunga tutakuwa tumetoka na maazimio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana kwenye kutafuta fedha za Taifa hili, lakini ukiisoma Ripoti ya *CAG,* narudia lugha moja kwamba, ukiwa huna akili huwezi kupata shida, ila ukiwa na akili timamu hii Ripoti ya *CAG* unaweza ukachukua maamuzi magumu sana. Ukisoma Ripoti ya *CAG* anazungumzia mtiririko wa matumizi mabovu ya fedha kwenye Taifa letu kwa muda wa miaka mitatu mfululizo. Kwa mwaka 2018/2019 *CAG* anasema matumizi mabovu yalikuwa ni bilioni 14. Mwaka 2019/2020, *CAG* anasema matumizi mabovu yalifika bilioni 380. Mwaka 2020/2021, *CAG* anasema matumizi mabovu yamefika bilioni 1.14, maana yake kila siku fedha za Serikali zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Joe Biden, Rais wa Marekani alizungumza alisema: *"Corruption is a cancer, a cancer that eats away at a citizen's faith in democracy, diminishes the instinct for innovation and creativity."*

Mheshimiwa Spika, Rais Rodrigo wa Ufilipino anasema: *"Where there is no corruption, there will be no poverty."*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa nataka kuzungumzia nini? Nataka kuzungumzia shirika moja tu la umma kwa mfano, Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini

*(GPSA)*. *CAG* anamtaja *GPSA* kama ni mtu ambaye hadi dakika hii amechukua zaidi ya bilioni 10 na hajaleta magari ndani ya miaka mitatu, ndani ya miaka miwili. Utajiuliza huyu *GPSA* ni Wakala wa Serikali, nakupa mfano mmoja tu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanamdai *GPSA* zaidi ya magari 500 na fedha amelipwa kwa muda wa miaka miwili, lakini hajaleta magari hadi leo. Ukimuuliza *GPSA* anasema kulikuwa na *Covid*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa namuuliza *GPSA* Bandari ya Dar-es-Salaam ni lini ilisimama kutoa huduma wakati wa *COVID?* Soko la Kariakoo lilisimama wakati wa *COVID,* lakini *GPSA* alisimama kutoa huduma wakati wa *COVID,* Serikali inamdai magari. Achana na hapo, Wizara ya Afya wamempelekea *GPSA* ombi la kuwanunulia magari ya bilioni 17. *GPSA* kawaletea *quotation* ya magari 487 kwamba, kwenye hizo bilioni 17 nitanunua magari 487. Wizara ya Afya wakajiongeza wakasema sisi hatununui kupitia wewe, wameenda *UNICEF,* wameenda kupata magari 663.

Mheshimiwa Spika, sasa unajiuliza *UNICEF* sio shirika letu la ndani ambalo tunafanya nalo kazi, ila tuna Wakala ambaye ni *GPSA* ameweka *difference* ya magari 100 ndani ya Wizara ya Afya, yeye angenunua angenunua magari 400, lakini *UNICEF* ameweza kununua magari 663 kwa fedha zilezile bilioni 17. Sasa najiuliza Serikali yetu, wataalam wetu wana lengo gani na wana nia gani na Serikali yetu?

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo inahangaika hawana fedha, *GPSA* hela anayo na ameshalipwa. Kwa hiyo, nashauri ni vema *GPSA* ikaangaliwa, ikaundiwa

tume, ikachunguzwa. Hakiwezekani kikawa ni chombo cha kunyonya badala ya ku-*regulate* matumizi ya fedha ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, nazungumzia vitu vitatu. Kuna kitu ambacho sijakisoma, hata kwenye Kamati humu sijakiona, kuna kitu kinaitwa bakaa. *CAG* anazungumzia bakaa kwamba halmashauri zetu nchini zilivuka na bakaa ya bilioni 30. Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewane, mimi niko Kamati ya USEMI, halmashauri nyingi nchini zina-*underestimate* ukusanyaji wa mapato, zikisha-*underestimate* ukusanyaji wa mapato, ndani ya muda mfupi unashangaa wamevuka lengo la ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, leo nazungumza, Halmashauri ya Tunduma anakotoka Mheshimiwa David Silinde, tayari robo hii wameshavuka tayari nusu ya ukusanyaji wa mapato wa bajeti waliyotuomba sisi. Maana yake ni nini? Wataenda zaidi ya asilimia 120 au 150, ile fedha inayobaki ya bakaa Wabunge jiulizeni wanaifanyia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda halmashauri mbalimbali hapa, ukienda Halmashauri ya Kinondoni walivuka karibu na milioni 500. Ukienda kwa Mheshimiwa Cosato Chumi wamevuka karibu na bilioni moja. Ukienda Halmashauri ya Mwanza wameenda zaidi ya bilioni moja. Hawa wote wanabakiwa na bakaa hizi ambazo ukifuatilia matumizi yake ni matumizi ya chinichini, fedha za Serikali zinapigwa. Naomba sana *LAAC* wachunguze matumizi ya bakaa kwenye halmashauri zetu kwa sababu kimekuwa ni kichaka cha ku-*underestimate* ukusanyaji wa

mapato, wanavuka lengo, fedha zinazobakia wanazipiga kupitia vikao na mambo ambayo hayamo kwenye bajeti na utunzaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kuna suala la *POS*. *CAG* anazungumzia *POS* anasema halmashauri 46, Mamlaka za Mitaa 46, kwa muda wa siku tatu hadi siku 400, hizi *POS* zilikuwa zinapotea, nyingine zinaonekana leo, kesho zinapotea kwenye mfumo hazionekani. Serikali imepoteza mapato zaidi ya bilioni 427. Sasa ni lazima tutafute mfumo bora wa jinsi gani ya kukusanya mapato kwenye halmashauri zetu, kwa sababu hizi *POS* zinatumika ni kichaka pia cha kuiba fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine, hili la asilimia 10. Asilimia 10 nilizungumza hapa kwa muda wa miaka mitatu yote hadi sasa tuna zaidi ya bilioni 100 za asilimia 10 ziko mitaani, lakini kwenye Taifa hili wenzetu wa Jiji la Dar-es-Salaam walijaribu kutumia *DCB Bank* kama sehemu ya kusambazia fedha na *DCB Bank* ilifanya kazi vizuri sana. Walivyogundua kwamba, inafanya vizuri sana kazi wakaiondoa kwa sababu walikuwa hawana sehemu ya upigaji, wameirudisha kwenye mfumo wa kawaida fedha zinapigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Burundi, Serikali ya Burundi inajua sana kusimamia hizi fedha. Wameandaa madirisha ya kibenki kwa ajili ya wanawake na vijana ili hizi fedha ziweze kusimamiwa vizuri, lakini kwenye Taifa letu wanakwepa huo mlango kwa sababu unakwepa mianya ya upigaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *CAG* anasema mwaka 2020/2021 bilioni 47 hazijarejeshwa, ziko kwenye mifuko ya watu,

lakini halmashauri hazijapelekwa zaidi ya bilioni sita, unakuta *is a lot of money*. Mheshimiwa Rais anatafuta hela ya ruzuku ya mafuta, hela zimefichwa. Mheshimiwa Rais anafuta ruzuku kwa ajili ya mbolea, hela zimepigwa. Tunamsaidiaje Mheshimiwa Rais wetu kama hizi fedha tutaendelea kuruhusu kuendelea kupigwa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu walishauri hapa kwamba, watu wengine wapigwe risasi na wengine wanyongwe, lakini nasema kabla hatujalifanya hilo lazima tufanye *list of shame*. Lazima tutangaze *list of shame of this country* kwenye *institutions* za Serikali, kwenye Mawakala wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupa mfano, kwenye *list of shame* mojawapo, kuna watu hapa wanaitwa Mamlaka ya Maji Safi ya Dar-es-Salaam. *CAG* anasema wamekusanya zaidi ya milioni 755 kwa kudanganya sio kusoma mita; wanafika mtu wanamwambia tupe hizo hela, zaidi ya milioni 700, hii lazima iingie kwenye *list of shame*.

Mheshimiwa Spika, nenda pia kwenye Shirika la Bima ambalo tuna ndege 11, lakini wanakata zaidi ya dola milioni tano wakati Rwanda wana ndege 12 wanakatwa kwa dola milioni mbili. Maana yake ni Shirika letu la Bima nalo ni kichaka cha wizi wa fedha ambazo ni fedha nyingi zinakwenda huko kwenye bima. Achana na hilo tu, Shirika la Bima la Afya limeacha dola laki tatu kwenye akaunti namba 1156119 kwenye benki iliyoko Uingereza kwa zaidi ya miaka mitano, halisemi kama hizo fedha zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwenye Shirika la Bandari. Ukienda kwenye shirika hili napo kuna upigaji. Wana zaidi ya vifaa vya bilioni mbili ambavyo vilitakiwa vipigwe mnada kwa miaka mitatu iliyopita, wanapiga chenga, vinaibiwa, vimepotea, vifaa vya bilioni mbili, lakini wana fedha zaidi ya dola laki tatu kwenye Benki ya *Deutsche* akaunti iliyoko Uholanzi, hawajawahi kuzisema kwa muda wa miaka mingi zipo kule. Mheshimiwa Rais anatafuta fedha hizi kila siku. Rais hawezi kufika kila kona, Watanzania hili ni Taifa letu tunataka tuamini kwamba, hii nchi inajengwa na wenye moyo na inaliwa na wenye meno? Hatuwezi kuamini katika hilo. Hili ni Taifa letu lazima tulipiganie na hawa wataalamu wanatusikia, nawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda kwenye Bodi ya Mikopo. Bodi hii ilikopa mkopo, ambao Mheshimiwa Mkenda anahangaika nao, walikopa mkopo wa bilioni 54, wame-*delay* kulipa, saa hizi wanadaiwa bilioni 68. Yaani kutoka bilioni 54 waliyokopa, sasa hivi wanatakiwa walipe bilioni 68, *over 100%* wanadaiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda kwenye Mamlaka ya Elimu. Mamlaka ya Elimu ya Ufundi, Makete Jimboni kwangu, wameingia mkataba wa kujenga na Wakala wa Nyumba za Taifa, jengo la bilioni 1.5 hadi leo; mtu amelipwa, majengo hayajajengwa, ametawanyika hadi saa hizi hayupo, hii ni *list of shame* kwenye Taifa letu, mnataka *list of shame* ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba tutakavyoondoka kwenye maazimio haya, hawa watu wasione kama sisi tunapiga *story,* ni muda muafaka wa Bunge lako, wa Kiti chako kuonesha kwamba, tuna msuli wa kupigania Taifa

letu, kuonesha kwamba, tuna uwezo wa kuwawajibisha. Kama hatuwezi kuwapiga risasi basi hata kesho tuwaone magerezani. Kama hatuwezi kuwanyonga basi kesho tuwakute magerezani kwa sababu, wote ni Watanzania wenzetu na wananufaika kwa pesa za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Erick James Shigongo na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii na pia nakushukuru kwa muda uliotoa ili tuweze kujadili taarifa hizi tatu zilizowasilishwa na Kamati zetu. Awali ya yote, sishauri tuanze kufikiria adhabu ya kunyonga, kumnyonga mtu ni kumhamishia kwenye mamlaka nyingine ambayo hatuna udhibiti nayo na ni kumpelekea Mungu wahalifu ambao bado hatujashughulika nao. Hawa tushughulike nao kwanza hapa, itakapofika wakati wameshatubu basi ndipo waweze kunyongwa na kupelekwa huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mchango wangu nitajielekeza kwenye Kamati ya *PIC* kidogo, lakini pia na kwenye Kamati yangu ya USEMI. Kwanza nianze kusema kwamba, naipenda sana Wizara ya Kilimo na hii ni kwa sababu, jimbo langu ambalo wananchi waliniamini na kunileta linategemea sana kilimo. Mwaka huu wakati wa bajeti wote kwa pamoja tulipitisha kwa kauli moja kuongeza bajeti kwenye Wizara ya Kilimo na moja kati ya

maeneo tuliyosema tuweke mkazo ni kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili utafiti uweze kufanyika unahitaji vifaa. Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inasema *TARI* iliomba vifaa vyenye dola elfu 50 hatukuwa nayo. *Bill & Melinda Gates* wakatoa msaada, tena hata kabla hawajaachana hawa maana wameshaachana. Vifaa vile vikaletwa bandarini mwaka 2018, bandari wakavishikilia, vifaa vya utafiti vya virusi ambavyo vinaweza kuleta athari kwenye hii nchi na hicho kilimo chote kisiwe na maana, 2018, wakasema wanataka kodi. Msaada umeletwa mabilioni ya *Melinda Gates,* vifaa hivyo huenda pia vina vitendanishi ambavyo ni sumu vimebaki bandarini, hadi hivi tunavyoongea viko pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesikia juzijuzi kuna nchi bandari iliungua kutokana na kemikali. Sisi tunawekaje vitu hivi kwenye bandari yetu ambayo nina uhakika wanaovishikilia hawana utaalam huo na bado tunategemea hii nchi itaendelea kuwa salama ambapo tumeweka vitu ambavyo hata hatuvifahamu, lakini ambavyo vingekuwa vinatumika kwenye maabara sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapata shida za magonjwa, virusi, kule kwangu mimi vitunguu kuna ugonjwa unaitwa kaukau hata hatuujui, maabara zetu vitendanishi viko bandarini toka 2018, kisa Wizara ya Kilimo imeomba msamaha. Ndio ile sasa jini likila kwingine linakula hata wakwake, Wizara ya Kilimo Serikali, imeomba msamaha kwa Wizara ya Fedha, msamaha 2018 hakuna, 2019 hakuna, 2020 hakuna, 2021 na leo hakuna, vifaa bado

viko bandarini. Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inasema vifaa hivi vinaweza kuharibika, vitolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengine sijui yanasubiri maazimio au hapahapa tu useme kabisa waweze kufanya maamuzi, mimi sijui, lakini kuna vitu vya hatari kama hivi ambavyo tusipovisemea tutakuwa hatuwatendei haki wananchi ambao wanasubiri kilimo ili kiweze kuwatia moyo. Hili ni jambo ambalo ni moja kati ya mambo unaweza ukayaona yaliyoko *TRA* kwa namna ambavyo tumekuwa tukitaja. Pia kuna taasisi hapa haupiti muda hatujazisema, tukija tunazisema, tukiondoka tunasema, nadhani huko nje wanasema, watasema watamaliza, halafu sisi tutaendelea na mtindo huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufike wakati ieleweke kwamba, tunapokuja humu ndani tumetumwa na wananchi milioni 61 na wale wananchi hawawezi kuja huku kusema ndio wametutuma sisi ili tuwasemee, walipanga mstari tarehe 28 Oktoba, kutupigia kura ili sisi tuje tuwasemee mambo ambayo yanawaathiri wao, tukinyamaza tutakuwa hatuwatendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiacha hilo la *TARI* ambalo linawaumiza wananchi kwa sababu, utafiti haufanyiki kwa sababu vitu viko bandarini kwa sababu Serikali inasubiri kodi kutoka kwenye Serikali yenyewe. Sasa naomba nizungumze kidogo kuhusu hao hao *TRA* ambapo wameng'ang'ania hivyo vifaa. Ukienda kwenye ripoti inasema kabisa, lita milioni 2.6 za mafuta ambayo yalikuwa yanasafirishwa kwenda nje hayakwenda nje, hiyo ni fedha yenye thamani ya bilioni 1.7, yalipotelea

humu ndani. Ripoti inasema mafuta haya kwa kuwa hayakutoka maana yake yatakuwa yaliuzwa humu ndani na Serikali haikupata kodi. Sasa badala ya kushikilia vile vifaa kule si wangeenda wakakusanya hii fedha ya mafuta ya kodi ambayo inapotea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii *TRA* iangaliwe. Wakati inaangaliwa ikumbukwe pia kwamba, hii ndio inayofanya ukusanyaji wa mapato makubwa zaidi ili iweze kuangaliwa vizuri, iangaliwe pia na watumishi wake idadi yake kwa sababu, ina upungufu wa watumishi 2,695 kwa mujibu wa Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, ni mambo ya kuangalia ili tuweze kufanya vizuri na tuweze kutekeleza vizuri Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kuzungumza ni mifumo ya taasisi tunazoziunda na dhamira yetu ya kuzifanya ziweze kuendelea. Nimesema pale awali mimi ni Mjumbe wa Kamati ya USEMI, hizi halmashauri zina chombo chake kinaitwa *ALAT*. Hiki chombo ambacho kinaitwa *ALAT* kinatarajiwa kuendeshwa kutokana na michango ya halmashauri, sasa kati ya mwaka 2015 na mwaka 2021, jumla ya bilioni 4.56 hazikupelekwa *ALAT* na kwa kutokupelekwa, hiyo ni asilimia 91 ya mapato ya hii *ALAT,* maana yake ni kwamba, haiwezi tena kujiendesha. Kwenye taarifa inasema kabisa kwamba, kuna hatari ya *ALAT* kushindwa kujiendesha kwa sababu haina mapato.

Mheshimiwa Spika, sasa ni vizuri tukatafakari tu kama haina haja ya kuwepo isiwepo, lakini kama kuna haja ya kuwepo, basi hizi halmashauri ambazo hazipeleki zipeleke ili iweze kujiendesha. Hii ndio ingeweza kuwajengea

uwezo hawa halmashauri, hii ndio ingeweza kuwajengea uwezo Madiwani wetu ili waweze kufanya kazi vizuri, hawajachanga, hawajapeleka, ofisi iko pale na mimi huwa napita pale karibu kila siku, ni njia ya kule naona kibao *ALAT,* pale ipo, lakini hii ni ofisi ambayo imekusanya asilimia tisa tu ya mapato yake kwa miaka karibu nane, inawezaje kujiendesha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye maazimio yetu ni vizuri kuweka mkazo kwenye zile taasisi ambazo zilitarajia kuchangiwa na hazikuchangiwa na ambazo haziwezi tena kujiendesha ili ziweze kufanyiwa tathmini na kuona uhitaji wake na kuona namna zinavyoweza kujiendesha, kama haziwezi kujiendesha basi maamuzi yafanyike ili zisiwepo, kwa sababu mwisho wake ni kuanza kuzalisha madeni ambayo Serikali yetu itakuja kuanza kuhangaika kuyalipa hapo baadae.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu hizi taasisi zetu. Mheshimiwa Sanga, aliyekaa alizungumza sana kuhusu *GPSA,* lakini tuzungumzie *MSD* ambayo pia imetajwa mara nyingi sana hapa. Huko nyuma nadhani kulikuwa na utaratibu wa taasisi kununua dawa *MSD*. Ikaonekana katika utaratibu huo *MSD* hailipi, Kwa hiyo ili kuweka utaratibu mzuri ikaamuliwa kwamba fedha ziende kwanza *MSD* halafu ndipo *MSD* ilete dawa. Sasa kibao kimegeuka, *MSD* inapewa hela na haitoi dawa. Kwa hiyo Bilioni 1.7 ambazo kila siku Waheshimiwa Wabunge tunalalamika, wananchi wanalalamika hakuna dawa, hizi fedha zililipwa *MSD* na *MSD* haikutoa dawa.

Mheshimiwa Spika, mwaka umekwisha, hizi fedha hazirudishwi kwenye Halmashauri na hazifanywi chochote. Kwa hiyo, kama mfumo huu ukiendelea

maana yake ni kwamba *MSD* itakuwa inapokea hela zaidi ya kile ambacho huduma imetoa. Ushauri wangu ni kwamba iangaliwe mifumo ya ulipaji, huu wa *GPSA* na taasisi yoyote inayopata fedha kwanza, iwe *GPSA, TEMESA, MSD* au taasisi yoyote inayopokea hela kwanza, mfumo wake uangaliwe vinginevyo tuweke mtu kati, kuwe na taasisi ambayo hela ile inapelekwa, ukishatoa huduma unaenda unadai, siyo umeshapokea hela unakuwa sasa unaamua wewe unachotaka kukifanya, maana yake ni kwamba kunakuwa na ugumu kwa sababu tayari umeshalipwa, umeshapokea fedha. Sasa isipoangaliwa hii mifumo, hii hali itaendelea na hii ni hali ambayo inaweza ikawa changamoto katika utoaji wa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo tuchunguze vizuri kwa nini dawa ambazo ni shida hazipatikani lakini kwenye taarifa inaonesha kuna dawa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 7.3 zimeteketezwa. Inawezekana pia kuna changamoto kwenye mfumo wa uagizaji wa dawa, kwa hiyo dawa zinapofika kwa watumiaji zinakuwa zimebakiza muda mfupi na kwa hiyo zinatakiwa kuteketezwa. Sasa taasisi hizi ambazo zimetajwa mara nyingi humu zinatufanya tuone kuna haja ya kufanya maamuzi na maazimio yatakayoweza kukomesha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, sisi umetuteua kwenye Kamati, tunakaa kule tunafanya maamuzi. Nakumbuka Kamati ya Bunge ya USEMI kwa mfano, Halmashauri zote zilikuja tukajadiliana nazo vizuri, wale ambao ni wa asilimia 10 tukawaambia. 2021 tuliwaambia asilimia 10 zote wapeleke kama ilivyopangwa, hawakupeleka! 2022 wamekuja wapo. Sasa tunawakuta ni walewale, Spika wewe umetutuma, tunawauliza tena walewale ambao

tuliwatuma iliyopita na hawakufanya lakini wanarudi tena kwetu ni walewale.

Mheshimiwa Spika, hata kama ingekuwa wewe, yule mtu ulimwambia, hakufanya, anarudi unamwambia hakufanya! Hivi keshokutwa nakaa naye namwambia tena? Sasa ntamwambiaje ten ana mtu huyo hataki kutekeleza?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja na ninaomba hatua kali zichukuliwe kwa wale wote ambao hawaitakii mema Serikali hii. Mungu awabariki sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuzungumza ndani ya Bunge hili Tukufu. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipa uhai. Namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na ninampongeza sana kwa kazi kubwa anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nimewahi kusema huko nyuma kwamba mwanadamu hupimwa kwa matendo yake, narudia tena kusema leo ya kwamba Tanzania ina Rais *smart,* Rais *intelligent* na Rais mwenye uwezo mkubwa sana wa kufanya kazi. Ushahidi wa jambo hili ni kwamba alichukua nchi hii ikiwa inakua kwa asilimia 2.2. Leo ninavyozungumza Tanzania inakua kwa asilimia 4.5, inaelekea Tano. Alichukua nchi hii ikiwa imeanza

kupunguziwa misaada ya wahisani kwa sababu ilikuwa imeshatambuliwa kama nchi ya uchumi wa kati, wahisani walikuwa wanaondoa misaada kwa kuona kama vile mtoto sasa amekuwa anaweza kujitegemea. Alichukua nchi ikiwa kwenye ugumu wa uchumi lakini ameweza kudhibiti mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hapa leo unaweza kusema kwamba Tanzania ina bei mbaya ya bidhaa. Lakini wacha nikupe *record* kidogo. Mfumuko wa bei nchini Sudan ni asilimia 285; mfumuko wa bei Nchini Kenya ni asilimia 6.7; mfumuko wa bei Nchini Uganda ni asilimia 7; mfumuko wa bei Tanzania ni asilimia 4.4. Tanzania ni nchi yenye *lowest inflation* katika nchi za Afrika Mashariki. Naomba tumpongeze sana Rais wetu kwa sababu anatupeleka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asubuhi ya leo nilikuwa napiga hesabu ya saa ambazo Mheshimiwa Rais amekwenda nje ya nchi kuitafutia Tanzania riziki. Amesafiri nje ya nchi saa 263, hivi ninavyoongea, Rais wangu yuko China anatafuta riziki kwa ajili ya watu wake. Kwa wanaosafiri kwa ndege wanaelewa maana ya saa 263. Tunastahili kumpongeza sana Rais wetu, mimi binafsi niseme jukumu langu la kwanza litakuwa ni kumlinda na kumtetea Rais wa nchi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme – na Mungu anisaidie – niseme yale ambayo naamini Mungu ametaka niseme. Nchi yangu inaumwa. Tulipoitwa na Rais Ikulu wakati ule nilisema Tanzania inaumwa *widespread Institutional failure;* mtakumbuka. Taasisi zimefeli. Nataka niseme leo ya kwamba Tanzania nchi yangu inaumwa magonjwa makubwa mawili; ugonjwa

wa kwanza ni *anemia* ya *integrity;* ugonjwa wa pili ni *anemia* ya *accountability*. Tanzania inaumwa ukosefu wa uadilifu na pili ni ukosefu wa uwajibikaji. Magonjwa haya ndiyo yamesababisha tatizo tulilonalo leo la *widespread institutional failure*.

Mheshimiwa Spika, tangu nimekuwa Mbunge nikiingia hapa ndani ripoti ya *CAG* ikija ni watu wameiba. Nilizungumza hapa mara ya mwisho nikasema na iko siku mtakuja kukubaliana na mimi ya kwamba iko sababu kubwa sana ya kuanzisha taasisi ya *monitoring and evaluation*. Mheshimiwa *Engineer* Ulenge huwa anazungumzia suala hili sana, na mimi ninataka kusisitiza, watu wanaiba. Sasa siyo kwamba hatuna watu waaminifu, wapo! Lakini katika asilimia kubwa ya watu wetu uadilifu na uwajibikaji umemomonyoka sana.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika Taifa hili niseme bila kupindisha maneno, tumefika mahali inaanza kuaminika kwamba mtu asipokuwa mwadilifu ni *hero*. Tanzania mtu asipokuwa mwadilifu ameanza kutafsirika kama *hero*. Kwamba alikuwa Mtumishi wa Umma akajenga ghorofa Nane, akanunua mashamba makubwa, sasa ameacha kazi anaonekana alikuwa *smart,* na watoto wake wanasema Baba yetu alikuwa Kiongozi, alikuwa *very smart*. Kumbe mwizi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yule aliyekuwa mwaminifu sana kwa Taifa lake, akaitumikia Tanzania kwa akili yake yote, kwa uaminifu, akaondoka kazini maskini, wakati mwingine amemwagiwa tindikali kwa sababu alikuwa *TRA* hataki kupokea rushwa, leo hii anateseka wanasema Baba yetu alikuwa Serikalini lakini alikuwa mjinga. Hatuwezi kuwa na

Taifa ambalo wezi wanaonekana *heroes.* Hatuwezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nipongeze sana Bunge leo, tangu nimeingia hapa ndani Bunge la safari hii nimefurahi sana. Natamani Bunge hili liendelee kama lilivyo hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka huko nyuma nilikuwa nawaambia kuna na Bunge la *Speed and Standards.* Natamani Bunge hili liwe la *Quality and Perfection,* chini ya uongozi wako ujipatie sifa ya kuwa na Bunge la 12 la *Quality* na *Perfection* ambalo tunakuja hapa kusimamia mambo bila hofu wala woga, tumsaidie Rais wetu aweze kuongoza Taifa letu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tutibu tatizo la *integrity* na uwajibikaji ndiyo maana tuko hapa, ndiyo maana tumeaminiwa na Watanzania wote tuje hapa tutibu tatizo hili. Taasisi za dini BAKWATA, *Episcopal Conference* na *CCT,* walim-*hire* marehemu Prof. Ngowi ili afanye utafiti kuonesha ni kiasi gani cha pesa kinapotea kila mwaka, ripoti hiyo nimeisoma ina kurasa 64.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inapoteza karibu Dola Bilioni Moja kila mwaka kwenye mapato yake kwenye mikono na mifuko ya watu wasiokuwa waaminifu. Lazima tuzuie mambo ya namna hii. Sitaki kupita kwenye *details* za kwamba ripoti ikoje, yameshasemwa yote hapa, kila mtu anasema ni madudu, ni wizi na wizi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nami naungana na wote waliozunguma. Nilimsikia Kaka yangu Mheshimiwa Tarimba akiongea jana kwa uchungu, nikamsikia Dada

yangu Mheshimiwa Kapinga anaongea kwa uchungu; na wote wameongea kwa uchungu kwamba tunaibiwa. Nasi kazi yetu kama Wabunge ni kuisimamia Serikali yetu tuzuie fedha zisiibiwe ili ziende kwenye huduma za jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mwanasheria unafahamu Katiba yetu imetamka na mimi nitanukuu Katiba ilivyotamka. Katiba imesema: **"***We, The People of The United Republic of* Tanzania*, do sovereignly agree that we are going to build a country under the principles of freedom, justice, fraternity and concord.*" Tumekubaliana kujenga Taifa ambalo litajengwa chini ya uhuru, haki, udugu na amani.

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia haki, haki ya Watanzania kupata huduma za afya, haki ya Watanzania kupata elimu, haki ya Watanzania kupata maji. Hatuwezi kutimiza haki hii kama watu wanaiba kiasi hiki. Ni lazima tuzuie wizi, na tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa maslahi ya muda niseme nini kifanyike. Jambo la kwanza, kuna kitabu kimoja aliandika Jack Welch ambaye anaaminika kama the *number one General Manager in the world,* aliandika kitabu kinaitwa ''*Straight from the Gut'',* akasema kuna njia mbili za kuongoza watu, njia ya kwanza ni *persuasion* (kuwasihi) ili waweze kwenda na wewe au *compassion* kuwalazimisha waende. Watanzania kwa kuwasihi hawawezekani, tuwalazimishe kuwa waadilifu, walazimishwe kuwa waadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, moja, tupandikize uadilifu kwenye mioyo ya watoto wetu. Watoto wetu

wasione kwamba wezi ndiyo mashujaa wa Taifa letu, ifanyike kwenye mitaala yetu, wazazi nyumbani watimize wajibu wa kuongea na watoto wao ili ionekane ya kwamba uzalendo, uadilifu kiwe kitu cha kwanza kwa kila mtoto wa nchi hii. Hilo likiingia ndani ya mioyo ya watoto wetu nakuhakikishia tutajenga Taifa la watu ambao watalipeleka mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tukimalizana na watoto, sisi watu wazima tulioshindikana – rafiki yangu, Mheshimiwa Dkt. Ntara, amenipa maneno hapa, yanasema hivi: Waarabu wanao msemo unasema: '*Yamshillah Jabari illah jadhaa*' ikiwa na maana kwamba punda haendi bila bakora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingekuwa ni maamuzi yangu Shigongo ningetangaza tuwe na siku ya uchapaji bakora Kitaifa. Fimbo zitoke Mbeya, wachapaji watoke Tarime halafu tukutane Uwanja wa Jamhuri siku ya uchapaji bakora Kitaifa. Unakuja pale na mke wako na watoto wako kama siku ile ulipokuwa unaapishwa, halafu unatajwa, Hamisi Taletale, unakwenda mbele, unachapwa, ili tujenge jamii ya watu wanaoogopa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hatutaki kuwachapa watu wetu, tumepitisha Sheria Tano katika Bunge hili, sheria ya kwanza ni Sheria ya TAKUKURU; Pili, Sheria ya Fedha; Tatu, Sheria ya Manunuzi; Nne, ni Sheria ya Utakatishaji Fedha na Sheria ya Tano ni Sheria ya Uhujumu Uchumu. Bunge hili limepitisha sheria hizo zisimamiwe! Kuwe na *law enforcement.* Changamoto yetu ni *law enforcement.* Tunayo sheria nzuri lakini hatuzisimamii. Kuna watu wanaishi uraiani walitakiwa kuwa jela leo kwa sababu ya

sheria hizi. Tuzisimamie sheria zetu, mwenye haki ya kuwa jela awe jela, mwenye haki ya kuwa uraiani awe uraiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Jimbo langu la Buchosa pale, nimesoma ripoti hii wametajwa kabisa kwamba wamekula Milioni 94 za bakaa. Halafu mimi naona aibu, hela za amana wamekula bila wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema maneno machache tu. Kwanza, lazima sheria zisimamiwe. Mwisho Waheshimiwa Wabunge niwaombe, neno la Mungu linasema kwenye Mathayo 12.25 ya kwamba Taifa lolote linalopingana lililogawanyika, halidumu. Nyumba yoyote inayopingana na iliyogawanyika, hufa. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu tusimame pamoja kwenye suala hili, tupambane kukomesha wezi kwenye Taifa letu, inawezekana. Utakumbukwa mbele tunakokwenda, Watoto wetu na wajukuu zetu watasema Bunge la 12 chini ya Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu lilibadilisha Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu wa Mbinguni awabariki sana. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii muhimu sana kuweza kuchangia mada yetu iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Kazi anayofanya ni kubwa nasi Bunge tuendelee kumsaidia. Nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati waliochakata taarifa hii hadi leo hii tunapojadili hapa kwenye Bunge hili kwa ajili ya kuweza kupata maamuzi na mwelekeo sahihi kwa Taarifa ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia sana *CAG* kwa sababu amefanya kazi kubwa. Taarifa yake ina zaidi ya kurasa 1,000. Ukipita, hakuna sehemu iliyo nzuri na muhimu na ambayo inaweza ikatia matumaini kwa Watanzania. Kwa kweli taarifa hii iko kwenye mitandano kwa Karne hii ya 21 ni taarifa muhimu sana. Watanzania wengi wanasoma siyo kwamba ni sisi tu tulioko hapa Bungeni, kwa kuwa wao pia wanasoma, wanasubiri mustakabali wa maamuzi yenye tija na malengo sahihi kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ya msingi sana japokuwa taarifa hii imeletwa kwetu kama Muhimili wa Bunge, kama chombo cha wananchi na kwa kuwa Watanzania wengi wanaisoma na kwa kuwa, Taarifa ya *CAG* inapokuja Bungeni, *CAG* ameshahangaika sana, tuna kila sababu ya kumpongeza kwa sababu mpaka ije kwetu ameomba vielelezo vyenye kumpa matumaini kwamba hoja hizi zinajifuta, zina usahihi na matumizi sahihi ya fedha zilizotajwa katika kurasa zote za taarifa ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, kwa kuwa alikuwa ameomba nyaraka za kuweza kuthibitisha matumizi sahihi na ikashindikana, hatimaye wakati anafunga taarifa zake amekuja kukitaka chombo hiki cha wananchi Bunge na Muhimili wa Serikali waweze kujadili na kuona maoni yake

yanafanyiwa kazi. Kwa miaka kadhaa tukiwa Wabunge tumekuta taarifa za CAG zinapokuja zinajadiliwa hapa Bungeni na hatimaye hatua zinazochukuliwa zinakuwa pengine hazikidhi na kutosheleza yale matakwa sahihi ya Watanzania na malengo wanayokusudia. Nitazungumzia mifano michache.

Mheshimiwa Spika, *CAG* anapotoa taarifa hapa yeye ameshachambua vya kutosha hivyo. Mimi siungani na wale wanao sema kwamba tuunde chombo kifanye utafiti tena. Tunachotarajia ni kwamba baada ya taarifa hii sisi kuijadili na kuisoma na kuona madudu yalivyo, matatizo yaliyojitokeza na matumizi mabaya ya fedha za umma; lengo letu kama Bunge, ninalishauri Bunge letu nakulishawishi, kwamba pengine sisi, kwa sababu wananchi wana matumaini kwetu, tuwe na maamuzi ambayo yatatoa matumaini kwao. Kwanza kuwawajibisha wale wote waliohusika kwenye taarifa hii na ambao wanaichezea mali ya umma.

Mheshimiwa Spika, vipo vyombo vya kutosha katika nchi hii kuchukua nafasi kuchambua taarifa hizi kuleta baadhi ya taasisi ambazo tayari ama wahusika wa ngazi mbalimbali wamehusika kwa namna moja au nyingine kutufikisha hapa tulipo. Kwa sababu hizi ni kodi za Watanzania na Watanzania wanataka huduma na viongozi wa nchi kama Rais na waandamizi wengine wote wanahangaika kutafuta namna ambavyo matatizo ya Watanzania yanatatuliwa; hivyo kuna kila sababu ya sisi kama Bunge kuweza kufikia maamuzi magumu kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninasema hivyo? labda nizungumze mifano michache. Mfano wa kwanza ni

fedha za *COVID 19.* Tulisubiri magari ya *ambulance* tunakaribia mwaka, fedha hizo hazijaleta magari ya *ambulance*. Kichwani kwangu au kwenye mawazo yangu nawaza kwamba hata hizi fedha pengine za kununua hayo magari ingekuwa ni watu wanafanya mchezo wa Pwagu na Pwaguzi wanaweka kwenye akaunti ya *deposit* leo hii ina shilingi ngapi? Kwa nini manunuzi yanachukua muda mrefu kiasi hiki? Hatuoni kuwa kiasi cha fedha kilichotarajiwa kununua mitambo ya magari ya *ambulance machine* za *X-rays* na mitambo mingine ya kuchimba maji na mitambo mengine kwa manunuzi ya Umma yamechukua muda mrefu kiasi kwamba kuna mchezo wa kuchelewesha huduma kwa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, hali hii inafanya Watanzania kutokuwa na imani na Bunge hili na kutuelewa vibaya. Kwa hiyo mimi nilikuwa nashukuru kama Mawaziri watakuja hapo, kila Waziri kwa kadri ya sekta anazosimamia na Wizara anayoisimamia aje na maelezo mahususi yatakayo wapa Watanzania Imani; kwanza ya kuchukua hatua lakini la pili kwa nini tunafika hapo, majibu yake yaweze kuridhisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo; kadri ambavyo *CAG* kila siku analeta taarifa hapa na sisi kila mwaka taarifa inapokuja tunakuwa tunachangia kwa kukwepa kwepa madhara yake ni kuwa tunamkatisha tamaa *CAG* na watendaji wake wote hadi ngazi ya chini. Kwa sababu yeye anafanya kazi ngumu na kazi ya kwenda kupekua watu na kazi ya kuleta taarifa hapa ni kazi ngumu, kazi ya kwenda kuandaa taarifa yenye ufafanuzi, wa kina na yenye kurasa zaidi ya elfu ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, wakati fulani, nchi hii ilipoingia kwenye tumbua tumbua hatukuielewa. Mimi nadhani hatukuielewa, sababu za kutumbua tumbua ilikuwa ni kwa kuwa wale waliokuwa wanapaswa kuchukua hatua hawakuchukua hatua kwa wakati unaofaa na kwa hivyo basi yule ambaye anamamlaka aliona ni nafuu nianze na yule aliyekaribu na mimi ili wale wengine waanze kuhofu kwamba kumbe mimi nisipochukua hatua kwa wakati basi wale wengine watachukua hatua na mimi naweza kufikiwa na janga hilo.

Mheshimiwa Spika, tutaishukuru sana Serikali, hasa Mawaziri, watakapo kuja, kwa sababu hivi punde tutahitimisha hoja hii, hivyo waje na kauli. kwa kwanza kuliomba Bunge maeneo ambayo wao wanahitaji msaada kwa Bunge, ushauri au hatua za kuchukua ili ziridhiwe kupitia sheria tulizopitisha. Pili, kuona ni kwa namna gani tatizo hili halijirudii. Tuanze na taasisi kadhaa ambazo kwa miaka mitatu taarifa zao zilikuwa chafu kupitia kwa Mkaguzi wetu *(CAG),* ili sisi pia kama Bunge tunapochukua hatua au tunapowapa wao nguvu kama Serikali basi nchi ipate unafuu na mafanikio wa yale ambayo Watanzania walio wengi wanatarajia.

Mheshimiwa Spika, hali nyingi zinajitiokeza kwa sababu ya uzembe, uadilifu na utimizwaji wa wajibu na majukumu. Haiwezekani tunachukua watendaji wabovu tunawazungusha kwenye nchi. kwamba anahama taasisi moja Kwenda nyingine ama halmashauri moja kwenda nyingine. Matatizo makubwa yanaendela katika nchi wakati nchi inawasomi wa kutosha. Ndani ya hiyo taasisi ambayo tunawahamisha hao watendaji wabovu, kuna watendaji wazuri lakini hawapewi nafasi kwa ajili ya

kulindana pengine au kujenga mfumo ambao ni dhaifu katika nchi na mfumo ambao hauna tija kwa Tanzania nchi yetu. Na sisi ipo siku ama kupitia dhamana zetu tulizopewa tutalaumiwa na kulaaniwa; au kupitia nafasi zetu kwa wananchi, wananchi watakosa imani kwetu sisi kama Bunge na Serikali yao.

Mheshimwa Spika, kwa nini nasema hayo? fedha nyingi ukizijumlisha unafika mwisho hazijumlishiki, fedha ambazo tayari zimekosa matumizi na hazijaenda kutoa huduma.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay kunataarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Muguta Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nilikuwa naomba nimpatie taarifa Mheshimiwa mzungumzaji kwamba anayosema ni sahihi. Nafikiri sisi kuhangaika na wale watendaji kule chini ni sawasawa na kufukuzana na nyuki. Sisi watu wetu ni hawa Mawaziri na Watendaji wengine Wakuu Serikalini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, mimi naipokea kwa mikono miwili *(Makofi)*. Nchi hii ina mihimiri, mimi nikupongeze sana, sisi kubebeshwa mzigo kuhangaika kule chini, mimi naungana na mtu aliyenipa taarifa. Si muda wetu sasa hivi, sisi ni chombo na chombo hiki, kiungo chetu ni Serikali na Mawaziri, wao wachukue hatua, na wao wakichukua hatua nchi inapata unafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunasema hivyo? Taarifa hii imechakatwa na kule halmashauri ilikotoka kuna mtu anaitwa mkaguzi wa ndani, na mkaguzi wa ndani atatakiwa apeleke vielelezo kwa wale ambao anawataka walete vithibitisho kwa ajili ya taarifa zenye utata. Kwa hiyo unapoenda kwenye ngazi ya halmashauri kwenye taarifa za halmashauri huko, zile halmashauri zinazofanya vibaya zilishapewa muda wa kupeleka nyaraka za utetezi ili mwisho wa siku hoja zao zifutwe. Hadi tunaletewa huku, walishashindwa, hawakupeleka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hawakupeleka Mkaguzi Mkuu *(CAG)* hawezi kuacha kazi yake, ni lazima alete taarifa yake kwetu sisi kama Bunge na chombo cha wananchi na muhimiri Serikalini kuelezea hali halisi ya taasisi zilivyo. Kwa hiyo kule zilishadaiwa zifutwe kwa nia ya kwamba nyaraka zipelekwe lakini zimeshindikana, hapa zimekuja mahakamani ili zihukumiwe, kwa sababu umepewa nafasi ya kutetea hukutetea umepewa muda hukutumia vizuri. Sasa ni wakati wa chombo hiki kuamua ili Watanzania wapate amani.

Mheshimiwa Spika, si kwamba tuna chuki sana na Mawaziri lakini kadri unavyochelewa kuchukua hatua basi tatizo linakuwa…

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nimpe taarifa mzungumzaji, kwamba ukweli sasa hivi inatakiwa tuchukue maamuzi magumu. Nitatoa mfano kidogo 2018, tuliingiziwa pesa za ujenzi wa Kituo cha Afya Nyang'wale tarehe 26 Mwezi wa 6, kufikia tarehe 1 mwezi wa 7 milioni 400 zikawa hazijulikani zilikokwenda, na hadi leo hii watu hao wako mtaani wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. Nilikuwa nataka kumpa taarifa Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay umepokea taarifa hiyo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa mikono miwili. Fedha milioni 400 anazozizungumza mtoa taarifa ni kodi za Watanzania; na fedha hizo kwa kuwa hazionekani ziliko halafu bado wale watu wako wanaendelea; na tunatunga sheria hapa za utakatishaji wa fedha, matumizi mabaya ya fedha na Sheria nyingine nyingi kama vile za manunuzi halafu hatuzisimamii. Tunaendelea kupiga kelele na kodi za Watanzania zinatumika kulipa vikao hivi vya Bunge na gharama za uendeshaji wa Bunge, je tunaitendea haki nafasi yetu kweli?

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani pamoja na sababu nyingi zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, mimi niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi hiki cha kujadili taarifa hii tumetendea haki nafasi zetu kwa hali ya juu sana. Hii ni kwa sababu sisi ndio tunaosubiriwa tuseme ili nchi ipone, na sisi ndio tunasubiriwa tuseme kwa niaba ya Watanzania milioni 60. Tunakwenda wapi kama endapo tunaanza kukwepa

maamuzi magumu ambayo yataisafisha nchi na yataiweka nchi mahali pazuri?

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe Wabunge wenzangu tuungane kwenye hoja hizi na tutazame kwa kina maslahi mapana ya taifa letu, tuweze kuzungumza tukiwa Wabunge kama sehemu ya Watanzania na hatimaye maazimio tunayoazimia hapa kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zetu za Bunge na Sheria nyingine za nchi yaweze kuwa na tija na kuhakikisha nchi yetu inapata ahueni na mafanikio ya maendeleo yanapatikana.

Mheshimiwa Spika, mengi yatazungumzwa lakini hatima yake, tunapo kwepa maamuzi magumu yote tuliyo yazungumza hayatakuwa na tija. Ili yale tuliyazungumza yawe na tija, na taarifa zimeletwa hapa na zimeeleza madudu ya kila sehemu, tuchambue kadhaa tuchukue hatua, tuweze kunoa Sheria inasema nini na wajibu wetu ni nini ili hatimaye nchi iweze kubadilika. Vinginevyo, kila mwaka CAG atahangaika kuleta taarifa hapa, taarifa zake atakazoleta hapa, hatutampa matumaini na hatutaona kama ni sehemu muhimu, na mwisho wa maamuzi yetu yatadharauliwa na Watanzania milioni 60.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja, mchano wangu uishie hapo.

**SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Edward Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi; na niungane na Wabunge wengine kukupongeza kwa unavyouendesha mjadala huu. Kwa kweli kama kuna mjadala ambao umefanyika kwa ufanisi sana. Ni mjadala huu wa ripoti ya *CAG;* na si kwa bahati mbaya, kwa sababu hii ndiyo imebeba kila kitu cha nchi hii, kwa hiyo nikupongeze sana, *I am very proud, as your student, I am very proud. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati hizi zote tatu, *LAAC, PIC* na *PAC,* kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana, na ni kazi ngumu kwelikweli. Mimi nadhani mwaka mmoja uliopita halmashauri yangu iliitwa kwa hiyo nilishuhudia mahojiano kati ya Kamati yetu ya *LAAC* na halmashauri; inafanana kabisa na *process* zile za *cross-examination* za mahakama, ni nzuri sana. Kwa hiyo kwa kweli tuwapongeze sana.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuangalia zile ripoti zota za CAG, takriban repoti 17, kama zote tutazifuatilia, *pages* 3,632. Hii maana yake nini? Ni kwamba, huko mbele ili tuweze kupata muda mzuri wa kuchangia vizuri, labda pengine tuangalie pia muda ili Wabunge waweze kuchangia. Niwapongeze Wabunge wale wote ambao wamepitia ripoti hizi, kwa kweli kazi nzuri sana wamefanya.

Mheshimiwa Spika, mimi nazipongeza pia halmashauri zilizofanya vizuri. Wale ambao wamefanya vibaya tuweze kuwasema sana. Tusipo shughulika na wale wanaofanya vibaya inaondoa uzalenda wa wale wanaofanya vizuri, kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Shigongo. Lazima wanaofanya vibaya waadhibiwe.

Mheshimiwa Spika, Jaji mstaafu wa Kenya aliwahi kusema hivi, "*the greatness of any nation lies in its fidelity to the its constitution and adherence to the rule of law but above all respect to God*".

Mheshimiwa Spika, *CAG* ameshafanya kazi yake ya kikatiba na ameonesha madudu ambayo yamefanyika kila mahala. Kazi iliyobaki ni ya Bunge. Bunge liko kwenye *trial* wanasubiri sasa kuona Bunge litachukua maamuzi gani. Kwa hiyo, kwa kweli tufanye maamuzi ambayo yatasaidia nchi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema Wajumbe wengine hapa, Mheshimiwa Rais anafanya kazi nyingi sana, anahangaika kila mahala  kutafuta pesa kwaajili ya miradi ya Tanzania. Lakini ukisoma ripoti hizi, na ukaangalia mfano tu wa zile fedha alizotafuta kwaajili ya miradi ya *UVIKO,* ilivyoleta heshima kila mahala nchi hii, halafu unaambiwa ni TirionI 1.3 tu; lakini ukisoma ripoti hii unaambiwa kuna zaidi ya Tirioni 1.8 zimepotea. Maana yake kwamba, kama hizi fedha tungeweza kupeleka kwenye miradi mingine heshima yetu ingekuwa kubwa zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu kimenisikitisha sana kama unakuta unaambiwa eti kuna halmashauri 47 wamenunua dawa zimeharibika. Fedha zimetumika na maisha ya Watanzania tunayaweka kwenye wakati mgumu wa kuwa na dawa ambazo zimeharibika, *this is shame*. Kwa hiyo si tu kwamba fedha zao zimepotea lakini wanaweza pia wakapata madhara ya afya kutokana na dawa ambazo zimeharibika.

Mheshimiwa Spika, nilitaka pia kupata *clarification* kwa ripoti hii ya *CAG,* ukurasa wa tano. Kwenye ku-*summarize* zile *recommendation*, wanazosema 10,824 kwenye jedwali namba mbili wanasema utekelezaji unaendelea kwa *recommendation* 10,864.Lakini *paragraph* iliyopo juu hapo, wanasema mapendekezo 1,864 sawa na asilimia 17 hayajatekelezwa, lakini ukiangalia kwenye chati ambayo hayajatekelezwa ni 3,637, nadhani hiyo *confussion* lazima iwe *clarified* ili tujue. Kwa sababu hapa ni kama ime *swap* kidogo.

Mheshimiwa Spika, habari za halmashauri zimezungumzwa hapa na sisi tunakutana hapa kama wawakilishi wa wananchi, na kila mahala tunakokwenda hakuna maji, hakuna barabara, hakuna zahanati hakuna vituo vya afya, madarasa, madawati halafu ukiambiwa kuna fedha zinapotea na watu wapo na Sheria zipo ni hatari kidogo.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ripoti hii, Mheshimiwa *Attorney General* ambaye kwa kweli namheshimu sana, *I think is the only man,* amekuwa *DPP* amekwenda *judicial* na Sasa ni *Attorney General* na *is the most qualified, by the way*. Naomba ulisaidie Bunge hili, *next* ripoti tusipate ripoti inayo tokana na mikataba ambayo inafungwa fungwa kwa ajabu ajabu. Bunge hili lilifanya mapinduzi ya sheria kwa kufanya wanasheria wote kuwa chini yako, hata wale wa halmashauri, nadhani nia ilikuwa ni mfanye *quality assurance* ili walau basi yale yanayotokana na mikataba mmusaidie *CAG* ili ripoti ijayo isiwepo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *TAMISEMI,* na ripoti imezungumzwa hapa, kwamba hamrejeshi fedha, na sijui kama Waziri wa *TAMISEMI* yuko hapa. Nakushukuru na

nakupongeza sana, ulisema unataka kuweka misingi ili wanao kufuata wakutane na misingi hiyo. Sasa, kuna suala linatusumbua kila wakati, kutorejeshwa kutoka hazina pesa mnazochukua kwa kigezo kwamba mwaka umeisha. Tumeshazungumza hapa, mnapeleka fedha na hamrudishi. Kwa mfano Kiteto imechukuliwa fedha milioni nane ya mfuko wa jimbo ambayo ilitakuwa iwe imejenga darasa Zambia Kata ya Lengateu, hamtaki kuleta milioni 32 za *Basket Fund*. Mheshimiwa Waziri kama unanisikiliza hizi pesa *Monday, Tuesday Wednesday or next week* hizi fedha zije tena. Haiwezekani mnatutengenezea hoja, kesho ripoti za *CAG* zije halafu mnatuambia kwamba miradi imechelewa, kumbe ni ninyi. Tulishasema hapa mzipeleke hizo fedha. Mheshimiwa Waziri hiyo ndiyo test yako ya Kwanza.

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mambo mengi hapa, wizi takriban kila mahala, eti mpaka kwenye Balozi zetu; *that is how desperate we area*, mpaka kwenye Balozi. Sasa ukiona madudu yanafanyika mpaka kwenye Ubalozi basi ujue kwamba tuko *desperate* sana.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *CAG* inatuambia, kati ya maagizo ya Bunge hili 619 kwa mamlaka 99 eti kuna maagizo 264 ya Bunge lako hili hayajatekelezwa. Sasa ndiyo tutashangaa zile za Waziri wa Elimu na Bodi ya Mikopo, *honestly* kama maagizo 264 ya Bunge hili hayatekelezwi!

Mheshimiwa Spika, nimesoma ripoti ya Bodi ya Mikopo inasikitisha sana, kwamba wananchi masikini hata wale wanaotokana na familia za *TASAF* ambao kimsingi walitakiwa kuwa na dirisha maalum, wanakosa mikopo. Watoto wa wakulima, watoto wa *single parent* eti

wanakosa mikopo. Mwalimu Nyerere alishasema hapa, ukitaka kumsaidia mtoto wa masikini, mpe elimu. Elimu haizuii umasikini, lakini ni silaha ya kupambana na umasikini. Sasa tusipoweka fedha kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wetu, watapambanaje na umasikini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, hiyo kengele ni ya mwisho, siyo!

**SPIKA:** Ni ya pili. Nakupata dakika mbili, malizia.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kweli hili la Bodi ya Mikopo, nashukuru sana kwa maazimio ya Bunge yaliyofanyika juzi. Wanafunzi wanahangaika kila mahali, wanatusumbua sisi Wabunge; "napiga simu hapa niangalie kama nitapata mkopo." Wanafunzi ambao hali zao wanatoka kwenye familia ambayo ni masikini sana. Inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno yangu ya mwisho kabisa, kwa sababu ni lazima tutengeneze majawabu. Nilikuwa nasoma kitabu fulani hapa. *Institute* inaitwa, *Wajibu Institute of Public Accountability*, wanasema hivi, naomba ninukuu, kwa sababu inaweza ikatusaidia mbele huko.

*"Naombeni ushauri, Serikali kuiwezesha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani kuwa na fungu au Vote ili kumjengea uwezo na kufanya kazi zake kwa uhuru zaidi. Aidha, wajibu wa kumshauri Mkaguzi Mkuu wa ndani awe anapeleka taarifa hizi kwa Katibu Mkuu Ikulu ili taarifa*

*zake zimfikie kwenye Baraza la Mawaziri ambalo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwenyekiti wake. Ripoti hii ikimfikia Rais kabla ya Septemba, tarehe 30, ambapo itakuwa ni miezi tisa baada ya mwaka wa fedha wa Serikali kumalizika, hii itampa fursa Mheshimiwa Rais kujua hali ya utendaji wa Serikali kabla ya ripoti ya CAG.”*

Mheshimiwa Spika, nadhani hili likichuliwa pengine linaweza likasaidia ku-*improve* ripoti huko mbele. Nakubaliana na maagizo yote na ripoti zote mbili, naomba Bunge hili sasa lionyeshe kazi yake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye taarifa hizi tatu ambazo zimewasilishwa na Wenyeviti wetu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, hivi vitu wakati mwingine vinalitia simamzi sana Taifa letu. Mambo haya ya ubadhirifu ambayo yanaendelea kwenye Taifa letu ni kitu cha ajabu sana na kinakwenda kutukatisha tamaa Watanzania hata kwenda kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo huko chini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa kawaida kule chini, akiiba kuku anakamatwa, anapelekwa Mahakamani,

anasomewa shtaka, anahukumiwa. Leo Mtanzania aliyesoma kwa kodi za akina mama kule chini; wapika pombe, wakulima wanahangaika kutafuta mbolea kwa shida, kasomeshwa na kodi hizo, amepata nafasi ya kulitumikia Taifalake, anaenda kuweka ubinafsi wa hali ya juu kwa kuweka fedha zote kwenye mfuko wake na tumbo lake, na bado sisi kama Taifa tunamwangalia, hatujitendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaomba nizungumzie mchango wangu kwenye suala zima la tozo zinazotozwa kwa ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi kwenye miradi mbalimbali ya Serikali. Tunafahamu fika kwamba Serikali huwa inaandaa bajeti; wataalam wetu huko wanatuandalia bajeti, wanatuletea ndani ya Bunge ili tuweze kuijadili bajeti na tuweze kuona kwamba, kutokana na mradi fulani bajeti tuliyoletewa inakidhi mahitaji? Kama haikidhi tuishauri Serikali kuongeza ama kama inakidhi na kubaki, tushaurI Serikali na kupunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachonishangaza, kama Serikali huwa inaleta bajeti, tunajadili hapa, nao wanatuhakikishia kwamba itakwenda kukidhi mahitaji ya kukamilisha mradi, badala yake mradi ule haukamiliki. Mbaya zaidi, miradi hiyo, wao ndio wanaoenda kuingia mikataba na Wakandarasi. Kwenye mikataba hiyo kuna kipengele ambacho kinasema, ukichelewa kumlipa Mkandarasi utatakiwa kumlipa faini ya kumcheleweshea fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha kwenye miradi mbalimbali imeendelea kucheleweshwa kutolewa kwa Wakandarasi wetu wanaotekeleza miradi mbalimbali. Nitasema

baadhi ya miradi hapa. Inapocheleweshwa, tukitozwa zile tozo tunakimbilia kwenda kulipa zile faini, tunaacha kwenda kuhangaika kupeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi hapa tukisema kuna dili linalochezwa baina ya mlipaji na mlipwaji tutakuwa tunakosea? Miradi haipelekewi fedha, haikamili, tunaletewa tozo ya kulipa kwa ajili ya ucheleweshaji wa malipo, tunakimbiila kwenda kulipa hiyo tozo. Kwangu binafsi naona kwamba kuna mchezo ambao tunachezewa na wataalamu wetu ndani ya Serikali wa kuchelewesha kwa makusudi kabisa; kwa sababu sisi kama Bunge, bajeti tunakuwa tumeshawapitishia. Kwa hiyo wanafanya makusudi wasipeleke zile pesa za utekelezaji wa miradi ili waweze kupata *channel* ya kwenda kupiga fedha kwenye tozo kule.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mifano michache kwenye suala zima la ucheleweshaji wa ulipaji wa Wakandarasi, tozo ambazo tumetozwa. Daraja la Kigongo - Busisi kwa taarifa ya *CAG* tumetozwa faini ya Shilingi bilioni 1.5 kwa kuchelewesha kumlipa Mkandarasi. *SGR* halikadhalika, tumetozwa faini ya Shilingi bilioni 8.9. Yaani hizi tozo zote tunatozwa. Sisi tunahangaika huku hatuna mbolea; hatuna watumishi maana hatuwezi kuwalipa mishahara, tumeshindwa kuajiri; hatuna maji leo, tunashindwa kuchimba visima, hata kuleta maji kutoka Ziwa Victoria tu yafike hapa Dodoma; watu tunakuwa na foleni ya migao ya maji, lakini kuna watu, washikaji wako hapa wanapiga hela, wamekaa kimya na tunawaangalia, wala hatuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, kwa kuchelewesha tu kuwalipa fidia wananchi waliokuwa wanapisha ule mradi, zaidi ya kaya 1,125 tumelipa zaidi ya Shilingi bilioni 22 kwa Mkandarasi. Hivi vitu ni kwa nini nchi hii? Ni kwa nini Tanzania yetu hii? Halafu tunatoka tunaenda kuhangaika nje huko, wakati tuna hela ziko hapa, watu wanazichezea pasipo kuwa na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija Mamlaka ya Ndege halikadhalika tumepigwa faini ya Shilingi bilioni 11.3. Hizi fedha ukizijumlisha hapa nyingi ambazo zingetusaidia kama Taifa kuondoa changamoto mbalimbali tulizonazo ndani ya Taifa letu na tukaishi maisha ya kutokwenda kuhangaika barabarani huko kuombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na Mawaziri wanaosimamia baadhi ya Sekta. Mwaka 2021 tulipitisha tozo, Watanzania wakati wanalalamika kuhusiana na suala la tozo kuna watu walijitokeza wakasema kama hawawezi kulipa hizo tozo, wahamie Burundi, sijui wahamie wapi? Ila kuna watu wako humu wanapiga hizi fedha, hatushughuliki nao, wala hatuwajibu majibu ya namna hiyo. Hivi nikisema kwamba tunakula nao, nitakuwa na shida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtanzania wa chini kule anajihangaikia mwenyewe, tunahangaika naye, tunamkamua mpaka dakika ya mwisho, mpaka tone lake la mwisho la damu, halafu kuna watu fulani tu hapa wapo, wala hawana shida, wanakula bata, wanaendesha magari mazuri wakati kuna mama zetu huko vijijini wanatembea kwa miguu zaidi ya kilometa 20 mpaka 30 kwenda kutafuta maji. Watoto wetu wa kike

leo kwa kushindwa kuwasogezea shule karibu, wanatembea umbali mrefu kwenda kutafuta shule, wanabakwa, wanapata mimba za utotoni, wanapata maradhi, tuko hapa, watu wanapiga hela, tunawapigia makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge hili leo likafanye maamuzi yatakayoleta maslahi mapana ndani ya Taifa letu kwa kuokoa fedha zinazokwenda kuteketea kwenye maeneo ambayo hayana sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia suala la fedha za maendeleo, asilimia 40 kwa halmashauri ambazo zina mapato ya chini na asilimia 60 kwa halmashauri ambazo zina mapato makubwa. Fedha hizi nazo zimekuwa kizungumkuti. Leo fedha zinazotumika kukamilisha miradi ya maendeleo kwenye majimbo yetu ni fedha ya Mfuko wa Jimbo, fedha ya Mbunge. Lakini fedha ya makusanyo ya ndani kwenye halmashauri, Wakurugenzi wetu wamekuwa hawapeleki kwenda kukamilisha miradi mbalimbali ambayo wananchi wanajitolea kule chini. Hivi vitu navyo siyo vya kuvifumbia macho. Naomba tuchukue hatua stahiki kwa wale watu ambao mapato yao yanawaruhusu kwa mujibu wa sheria kuchukua fedha ya asilimia 40 kwenda kumalizia miradi mbalimbali inayotekelezwa na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nilisemee suala la mbolea. Namshukuru Mheshimiwa Waziri ametoa ufafanuzi hapa. Pamoja na ufafanuzi alioutoa Mheshimiwa Waziri kwamba hawawezi kuifikisha mbolea kwa wananchi wetu kule chini, wameiweka hapa mjini; hivi mjini hapa ndiyo kuna wakulima? Jana wakati naangalia taarifa ya habari, kuna mwananchi mmoja

Songea amefariki akiwa kwenye foleni anasubiri mbolea. Kapanga foleni, ameanguka chini, amekufa pale kutokana na msongamano wa kwenda kutafuta mbolea. Ametoka huko kijijini kwao, ni mbali, amefika pale, foleni ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa tunachomwomba Mheshimiwa Waziri, hao Mawakala wake ambao amewapa hiyo kazi ya kusambaza mbolea, mbolea hii isikae Makao Makuu ya Wilaya ama kwenye hivyo vituo. Tuwapelekee wananchi wetu, tuwasogezee angalau kwenye Makao Makuu ya Kata ambapo kwanza tutapunguza msongamano mkubwa; pili, tutawasaidia wananchi kutembea umbali mdogo kuja kufuata hiyo mbolea kwenye hayo maeneo. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika,…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hussein Amar.

**T A A R I F A**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nimpe taarifa Mheshimiwa Majala. Kufariki kwa yule mwananchi akiwa kwenye foleni akisubiri mbolea, hiyo ni ahadi ya Mwenyezi Mungu, na siyo sababu ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana Mzee Hussein, sana, sana. Huyu mtu ingekuwa ni ahadi yake, angefia huko nyumbani kwake. Hata kama alikuwa na maradhi yake, laiti ile foleni isingekuwepo na ule msongamano; na tunafahamu Watanzania wengi kwenye suala la afya pia sio watu ambao tuna utamaduni wa kwenda ku-*check* afya zetu. Yule mtu hata kama alikuwa na maradhi yake na kwamba ahadi yake imefika, lakini katika yale mazingira, chanzo kilichoripotiwa ni mkulima kufariki kwenye foleni ya kutafuta pembejeo, kwa maana ya mbolea na siyo kitu kingine chochote. Kwa hiyo, kama ilikuwa ni ahadi ama haikuwa ahadi, kafia kwenye foleni ya kutafuta pembejeo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Kama unamtetea mwanao, *well and good,* siyo mbaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kumpa mwenzangu taarifa. Kwanza nimpongeze kwa mchango wake mzuri wenye *input* nzuri sana. Ila kwa anachokizungumzia, kwa sababu tunazungumza kwenye Bunge na huwa sababu za vifo haviamuliwi na magazeti, mtu unaweza ukafa ukitembea, unaweza ukafa ukifanya chochote, lakini sababu iliyopelekea kifo ni *clinical.* Kwa hiyo, namwomba, inawezekana anataka kuonesha uzito

wa jambo analolisema, lakini sababu ya kifo haiwezi kuwa kukaa kwenye foleni.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, unapokea taarifa hiyo.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge, hatuna sababu za kuanza kuvutana, ila mtu amekufa akiwa kwenye foleni ya kusubiri mbolea. *(Makofi)*

*(Hapa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Alisimama)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 71(1)(a) Wabunge hatupaswi kutoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, taarifa gani haina ukweli? *(Kicheko/Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya kifo; kifo cha binadamu huthibitishwa na daktari na vile ville kifo cha mashaka kimetolewa mwongozo kwenye kifungu cha 7 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai. Kwa hiyo, mchango wake inawezekana yeye ana taarifa ambazo ni za upande mmoja, lakini mwenye kuthibitisha *cause of death* kwa mujibu wa *postmortem examination report*

Kifungu cha 8 huwa inatajwa pale. Kama haijatajwa haiwezi ikawa taarifa ambayo inakuwa *classified* kuweza kutolewa kwenye mamlaka na kufanyiwa kazi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, akatupeleka kwenye Kanuni ya 71 fasili ya (1) ambayo inazungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Pia ametupeleka kwenye mchango wa Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ambapo wakati akichangia alikuwa anaeleza namna ambavyo kuna changamoto kwenye jamii kwa maana ya upatikanaji wa huduma kwa sababu ya taarifa ambazo zipo za CAG na namna ambavyo kuna upotevu wa mapato ambayo yangeweza kusaidia kwenye hayo maeneo mengine. *(Makofi)*

Sasa hapa jambo ambalo halibishaniwi ni kwamba mtu ni kweli amefariki; na huyo mtu amefariki akiwa kwenye eneo ambalo linatolewa mbolea. Ikiwa hilo siyo linalobishaniwa, kwa sababu mimi katika kusikiliza; maana la sivyo itabidi niitishe Taarifa Rasmi za Bunge; sijasikia kama anasema kilichosababisha kifo ni foleni ya mbolea. Anachoeleza ni eneo alilofia huyo Mtanzania. Ni kwamba eneo alilofia ni eneo la kusubiri mbolea. *(Makofi)*

Sasa kama kuna taarifa yoyote, pengine kama huyo mtu hajafa, moja; la pili, kama amekufa na hajafia pale ambapo mbolea inatolewa, labda hilo ndilo linaweza kubishaniwa. Ila kwa maana ya kwamba mtu amefariki na amefariki sehemu ambayo mbolea inatolewa, hiyo siyo sababu ya kifo, lakini ni kwamba amefia pale. Eneo ambalo amefia ni la kusubiri mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kunti Majala, kwa sababu hapa nilikuwa sijaombwa mwongozo, ndiyo maana hamjasikia nikisema mwongozo, lakini ilikuwa inatolewa taarifa ili mchangiaji apokee taarifa vizuri. Kwa hiyo, lazima niliongoze vizuri ili hiyo taarifa iwe imetolewa kwa namna inayostahili. *(Makofi)*

Kwa hiyo Mheshimiwa Kunti Majala, kwa sababu sijaitisha Taarifa Rasmi za Bunge hapa, mimi ndivyo nilivyosikia. Ila kama umesema kwamba yule mtu amefariki kwa sababu ya kusubiri mbolea, nadhani hata gazeti litakuwa halijaandika sababu ya kifo, ila limeandika eneo ambalo huyo mtu amefia.

Mheshimiwa Kunti Majala, endelea na mchango wako.

**MHE. KUNTI MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kutoa huo ufafanuzi vizuri na naamini ulinisikia vizuri na umenielewa vizuri. Wabunge ni lazima tuwe watu ambao tunasikiliza na kutafakari ili tuweze kuchukua maamuzi. Hizi biashara za kuwa tunateteatetea na kujizingazinga na kutaka kufichaficha vitu, unaficha kitu gani wakati kitu kiko hadharani? Ndio maana tunaendelea kuibiwa humu ndani ya Taifa letu kwa sababu ya kubebanabebana kusikokuwa na tija na kuteteanateteana kusikokuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa na naomba niishie hapo kwa mchango maana yake naweza nikaendelea kuharibu hali ya hewa aaidi. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa Fedha Na Mipango, ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwe sehemu ya kuchangia taarifa hizi tatu za Kamati zetu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwa mzima na kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. Nizipongeze Kamati zote pamoja na Wenyeviti wa Kamati kwa kuwasilisha taarifa zao vizuri ndani ya Bunge letu hili.

Mheshimiwa Spika, kipekee nikupongeze Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuweka rekodi mpya ya namna Bunge lako linavyojadili ripoti hizi ni mwaka huu tarehe 16 Februari, 2022 siku moja tu ilitumika kujadili ripoti zote hizi tatu, lakini mwezi huu Novemba kwa maboresho kidogo na kwa ridhaa yako Bunge lako linatumia siku nne kujadili ripoti hizi tatu inaonesha ni namna gani tunakwenda kuweka Bunge la Kumi na Mbili, pengine Mungu atajalia litaweka historia ya kuisimamia Serikali kwenye mapato na matumizi ya fedha ambazo zinaidhinishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa kazi nzuri inayofanyika ambayo inaonekana waziwazi kwa taarifa ya utekelezaji wa bajeti iliyoishia Juni, 2022. Taarifa ile ilionesha Serikali ilikusanya zaidi ya 95% ya mapato ya ndani trilioni 24.3, taarifa ile ilionesha kuna ongezeko la zaidi ya trilioni 3.8 kwa bajeti iliyopita iliyoishia Juni, 2021, lakini taarifa hii ilionesha kwamba pesa nyingi zimepelekwa kwenye miradi kutokana na mapato ya ndani zaidi ya tirioni 11.55,

99.7% na ni kwa mara ya kwanza imevuka lengo hilo na ukilinganisha na trilioni 8.34 zilizopelekwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri hii ndio maana naifurahia hatua yako hii, tusipoweka msingi imara wa kuisimamia Serikali tutakwenda kushuhudia upungufu unaoendelea kujitokeza kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hapa nimpongeze kwa dhati kwa kazi yake nzuri. Mwezi Agosti mwishoni uliruhusu Kamati zako nne ya *PAC, PIC, LAAC* na Bajeti kupewa semina na Taasisi ya Wajibu ambayo ilihusu ripoti ya uwajibikaji. Katika ripoti hiyo ilifanya kazi ripoti zote za *CAG* na taarifa yake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja zote za *CAG,* ziwe za mapato, ziwe za matumizi, ziwe za manunuzi na yote, zote zile ukizisoma zina viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu na ndio maana taasisi hii inayoongozwa na *CAG* mstaafu Ndugu Ludovick Uttoh ilifanya tathmini ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa viashiria vya rushwa, udaganyifu na ubadhirifu ambao taarifa hii ni kwa ajili ya *CAG* kwa mwaka 2018/2019 ilikuwa jumla ya bilioni 232.5. Kwa mwaka 2019/2020, ilikuwa jumla ya tirioni 1.77. Kwa mwaka 2020/2021 viashiria hivyo kwa ripoti ya *CAG* ni trilioni 4.5, zaidi ya 15% ya matumizi yote ya trilioni 31.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni ongezeko la 159% kutoka mwaka wa fedha 2019/2020 ambao kiuhasibu tunaita yote hayo ni *nugatory expenditure* na ni viashiria gani? Ni mapato kutopelekwa benki, kukosekana kwa hati za malipo, kutumia hundi za malipo

zilizoghushiwa, kufanya malipo kinyume na matakwa ya Sheria Kanuni na Taratibu za Manunuzi, malipo ya huduma au bidhaa ambazo hazijapokelewa, malipo kwa watumishi hewa, malipo kwa Wakandarasi ambao hawajulikani.

Mhwshimiwa Spika, hakuna taarifa yoyote ambayo itapelekea matumizi haya au hoja hizi ni rushwa, ubadhirifu na udanganyifu. Katika vigezo vyake alivyotumia katika hiyo taarifa ya wajibu ambayo imesambazwa katika taasisi mbalimbali za ndani na za nje na Mabalozi mbalimbali inaonesha kwa mwaka 2020/2021, kati ya viashiria vya trilioni 4.9, viashiria vya upotevu wa mapato ni trilioni 1.8. Viashiria vya matumizi ya kawaida, usimamizi wa mishahara, mafao na rasilimali watu trilioni 1.1, viashiria vya matumizi ya Mikataba kinyume cha taratibu na kanuni ni trilioni 1.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Kamati na maazimio ya Bunge naomba mimi binafsi nishauri azimio lingine mojawapo. Ikikupendeza, kwa kuwa tunataka tuweke rekodi na kwa kweli inaonekana ni dhamira ya Serikali yenyewe tupendekeze kuundwa kwa Kamati Teule ya kuangalia kwa nini kunakuwa na ongezeko la hoja za ukaguzi. Sitaki kuamini wataalam ndani ya Serikali ni wengi, Wahasibu waliosoma, wenye *CPA*, wenye *MDA*, Maafisa Masuuli lakini ongezeko la 159% la mapungufu ya usimamizi wa fedha ya mapato na matumizi kutoka trilioni 1.7 mpaka trilioni 4.9, inataka Kamati Maalum ya kuyapitia hayo na kujua kulikoni.

Mheshimiwa Spika, haiyumkiniki, ukaguzi siyo kuviziana, mimi nilikuwa Mkaguzi wa Hesabu, unaingia, unaitisha kikao, unawambia utaenda maeneo gani,

utatumia *sampling* ya aina gani. Unamaliza, unaitisha kikao unawaambia haya niliyoyaona, unarudi ofisini, unaandika *management letter,* unawapelekea, wanapewa siku 21 wajibu, unapoona kimya hizi zilizowasilishwa hapa hawakuwa na majibu. Iweje inapowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais anaiwasilisha Bungeni, zinavyoanza Kamati ndio majibu yanapatikana, huo wote ni ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende kwenye Kamati ya *PAC*, pamoja na mapendekezo ya maazimio ya Bunge, naomba niongeze azimio mojawapo namba 3.3 kuhusu ukaguzi maalum. Kwa kuwa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali upande wa Mashirika ya Umma umebainisha ubadhirifu mkubwa wa pesa za umma kwenye kaguzi maalum na kaguzi za uchunguzi, naomba tuweke waziwazi ukaguzi maalum katika Mamlaka ya Bandari, wizi wa zaidi ya bilioni 22.64, wizi wa zaidi ya bilioni 24.29, wizi wa bilioni 2.9, wizi wa bilioni 8.38 *cash* yaani *cheque* zinaandikwa zitoe *cash* hazina kiambatanisho chochote, lakini katika hilo wizi wa bilioni 64 Mamlaka ya Bandari Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 3/8/2019 Mkandarasi wa kufanya kazi ya kutengeneza sehemu ya kugeuzia meli Bandari ya Tanga alipata mkataba wa bilioni 172, ndani yake zaidi ya bilioni 104 ni kwa kazi mbili tu ya kuongeza hilo lango la kugeuza meli. Tarehe 1/8/2019 hata kabla hajasaini mkataba alifaulisha hiyo kazi kwa kiasi cha bilioni 40. Huyu mtu alichukua cha juu bilioni 60. Lazima Bunge lako liweke azimio waziwazi na hawa ndio wa kuweka kwenye orodha hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bandari imezoea ubadhirifu, ripoti ya kwanza aliyopokea Mheshimiwa Rais ya mwaka 2020 iliyoishia Juni, 2020, walikwapua bilioni 3.5, lakini ukaguzi maalum wameendelea kuonesha kwamba ni mamlaka inayokwapua pesa na bandari tunaitegemea kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwenye ripoti ya *PAC*, naomba niongeze kuhusu kaguzi maalum wamezitaja pale kama moja ya azimio la Bunge, lakini naomba iwekwe wazi pia ukaguzi maalum juu ya tuhuma za ubadhirifu wa noti Benki Kuu, bilioni 3.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia tuongeze ukaguzi wa kuchunguza malipo ya dawa za Kimarekeni kutoka akaunti ya Benki ya Mradi wa Kuongeza Tija ya Uzalishaji Mpunga wa Benki Kuu ya Tanzania zaidi ya dola za Kimarekani 298,500. Naunga mkono taarifa hizi, lakini kwa kweli Serikali na jitihada za Mheshimiwa Rais kuzunguka nchi mbalimbali hata za ndani mapato yake yanavyoongezeka na rekodi mbalimbali, lakini hazitakuwa natija kama tunawaacha na Serikali iboreshe Sheria ya Manunuzi ya Umma, Serikali iboreshe Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, iweke adhabu, yeyote anayeendelea na hoja za ukaguzi aadhibiwe kama kukatwa mshahara, kushushwa cheo…

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, kengele ya pili ilikuwa imeshagonga, lakini naona kwa sababu nilikupa muda wa kumalizia, naona Mheshimiwa anataka kukupa taarifa. Mheshimiwa Kenneth Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe mzungumzaji taarifa kwamba jana tumepata msamaha kwa nchi ya China shilingi bilioni 31. Kwa hiyo ukiangalia bilioni 60 tena zinapigwa pale Tanga kimchezo mchezo, ndio unaweza ukaona ni namna gani tupo kwenye *dilemma* ambayo huwezi kuielewa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, dakika moja malizia mchango wako, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, naipokea hiyo taarifa na ni kweli kwamba nchi yetu ukiangalia namna ambavyo ubadhirifu katika ripoti ya *CAG* tuna uwezo wa kuongeza mapato zaidi lakini hata hiyo misaada sasa ikaleta tija zaidi. Niwaombe sana watumishi wa umma, niwaombe kuwa wazalendo, haipendezi.

Mheshimiwa Spika, niwaombe pia Watanzania, ubadhirifu hauna awamu, hata sasa tunajadili miaka ya fedha iliyopita, lakini hauna awamu kwa sababu si mamlaka ndio inayotuma ubadhirifu na tunaona Wabunge tunaendelea kupongezwa kwamba mnafanya hivi na kwamba Rais awe mkali. Nataka niseme tu ni ubadhirifu wa miaka mbalimbali iliyopita, lakini tunaweka tahadhari na kwa kadri miaka ya fedha inayopita kwa kweli niwaombe sana Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali majibu yanayokwenda Ofisini kwake baada ya taarifa kufika Bungeni naomba ayahakiki vizuri, walikuwa wapi hawa wakaguliwa, wayalete sasa, kwa kweli siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ajiandae.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na kutuwezesha kuwepo kwenye majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru pia wewe binafsi kwa jinsi ambavyo umeendelea kuongoza shughuli za Bunge hili. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuendelea kusimamia Utawala wa Sheria na vile vile naamini kazi inayofanyika kwenye Mkutano huu hasa kwa hizi siku nne, ni matokeo ambayo ni ya kazi ya Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo kwa mujibu wa Ibara ya 153(4) kila anapokabidhiwa basi inawasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Ndio msingi kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ile, Sehemu ya Nne ya Kamati hizi tatu zilizowasilisha taarifa hii kuweza kuwasilisha taarifa zao pamoja na kuwezesha mjadala ambao unaendelea.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Wenyeviti wa Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao na vilevile niendelee kuwashukuru sana Wabunge kwa yote ambayo wamechangia. Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na nikimaanisha Mawaziri kwa maana yangu na kwa maana ya sheria zetu na Katiba hasa kwa mujibu wa ile Ibara ya 54. Wao ni sehemu ya utendaji kazi zinazoongozwa na mamlaka

inayotawala chini ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo Waheshimiwa Mawaziri nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya wachangiaji 70 wameshiriki kuchangia hoja ambayo iko mezani na mambo kadhaa wa kadha yamejitokeza. Wapo ambao wameeleza ni vizuri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aongezewe mamlaka na hata ikiwezekana kuendesha mashtaka ya wale ambao wanabainika kuwa wamekinzana na sheria. Pia wapo wale ambao wameona kwamba sheria zinazotolewa kwa wahusika hazifai kabisa na wengine wamependekeza adhabu za kunyongwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vilevile wako ambao wameshangazwa na kuona watu ambao kwa njia moja au nyingine wameonekana kwenye taarifa kwa kipindi husika wakiwa bado kwenye utumishi wa umma. Pia wapo ambao wameona kipindi kichotolewa kujadili taarifa hizi ni kifupi mno na hakitoshi na muda unastahili kuongezwa. Wapo vile vile ambao wamesema Halmashauri za Wilaya zifutwe na wapo ambo wametaka kuwe na *list of shame*.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hili la mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ningependa tu kurejea kwamba nchi yetu inaongozwa kwa utawala wa sheria na misingi ya utawala bora, ambapo kunakuwa na mgawanyo wa majukumu, lakini vilevile ni kitu ambacho Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepungukiwa. Tukiangalia mamlaka aliyonayo chini ya ibara ya 143, bila shaka wengi watakubaliana nami kwamba Katiba imempatia mamlaka yanayojitosheleza kwa sababu hata kama

taarifa yake isingeletwa na Serikali, yeye kwa mujibu wa ibara ya 143(4), angekuwa na mamlaka ya kuileta.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukisoma Katiba pamoja na ile Sheria anayoifanyia kazi *Public Audit Act,* kifungu cha 27, 28 na 29 vimempa wigo mpana kufanya *Forensic Audit, Performance Audit* na *other audits*. Sasa tunapofika hapa ndipo tunaona uwajibishwaji wa watu wale ambao wamepewa dhamana ya kutekeleza majukumu ya Serikali na mashirika yake wanavyowajibishwa kwa njia mbalimbali kwa kufuata misingi yetu ya utawala bora na vilevile kwa kuzingatia nchi yetu ina mgawanyo wa madaraka. Wapo ambao wanatuhumiwa ambao wamebainika na wakachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi ambapo kifungu cha 6(1) kinagatua mamlaka ya kinidhamu kwa *Accounting Officers*. Kwa hiyo tunapofika mahali hapa mamlaka haya yako mpaka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, yawezekana baadhi ya michango watu wanashangaa kuwaona watu mtaani, lakini yule mtu tayari shauri lake lilishachunguzwa na tayari lilishafanyiwa kazi na mamlaka zinazohusika kwa mujibu wa taarifa ya TAKUKURU, kwa mfano kwa 2020/2021, kati ya taarifa walizopokea wao kufanyia kazi kutoka kwa taarifa ya *CAG* ni 533, taarifa 110 zilifungwa kwa kukosa mashiko. Hii maana yake ilikuwa ni kutekeleza yale majukumu ambayo yapo kisheria, vyombo chunguzi vinapopokea taarifa vinachunguza.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna hatua za kidhamu katika taarifa 102 zilichukuliwa. Kwa hiyo nalisema hili ili kutuhumiwa ni jambo moja, kuthibitishwa na ukosaji au

hatia ni jambo lingine na mchakato wa kusikiliza mashauri yenye tuhuma umegatuliwa kikatiba, mahakama kwa upande mmoja kama chombo na mhimili unaosimamia haki wa ngazi ya juu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa mujibu wa Ibara yetu ya 13(6) tunajua kuna vyombo vingi pamoja na hao *Accounting Officers*, hivyo, ningependa ieleweke kwamba tuhuma ni jambo moja na mchkato wa kuthibitisha ni jambo lingine. Mijadala kama hii inavyoendelea inawezekana watu wakaonekana mitaani na ndiyo hao wanasema kwamba ni vizuri waorodheshwe ikibidi waletwe au wakutwe Gerezani kesho, lakini yule mtu kwa mujibu wa Sheria zetu ameshafikishwa mbele ya Mwajiri ambaye ndiye *disciplinary authority,* akasomewa mashtaka wakaleta utetezi na akatiwa hatiani kwa mujibu wa zile taratibu zilizopo kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na *Public Finance Act*.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu habari ya kuongezewa muda, nafikiri hili ni jambo ambalo mimi sioni kama ni baya, kwa sababu hata kwa mujibu wa Ibara ya 143 (3), *CAG* anachotakiwa ni kuandaa taarifa walau afanye mara moja na kuwasilisha taarifa sasa akiongezewa inakuwa vizuri zaidi, lakini Kamati hizi nazo zikiongezewa muda ni jambo la heri. Pia kuna jambo lingine ambalo limenivutia sana la wale Wabunge wenye kusema Halmashauri zifutwe, ninatambua Waheshimiwa Wabunge wao ni sehemu ya Mabaraza ya Madiwani na wao wapo kwenye *Planning and Finance Committees.* Kwa hiyo, ningependa ieleweke kwamba ni vizuri sana chochote kinachoazimiwa hapa, vilevile labda na waliohusika

kwenye Halmashauri zile kwa ujumla wao, ni vizuri tusiangalie *in isolation*.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ningetamini ingelikuwa ni mimi, Bunge hili lilivyo - *live* na yale Mabaraza au ngazi ya chini yangekuwa *live*. Yawezekana ndugu zangu wengine mmeongea hapa, msingeweza kuyaongea kama mlivyoyaongea. Ninapenda kuomba na kuungana na baadhi ya Wabunge wengi ambao wamesema ni vizuri sheria zetu tuendelee kuzihuisha na nipende tu kutoa taarifa kwamba Sheria ya *Public Procurement Act* tayari inafanyiwa *review* na wakati wowote kwa mujibu wa taratibu zetu za mkondo wa kutunga sheria na marekebisho, itawasilishwa kwenye Bunge lako kila kitu kitakapokuwa kimekamilika, ni pamoja na sheria zingine ikiwemo ile ya *PPP* na zinginezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mikataba, vilevile Serikali imeendelea kuchukua hatua ambazo ni mahsusi na nafikiri tumejitahidi kuwa wawazi sana, mmeona tarehe 29 Mwezi wa Tisa mwaka 2022, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo yake kuhusiana na Watendaji ndani ya Serikali kuhakikisha kwamba mikataba yote iingiwe kwa kufuata miongozo pamoja na taratibu ambazo inatuwezesha kama Taifa kuwa na mikataba bora.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba niendelee kupongeza chochote kilichoendelea katika mijadala hii ni ombi langu kwamba nia njema iwepo ili tuweze kufikia maendeleo mazuri. Mheshimiwa Shigongo ameelezea yale mafanikio ambayo nchi yetu inaangaliwa na nchi zingine na inavyopimwa, sasa tukisema kwamba hatuna mchango mzuri kama Serikali, Mawaziri hawa hawachangii chochote kidogo inashangaza! Siyo kutetea

kwamba kule ambako kuna udhaifu vilevile ni vizuri ukashughuliwa kwa nafasi ile inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa kumalizia, Bunge hili katika majukumu yale tuliyonayo ile Ibara ya 63, mojawapo ni kutunga sheria. Kwa hiyo, ninaomba sana mijadala yote tunayoitoa humu ambayo imekwenda kinyume na sheria zetu wenyewe tulizotunga, unaposema mtu anyongwe na unajua Bunge hili halijatunga sheria ya kunyonga mtu kwa makosa ambayo yapo humu. Nafikiri iwe ni uamsho kwamba tujitahidi sana kuelewa mipaka ya sheria zetu, inatoa nini. Vilevile kuangalia namna ambavyo tutatekeleza majukumu ambayo tunayo, kila muhimili ukitekeleza majukumu yake ili mwisho wa siku wananchi ambao tunawatumikia basi waweze kunufaika na utumishi wetu. Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na Naibu Waziri wa Nishati ajiandae. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyokuwa nimesema tangu mwanzo, hoja hii ni ya Bunge, kwa maana ya hizi hoja tatu za Kamati, kwa hivyo Serikali inapotoa ufafanuzi wanachangia. Kwa hiyo, na wao wanaruhusiwa kupewa taarifa na Wabunge kama ambavyo wao huwa wanawapa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nami nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim ambaye ametuwezesha kukutana katika Bunge hili na kujadili

taarifa hizi tatu za Kamati zetu na bado anatupa thamani ya ubinadamu. Thamani ya ubinadamu ni uhai tu, ukiondoka uhai, basi tumekosa thamani ya ubinadamu na ndiyo maana tunaondolewa katika makazi ya watu na kupelekwa katika makazi maalum. Jambo la pili, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyo pambana na kupigania kwa kujitoa kabisa kwa maslahi ya Taifa na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa mchango wangu katika mjadala huu, Mungu akubariki sana. Naomba niwashukuru Wenyeviti wa Kamati hizi tatu lakini na Wenyeviti wa Kamati zote, niwashukuru na niwapongeze sana Wabunge wenzangu ambao mmechangia na kwa kweli mchango unalenga kujenga Taifa letu. Michango yenu ni mizuri sana na kila mmoja ambaye amesimama hapa nilikuwa namuona anaongea, anatoa hoja kwa hisia kali sana, kwa uchungu wa nchi yake, nawashukuru na ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba moja kwa moja nijielekeze katika hoja ambazo zimeletwa na Waheshimiwa Wabunge. Nikianza na hoja ya mwenendo wa utoaji fedha kwenda *LGS* siyo mzuri, ametoa mfano Mheshimiwa Mbunge, Halmashauri ya Mwanga.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021/2022 bajeti yao ilikuwa ni bilioni 2.31 kwa ajili ya kujenga miradi ya maendeleo ya Halmashauri hiyo ya Mwanga. Serikali ilitoa shilingi bilioni 5.07 sawa na asilimia 219 kupeleka ndani ya Halmashauri hiyo. Mwaka 2022/2023 bajeti yao

ilikuwa Bilioni 5.55 hadi kufikia Oktoba tayari Serikali imeshatoa Bilioni 1.85 sawa na asilimia 33.74. Ofisi ya Msajili wa Hazina ipo katika mchakato wa kuboresha sheria ili kuonesha baadhi ya vipengele vyenye upungufu hususan utaratibu wa kutoa adhabu kwa baadhi ya viongozi wa Taasisi za Umma ambao wanakiuka taratibu na sheria.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni ya *GPSA*. Kwanza naomba nikiri kwamba *GPSA* imechelewa au imecheleweshа kutoa huduma hiyo ya magari. Kwa kweli, suala hili limechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo UVIKO–19 pia vita vya Ukraine, hii imechangia sana ucheleweshaji wa ununuzi wa magari hayo. Serikali imelipokea hili nikuhakikishie na nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba tutalichukulia hatua haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ambayo inasema Wizara ya Fedha na Mipango iboreshe mazingira ya *Internal Auditors* katika Serikali za Mitaa. Wizara ya Fedha na Mipango, tayari imepitia muundo wa Idara ya *Internal Auditors na* Mamlaka za Serikali za Mitaa…

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika taarifa!

**SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jerry William Silaa.

**T A A R I F A**

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza mchangiaji kwa makini na nimechelea kidogo. Nimemsikia akisema ziko hoja zimetolewa na

Wabunge na anataka kutoa majibu, lakini hoja iliyoko mezani ni hoja ya Kamati za Bunge na Wabunge wote waliochangia wamechangia hoja ile na yeye kama mchangiaji ni vyema akachangia hoja ili tuweze kuihitimisha hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nafikiri kwa sababu hapo mwanzo alikuwa anaelezea utangulizi sasa anaenda kwenye hoja. Kwa hiyo, akishaanza hizo hoja ndiyo tutajua anazungumzia hoja za Kamati, kwa sababu pia Wabunge mmechangia humu ndani. Kwa hiyo, yeye yale yanayohusu Wizara yake ni muhimu ayatolee ufafanuzi. Kwa hiyo, mpaka tuanze kumsikia ndiyo tutajua kama ametoka nje ya hizi Kamati tatu na taarifa zake na je hilo jambo ambalo analolisema lilichangiwa humu ndani au hapana. Mheshimiwa Naibu Waziri karibu uendelee na mchango wako. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa ruhusa hii. Naomba nitoe ufafanuzi kwenye hoja iliyotolewa na Bunge kuhusu mtaji wa Benki ya Kilimo ya Tanzania. Kwanza naomba nikiri kwamba ni kweli Serikali iliahidi kutoa mtaji wa kupeleka katika Benki ya Kilimo ya Tanzania lakini mpaka sasa imetoa Bilioni 60 kutokana na uchache au uhafifu wa bajeti tuliyokuwa nayo. Serikali ipo katika juhudi mbalimbali kuhakikisha kwamba imeongeza mtaji katika benki hiyo kwa maendeleo ya benki hiyo lakini wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, juhudi ambazo Serikali imechukua, kwanza Serikali imechukua mkopo nafuu wa Dola za Kimarekani Milioni 92.55 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na kuikopesha *TADB*. Pili, Serikali imeamua kuifutia Benki ya Kilimo mkopo wa Dola za

Marekeni 92.55, takribani Bilioni 216 na kugeuza kuwa mtaji wake ndani ya benki hiyo. Tatu, Serikali imechukua mkopo nafuu wa *Euro* Milioni 80 takribani Shilingi 185 kutoka Benki ya Maendeleo ya Ufaransa na kuikopesha benki hiyo. Hatua nyingine ambayo imechukuliwa na Serikali, ni Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iliipatia Benki ya Maendeleo pesa takribani Dola za Kimarekani Milioni 25 kwa ajili ya dhamana kwa wakulima wadogo kutoka *IFAD*. Aidha, Serikali inaendelea kuangalia vyanzo vingine vya fedha ili kuipatia benki hiyo kwa maendeleo ya benki hiyo lakini na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilizungumzwa na baadhi ya Wabunge ni kuhusu makinikia. Kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021 ukurasa wa 63, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibainisha kuwa baadhi ya mashauri ya kodi hususan yanayohusiana na sakata la makinikia yaliondolewa katika Mahakama za Rufaa za Kodi ili kushughulikiwa kwa utaratibu wa majadiliano kati ya Serikali na Kampuni za Madini. Katika majadiliano hayo Serikali ilijenga hoja na kufanikiwa kupata mafanikio haya yafuatayo: -

(i) Kulipwa Dola za Marekani Milioni 300, takribani Shilingi za Kitanzania Bilioni 700.

(ii) Kampuni ya Barrick kukubali kufuta kesi ya madai ya fidia kwa Serikali Dola za Marekani Bilioni 2.7.

(iii) Pia, kupewa umiliki wa asilimia 16 kwenye migodi ya kampuni hiyo ambapo imeunda kampuni mpya inayojulikana kwa jila la Twiga *Mineral Cooperation*. Barrick wao wana asilimia 84 na Serikali ina asilimia 16 katika hisa iyo.

(iv) Serikali imepokea jumla ya gawio la Dola za Marekani Milioni 36 na kupokea gawio kutokana na marekebisho ya mkopo kwa wanahisa. Dola za Marekani Milioni 16 kwa kipindi cha 2020/2021 na Barrick imekubali kutenga kiasi cha Dola za Marekani Sita kwa kila wakia kwa dhahabu zote ambayo itauzwa kwa ajili ya shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, sakata la madai ya kodi ya Shilingi Trilioni 360 lilihitimishwa kwa Serikali kuridhia makubaliano haya kama ilivoainishwa katika maelezo ambayo ameyatowa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango katika Bunge lililopita.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni malimbikizo ya madeni hasa *TANROADS*. Serikali imechukua juhudi kubwa sana, kwa sababu madeni haya Serikali ya Awamu ya Sita imeyarithi, lakini imechukuwa juhudi kubwa sana katika kulipa madeni hayo yaliyokuwepo na tunaendelea. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kulipa na miradi yote ambayo imeandaliwa na Serikali ya kimkakati basi itatekelezwa na tutalipa *certificates* hizo zikishaletwa kwa wakati kabisa.

Mheshimiwa Spika, ilikuwepo hoja ambayo imezungumzwa kuhusu utaratibu wa kufuta madeni chechefu katika benki zetu za *TIB* na *TCB*. Serikali imeshaanza kuchukua hatua za kuondoa madeni chechefu katika benki za *TIB* na *TCB* ambapo taratibu zinaendelea kuhakikisha madeni hayo yanaondolewa kwenye vitabu vya benki.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ambayo imezungumzwa kuhusu kukosekana kwa bodi kunasababisha mashirika kukosa umakini wa kufanya kazi. Serikali imeendelea kuweka juhudi katika kuhakikisha Taasisi na Mashirika ya Umma yanakuwa na Bodi za Wakurugenzi hai. Kwa sasa Serikali imeshafanya uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi zipatazo 23 kati ya Bodi 31 ambazo zimesalia Bodi Nane na hizo Serikali inachukuliwa hatua katika kipindi kifupi kabisa Serikali itakuwa imefanya uteuzi wa Bodi hizo.

Mheshimiwa Spika.…

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hebu rejea hapo kwenye takwimu za Bodi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka juhudi katika kuhakikisha Taasisi na Mashirika ya Umma yanakuwa na na Bodi za Wakurugenzi hai, kwa sasa Serikali imeshafanya uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi zipatazo 23 kati ya Bodi 31 ambazo zilikuwa hazina Bodi. Serikali inakamilisha utaratibu wa kuteua Bodi za Taasisi Nane zilizosalia…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba

Bodi anazosema Serikali iko katika mpango wa kuteua Wajumbe wake kwa taarifa ya *CAG*, Bodi zingine zipo toka mwaka 2015, Serikali bado tu inaendeleaa na utaratibu wa Wakurugenzi wameshakuwa wamiliki wa hizo kampuni. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamadi Chande unapokea taarifa hiyo. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nina ukakasi kidogo wa kupokea hiyo taarifa, lakini mimi niseme tu kwamba takwimu ambazo tunazo ni hizi 31 na 23 tumeshafanya uteuzi wa bodi, zilizosalia ni nane. Nadhani tuna asilimia zaidi ya 70, kwa hiyo awe na subira tu Mheshimiwa Mbunge ataona matokeo hivi karibuni, bodi zilizobakia tunateua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu kwenye taarifa ya Kamati walitaja Bodi zaidi na ni sehemu ya maazimio ya Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ambayo inazungumzia hizi Bodi ili tutakapofika kwenye maazimio tusianze tena kurejea nyuma. Mwenyekiti wa Kamati zile takwimu ulizonazo na hizi Bodi anazozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ni tofauti ni hizi au hili ni jambo jipya.

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kuna tofauti kubwa sana. Taarifa tulizonazo kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina mpaka kufikia tarehe 31 Oktoba, jumla ya mashirika 23 hayana Bodi za Wakurugenzi. Kuna mashirika 12 ambayo tayari Mheshimiwa Rais ameshateua Wenyeviti wa Bodi lakini bado Wajumbe hawajateuliwa. Kwa hiyo, jumla ni

mashirika 35 mpaka kufikia tarehe 31 Oktoba wakati tunaandaa taarifa hii mashirika hayo hayana Bodi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hizi takwimu anazosema Mwenyekiti zipo sawasawa? Nataka tu kwenye takwimu ili wakati wa Azimio tusije tukaazimia na yale ambayo Serikali imeshayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma anasema Bodi 23 kufikia mwishoni mwa Oktoba zilikuwa hazina Wajumbe wala hazina Wenyeviti, Bodi 12 zina Wenyeviti ambao Rais ameshawateua lakini Wajumbe wale wanaoteuliwa na vyombo vingine ama na Mawaziri bado. Hizi takwimu zipo sawasawa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa swali hilo. Suala hili la Bodi ambazo tuko na uhakika nazo ni Bodi 23 ambazo Wajumbe wake wameshateuliwa na zimeshakamilka. Hizi nyingine labda zipo kwa upande wa Taasisi nyingine ama Wizara nyingine lakini mimi nazungumzia ambazo ziko ndani ya Wizara ya Fedha.

**SPIKA:** Hivi *Treasury Register* anaripoti wapi? Mheshimiwa Mwenyekiti *Treasury Register* anaripoti wapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwenyekiti, *Treasurer Registrar* anaripoti wapi?

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, Msajili wa Hazina anaripoti Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

**SPIKA:** sawa. Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi nimekuelewa hoja yako. Ni kwamba hizi taasisi zinaweza kuwepo lakini kwa sasa hivi hapo hauna takwimu nazo, kwa hiyo sisi tutaendelea na azimio letu kuhusu hizi taasisi. Mheshimiwa Waziri wa Nchi anataka kutoa ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sana ya kikao chako hiki cha Bunge, kwa *spirit* ambayo ameingia nayo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, na hasa baada ya kukuta tatizo hili la teuzi za bodi kwamba ni tatizo ambalo limekuwa likijitokeza sana Serikalini; Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo na *Chief Secretary* na taasisi zinazohusika walishapewa kazi ya kusimamia.

Mheshimiwa Spika, itakuwa ni kumtendea haki Mheshimiwa Rais na kazi nzuri ambayo imekwishakufanywa kwani katika kipindi hiki…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam ngoja nijaribu kuelewa hoja kwanza kabla hujatoa taarifa yako, maana hajaanza bado kutoa hoja. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nadhani itakuwa ni vizuri kama katika kipindi hiki ambacho tunaelekea kuhitimisha hoja hii tukapata fursa ya kupata taarifa ambazo ziko kamili. Ninaheshimu taarifa za Mwenyekiti ambazo zimeishia

mwezi Oktoba, lakini tangu mwezi Oktoba, mpaka sasa tunaweza kuwa na taarifa ambazo ni *current*.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sana, kama utaridhia, tuweze kupata taarifa hizo ambazo tunaweza kuzipata sasa hivi kutoka kwa *Treasurer Registrar* ili azimio letu tukishalipitisha hapa liwe ni azimio ambalo limebeba dhana kamili ya idadi kamili ambayo inatakiwa kuwasilishwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Sasa, kulikuwa na taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam, sijajua taarifa nyingine inatoka wapi. Sasa ngoja, kwa sababu mtapata fursa ya kuchangia, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI nawe ni kuhusu Bodi pengine zilizokuwa chini yako ambazo umezifanyia kazi kati ya huo muda. Sawa, Mheshimiwa Tabasam.

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, leo tupo *serious* na tumeamka vibaya, na ninaomba kabisa Waheshimiwa Mawaziri waje na nidhamu kabisa kwa siku ya leo, kwa sababu suala la *vetting* liko chini ya Ofisi ya Rais ambapo Waziri anayekuja kuzungumza maneno haya *vetting* iko kwake, na yeye ndiye sehemu ya ucheleweshaji wa vitu hivi. Tusubiri tufike mwisho leo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwenyekiti nimekuona. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, naona ulisimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nami nilitaka kutoa tu taarifa; kwamba katika bodi tatu, sijajua taarifa ya Mwenyekiti wa Hesabu za Mashirika ya Umma au Uwekezaji katika Mashirika ya Umma kama na za kwetu zimo. Endapo zimo, kwa Bodi ya *DART* tayari imeshaundwa, kwa Bodi ya Masoko ya Kariakoo tayari imeshaundwa, na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa pia nayo tayari tumeshaiunda, kwa hiyo kwa upande wangu wa TAMISEMI bodi zote tatu zipo.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, naona ulikuwa umesimama.

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo madogo kutokana na taarifa zilizotolewa hapa, na kwa kuwa jina la Mheshimiwa Rais limetajwa, naomba ninukuu Hotuba ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa tarehe 30, Machi 2022, nanukuu; "CAG umeeleza kuwa, mwenendo wa Mashirika ya Umma ambayo umebainisha Mashirika 38 ya Umma yanaendeshwa bila kuwa na Bodi. Hii inashangaza kwa miaka kadhaa mashirika yanaendeshwa hakuna Bodi za Wakurugenzi. Mimi nakumbuka nilipoingia nilipata mtiririko wa maombi ya bodi na yote nimeshayatoa. Sasa kama Waziri ana mashirika, bado anaendesha mashirika yasiyo na bodi, siwezi kumuelewa na sijui tatizo ni nini." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema niyaseme haya kwa sababu kuna mashirika ama kuna Wizara wakati

mwingine zinatupa mzigo wa uteuzi kwa Mheshimiwa Rais, lakini Mheshimiwa Rais alishasema hadharani kwamba yeye anateua bodi kwa wakati, la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, Ofisi ya Msajili wa Hazina inao mfumo ambao unatoa taarifa kwa Wizara miezi tisa kabla bodi haijamaliza muda wake ili mchakato na urasimu wote wa *vetting* ukamilike kwa wakati. Kwa hiyo tunaporipoti hapa, tunaripoti mambo ambayo tunauhakika nayo na yamethibitshwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina na yako sahihi, na kwa nyongeza, tarehe 30, Oktoba ni siku nne kuanzia sasa ndiyo taarifa yetu imetoka.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, malizia mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia tena fursa hii. Nimalizie mchango wangu kwa hoja iliyokuwa inazungumzia Sheria ya Manunuzi kwamba inaupungufu.

Mheshimiwa Spika, hili nikiri kwamba sheria hii ina upungufu; na kama alivyoeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali hatua ambayo imefikiwa kwa sasa ya kufanya marekebisho ya sheria hiyo iko katika ngazi ya maamuzi na karibuni hivi itaingia Bungeni kwa ajili ya kupata mapendekezo na maoni kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. kwa hiyo niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la Sheria ya Manunuzi na sura 410 lipo katika hatua ya maamuzi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, wapo wachangiaji wengi ambao walichangia kuhusu manunuzi. Kwamba kuna upotevu

mkubwa sana wa fedha katika manunuzi. Naweza kusema kwamba zaidi ya asilimia 70 ya fedha za bajeti za Serikali zipo katika manunuzi. Kwa hiyo hii ni sehemu moja nyeti na muhimu sana na Serikali imeichukulia hatua sehemu hii kwa kiasi kikubwa sana. Kutokana na mapungufu yaliyokuwepo pale, Serikali imeamua kuanzisha mfumo mpya wa manunuzi ambao unaitwa *NEST* ili kuepuka changamoto ambazo zinajitokeza wakati wa kufanya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, na hii yote ni kwa sababu ya mfumo tulio nao si rafiki kwa matumizi ya watumiaji na pia utoaji wa taarifa sahihi. Kwa hiyo tumeamua Serikali kuanzisha mfumo huu, na faida ambazo zinaweza kupatikana kutokana na mfumo wa sasa wa *NEST* ni nyingi sana. Kwa mfano, itaongeza uwazi *(transparency)* kwa sababu mfumo uliokuwepo usiri ulikuwa ni mkubwa sana ambao unaweza kupelekea mianya ya rushwa. Mfumo huu utakuwa uko wazi na watumiaji wote watakuwa wana-*access*.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, utaongeza uwajibikaji; kutakuwa na uwajibikaji mkubwa sana katika mfumo huu. Faida nyingine ambayo inaweza kupatikana katika mfumo huu ni kuweka ukomo wa bei za bidhaa, yaani kuweka bei kikomo au bei elekezi, kwamba bidhaa hii bei yake ni hii hapa ili kusudi kuepuka manunuzi holela. Maana inawezekana bidhaa moja hii mfano ya kalamu kwa idara tofauti zikawa na bei tofauti kutokana na mfumo ambao ulikuwepo, lakini kwa sasa mfumo huu unaenda kujenga na kutuweka wazi. Na huu ndiyo mwarobaini pekee wa ku-*save* fedha za Watanzania.

**SPIKA:** Dakika moja malizia mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika….

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Deus Sangu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**T A A R I F A**

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana; naomba kumpa taarifa mzungumzaji. Mfumo huu wa *TANEPS* ambao upo sasa ni mfumo ambao umewekwa hivi karibuni, mwaka 2020 ndio ulikuwa *mandatory* kwa taasisi zote za umma na umegharimu mabilioni ya fedha za Watanzania. Leo hii ndani ya miaka miwili Serikali yenyewe iliyoweka huo mfumo inatuambia kwamba ni *redundant* na hauna maana, na wanatuambia wanakuja na mfumo wa *NEST* ambao uta-*address* matatizo haya. Hivi kweli huu sio ufisadi mwingine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sangu kwa kawaida taarifa huwa haina maswali lakini, Mheshimiwa Naibu Waziri wa fedha na mipango unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, hii taarifa siipokei kwa sababu unaweza kuishi na mke hata kwa siku tatu tu; bila kujali gharama ya mahari uliyotoa; ukaona kwa mwenendo huu sasa huyu hanifai tena. Kwa hiyo unaweza kuacha. Hata kama umetumia siku tatu, achilia miaka miwili. Kwa hiyo taarifa hii mimi siipokei.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu tunaotarajia kuutumia endapo utatumika, kwa utafiti mdogo ambao tumeufanya, utakoa zaidi ya shilingi trilioni mbili. Pia mfumo huu utawezesha Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali angalau kuwa na matokeo mazuri badala ya kuwa na matokeo hasi siku zote, kwa sababu tunakwenda kujadili na kuona wapi kuna mwanya au kuna viashiria vya upotevu wa fedha kabla mradi haujaanza, tofauti na mfumo ambao ulikuwepo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kutoa wito kwa taasisi zote za Serikali kujiunga na mfumo huu ambao utasaidia matumizi halali. Ahsate sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ajiandae.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nami napenda kuchukua fursa hii, kama walivyoanza wenzangu, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Kipekee kabisa napenda nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja za kamati tatu zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati pamoja na Wenyeviti wa Kamati zote tatu na Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia kwenye hoja hizi. Naomba niwahakikishie Wajumbe wa Kamati kwamba michango yao ni mizuri na tunaendelea kuithamini.

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa siku tatu kulikuwa na mchango uliendelea kwa muda mrefu kuhusu *KADCO*. Ninaomba nami nianze kuzungumzia *KADCO*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1998 Serikali iliagiza ukodishaji na uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha *KIA (Kilimanjaro International Airport)* utekelezwe na kampuni ya binafsi. Hii ilikuwa ni moja kati ya uendelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma yaliyofanywa kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchakato wa ubinafsishaji kukamilika, Kiwanja cha Ndege cha *KIA* ilianzishwa kampuni binafsi ambayo ni *KADCO* tarehe 11, Machi 1998 chini ya Sheria ya Makampuni sura 212, wakati huo kampuni hiyo ikiwa na wanahisa wawili. Mwanahisa wa kwanza alikuwa ni *Motor Mc Donald International* ya Uingereza na mwanahisa alikuwa ni *Inter-consult Tanzania limited*. Baadaye waliongezwa wanahisa wawili ambapo mwanahisa mwingine alikuwa ni Serikali na mwanahisa mwingine wa nne alikuwa ni *South African Infrastructure Fund.*

Mheshimiwa Spika, wanahisa hao walikuwa na mgawanyo wa hisa kama ifuatavyo: -

(a) *Motor Mc Donald International* ya Uingereza ilikuwa na hisa 41.40%,
(b) *South African Infrastructure Fund* ilikuwa na hisa 30%,
(c) *Inter Consult Tanzania Limited* ya Tanzania ilikuwa na hisa 4.6%, na
(d) Serikali ilikuwa na hisa 24%.

Mheshimiwa Spika, katika ubinafsishaji huu kulikuwa na changamoto kubwa zilizojitokeza. Changamoto ya kwanza iliyojitokeza ni kuwa wanahisa walishindwa kuwekeza kwenye Kiwanja cha Ndege cha *KIA,* changamoto ya pili ilyojitokeza ni Serikali kutonufaika na mkataba wa uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha *KIA,* na Changamoto ya tatu iliyojitokeza ni kukosa kipengele cha kuitaka *KADCO* kulipa ada ya uendeshaji *(concession fee),* na changamoto ya nne iliyojitokeza, kulikuwa na *exclusive right* ya kuzuia uwekezaji au ujenzi wa kiwanja cha ndege ndani ya usawa wa mzunguko *(radius)* ya kilomita 240. Yaani ndani ya *radius* ya kilomita 240 hakukutakiwa mwekezaji yeyote aweze kujenga kiwanja cha kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizi Serikali iliona mkataba huo unamaslahi machache. Kwa hivyo Serikali ikaamua kwamba sasa iko haja ya kuvunja mkataba huo. hata hivyo kabla ya hapo kulikuwa na mikataba mitatu ambayo ilisainiwa. Mkataba wa kwanza ilikuwa ni *sharehold agreement,* mkataba wa pili ulikuwa ni uendeshaji *(concession fee)* na mkataba wa tatu ni wa ukodishaji *(lease agreement)* ambao uliwekwa kati ya Serikali na *KADCO.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizojitokeza Serikali ilifanya maamuzi ya kuamua kuwanunua wanahisa. Ambapo Kampuni ya *Motor Mc Donald International* ya Uingereza ililipwa dola za Marekani 2,752,540.6, hizi ni Dola za Kimarekani, *South African Infrastructure Fund* ililipwa dola za Marekani 1,994,593.52 na *Inter Consult Tanzania Limited* ya Tanzania ililipwa dola za Marekani 339,373.01.

Mheshimiwa Spika, baada ya kulipwa fedha hizo na Serikali, Kampuni ya *KADCO* ikawa asilimia 100 ni Kampuni ya Serikali na *share* zake zote zipo chini ya Msajili wa Hazina kama ilivyo kampuni nyingine za Serikali. Haya yote yanathibitishwa kupitia hati ya usajili namba 33,616 ya *BRELA* kuhusu usajili wa *KADCO*.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kununua *share* hizo, *shareholding agreement automatically* ilikufa yenyewe kwa sababu wana-*share* hawapo. Mikataba miwili iliyobaki, *concession agreement* pamoja na *lease agreement* zilikuwepo lakini hazikufanyiwa mabadiliko yoyote. Tulitegemea pengine zingefanyiwa mabadiliko na kukawa na *agreement back* kati ya *TAA* na *KADCO* lakini haikufanywa hivyo. Nitaeleza huko mbele hatua ambazo Serikali itazichukua kwa ajili ya kufanya mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu wafanyakazi wa *KADCO*. Kama nilivyosema, *KADCO* ni kampuni ya Serikali kwa asilimia 100 na bodi ya *KADCO* pamoja na wanabodi wa *KADCO* na Mwenyekiti wa bodi wanachaguliwa na Serikali na hivi ninavyosema kwamba bodi hii iko na inaenda vizuri.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuna taarifa kuktoka kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Waziri, alikuwa ametupeleka vizuri, ametuonesha njia na dola zilivyolipwa na mikataba ile mitatu, sasa angetumaliza kwenye hiyo hoja halafu akaenda ya wafanyakazi ili tukawa na mtiririko mzuri wa mambo hayo. Kwa sababu akiturudisha huku tena tutakuwa tumesahau, atupeleke huko huko alikokuwa anatupeleka tumalizie. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere yeye ndiyo alilvyopanga mtiririko wa mchango wake sasa tusimchanganye ila tusikilize kama unalo kwenye hili analosema unaruhusiwa kutoa taarifa, lakini yeye amepanga mtiririko ambao yeye anauelewa maana yeye ndiyo anatoa maelezo. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nitakwenda hivyo anavyotaka kwa sababu kila kitu kiko hapa, hakuna tofauti yoyote. Kama nilivyosema *KADCO* ilianzishwa kama kampuni kwa sura ya 212. Lakini *TAA (Tanzania Airport Authority)* ilianzishwa kupitia tangazo la Serikali Namba 404 la mwaka 1999 chini ya kifungu namba tatu cha Sheria ya Uwakala wa Serikali. Kwa vile *Tanzania Airport Authority* si mamlaka, inaitwa tu jina hilo kwa sababu sheria iliyoanzisha ilikuwa ni Sheria ya Uwakala wa Serikali Sura Namba 244 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo la *KADCO* na kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha viwanja vya ndege, Serikali tumeanza mchakato wa kutengeneza Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kama mamlaka, na kwenye sheria hiyo tutahakikisha kwamba

*KADCO* inaelekezwa vizuri. Kwenye sheria hiyo, tutahakikisha kwamba *KADCO* inaelekezwa vizuri, aidha imilikiwe moja kwa moja; sasa hivi inamilikiwa na *TAA,* lakini imilikiwe ndani ya sheria au *alternative* ifanyike kwamba, ianzishwe kampuni tanzu ambayo yenyewe ndiyo itaendesha Kiwanja cha Ndege cha *KIA*. Suala la *KADCO* linaweza kuwepo ama linaweza kufa moja kwa moja, itategemea sheria itakavyoelekeza. Hayo tutayafanya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, kwenye sheria hiyo tunaangalia utaratibu ambao utavifanya viwanja vyetu vya ndege viwe salama na ulinzi ukamilike kwa sababu kuna changamoto kubwa sana kwenye viwanja vya ndege. Sheria iliyopo sasa hivi haikidhi uendeshaji wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba sheria hii itakapokuja kupitishwa hapa Bungeni tatizo la *KADCO* litamalizwa maisha, litakuwa limeisha. Inaweza kuendeshwa moja kwa moja kupitia *TAA* yenyewe au inaweza kuanzishwa kampuni nyingine ambayo itasimamia Kiwanja cha Ndege cha *KIA*.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**T A A R I F A**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa kwamba wananchi wa Hai sasa

hivi wako kwenye *TV* wanasubiri maagizo ya Serikali kwenye jambo hili. Ameeleza historia vizuri, akaja akatuambia *KADCO* ni ya Serikali, katikati hapa anasema inaweza ikawepo au isiwepo. Kwa hiyo, nataka tu kumwambia, leo tunategemea kupata majibu ya Serikali thabiti kwamba *KADCO* ni ya Serikali au siyo ya Serikali; na hatma yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa taarifa yangu kwa sababu kule kuna jambo linaendelea na hizi taarifa kule zinachanganya wananchi. Sasa hapa tunaambiwa ni ya Serikali asilimia 100, lakini inaweza ikaondolewa au isiondolewe. Serikali inasemaje kuhusu jambo hili ili sisi wananchi wa Hai tunaosikiliza Serikali hapa tujue hatma ya jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kikanuni unapotoa taarifa ni kwamba unamwongezea yule mchangiaji jambo fulani, siyo unamwuliza maswali. Sijui tunaelewana! Eeh, yaani siyo umwulize maswali, sasa inakuwa kimegeuka kuwa kipindi cha maswali na majibu. Hapa anayeruhusiwa kuuliza maswali ni mimi hapa. Mimi ndio naruhusiwa kuuliza maswali, lakini ninyi toeni tu taarifa kwa mujibu wa kanuni zetu.

Mheshimiwa Waziri, malizia mchango wako.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tutaleta sheria hapa kama nilivyosema ambayo itaeleza mfumo mzima wa uendeshaji wa viwanja vya ndege, ikiwemo Kiwanja cha Ndege cha *KIA*. Wakati utafika Waheshimiwa Wabunge nyote mtapata hiyo fursa,

mtalichambua jambo hili kwa kina na ushauri wenu sisi tutaupokea.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwamba Serikali kupitia Kikao cha Baraza la Mawaziri namba 15 cha mwaka 2009 kilichofanyika Mei 14 mwaka huo, kilielekeza kwamba Wizara ya Uchukuzi iache majadiliano na Kampuni ya *Omniport* ambayo ilikuwa inataka ikabidhiwe Uwanja wa Ndege wa KIA badala ya *KADCO* kwa kuwa *KADCO* alishindwa kuwekeza. Taarifa zilizoletwa zilionesha kwamba hata huyo *Omniport* ambaye alikuwa apewe huo uwanja, naye hakuwa na uwezo wa kuwekeza, ilikuwa ni usanii. Hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili, Serikali…

**SPIKA:** Mheshimiwa taarifa ni moja.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, inaendana na hiyo tu. Ni kwamba katika maamuzi hayo ya Serikali, ikaelekezwa kwamba *KADCO,* huyo Omniport wote watolewe, Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro urudishwe chini ya mikono ya *TAA*. Sasa ni kwa nini haukurudishwa na mpaka leo hii tunajadili *KADCO*

wakati maelekezo ya Serikali yalikuwa upelekwe chini ya mikono ya *TAA? (Makofi)*

**SPIKA:** Sawa ahsante. Mheshimiwa Waziri unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, inanipa taabu kwa sababu kujibu kwa nini haikurejeshwa, hilo swali siwezi kulitolea ufafanuzi hapa.

**SPIKA:** Nami nimekusaidia. Yaani mtu akitoa taarifa, ni ile taarifa ambayo haina swali, kwa sababu wewe siyo kazi yako kujibizana na Mbunge. Au umeshamaliza mchango wako? Wewe malizia mchango wako, kama taarifa yake unaona imeuliza swali, wewe endelea na mchango. Maswali ni mimi hapa ndio naruhusiwa kuuliza.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi wa *KADCO,* kama nilivyosema, *KADCO* ni kampuni ya Serikali na Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Mwenyekiti wanachaguliwa na Serikali. Hivi ninavyozungumza, tuna bodi pamoja na wajumbe wote na wanafanya kazi. Wafanyakazi wote wa *KADCO* ni Watanzania. Pia *KADCO* inayo mwanasheria ambaye anaitwa Winfrey Komba ambaye yeye alihamishwa *KADCO* mwezi Januari, 2021.

Mheshimiwa Spika, pia *KADCO* inaendelea kulipa kodi mbalimbali, kwa mfano tu imelipa gawio mwaka 2016/2017 Shilingi milioni 555; mwaka 2017/2018 ililipa Shilingi milioni 583; mwaka 2018/2019 ililipa Shilingi bilioni moja; miaka miwili iliyofuatia 2019/2020 na 2021 haikulipa kutokana na ugonjwa wa *Covid* na sekta ya anga iliathiriwa kwa asilimia kubwa. Pia *KADCO* inayo akaunti

Benki Kuu ya Tanzania na malipo yote yanayofanywa na makampuni ya ndege yanawasilishwa kule. Hiyo ni hoja kuhusu *KADCO.*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niongelee hoja kuhusu maingiliano kati ya *TANROADS* na *TAA* kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege. Ni kweli yalifanyika maamuzi mwaka 2018 kuhamisha ujenzi wa viwanja vya ndege kwenda *TANROADS.* Kulikuwa na changamoto ambazo zilisababisha kufanya hivyo na ilifanya hivyo kupitia *GN* namba 293 ya mwaka 2000 ya *TANROADS* ambayo ilifanyiwa mabadiliko ili kazi hiyo iweze kufanyika ndani ya *TANROADS.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia mchango wako.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea, sasa hivi tumeshafanya mchakato na ujenzi wa viwanja vya ndege sasa vitaanza kurejeshwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA).* Ila kwa ile miradi ambayo inaendelea, kwa mfano Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, Sumbawanga, Kigoma na Tabora, mchakato utaendelea chini ya *TANROADS* kwa sababu tukiurejesha tena utachukua muda mrefu na viwanja vya ndege hivyo havitajengwa.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Msalato ambacho kinajengwa chini ya ufadhili wa *ADB* nacho kitaendelea kutekelezwa na *TANROADS* kwa sababu mchakato wenyewe kuurejesha tena utatuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo nilitaka kuligusia ni kuhusu suala la Bandari ya Tanga. Mheshimiwa Kapinga alilizungumza kwa hisia kali suala hili, lakini naomba kumwambia tu na Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla kwamba Bandari ya Tanga ni muhimu sana kwetu sisi na tunaendelea na ujenzi na mkandarasi yuko *site*. Kuhusu kwamba kuna Mkandarasi alipewa *subcontract* kwa bei ndogo, hili linafanyiwa kazi na *CAG* na naliomba Bunge lako Tukufu, utupe muda *CAG* afanye uchunguzi maalum, halafu tutapata ripoti na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naamini Mwenyekiti ameshasikia. Sasa katika ufafanuzi wako Mheshimiwa Waziri; kwanza Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka ile siku nadhani ni juzi, nilisema ningempa nafasi Mheshimiwa Waziri leo na amepewa. Nilisema katika majibu yake, mojawapo ya mambo anatakiwa atuambie ni akaunti za *KADCO* ziko wapi? Leo amejibu hapa, nadhani mmemsikia, amesema akaunti za *KADCO* ziko Benki Kuu. Nimesikia vizuri Mheshimiwa Waziri au sijasikia vizuri?

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo akaunti ya *KADCO* iko *BOT*.

**SPIKA:** Sawa. Sasa Mheshimiwa Waziri ili tuongozane vizuri kwenye haya maazimio ya Kamati na Wenyeviti wanasikiliza hapa kwa sababu kuna maeneo watafanya marekebisho kwa kuwasikiliza na kama watakuwa wameelewa. Wakati hii *KADCO* ilikuwa ni kampuni binafsi; na natumia neno "ilikuwa kampuni binafsi", Serikali

ikanunua *shares* zote, ikalipa pesa wale watu binafsi; ikahamia kuwa kwenye umiliki wa Serikali kwa asilimia 100. Mkataba ambao umesema kwamba ulikufa, ni mkataba mmoja tu kati ya mitatu uliyoitaja, kwamba ni ule mkataba wa hisa ndiyo uliokufa. Mkataba wa upangishaji *(lease agreement)* bado upo, kwa maelezo uliyotoa. Mkataba wa *concession* ambao ulikuwa unaipa kampuni binafsi mamlaka ya kuendesha pale na kufanya hivi, bado upo. Huu mkataba wa upangaji, nani ni mpangaji sasa na nani mpangishaji? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema kuna mikataba miwili ambayo ipo *concession agreement* na *lease agreement* na mikataba hii ilikuwa kati ya Serikali na *KADCO*. Kwa hiyo,…

**SPIKA:** Ilikuwa kati ya Serikali na *KADCO* wakati *KADCO* ni binafsi.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni wakati huo. Wakati huo *KADCO* ilikuwa ni Kampuni ya binafsi, lakini baadaye *KADCO* ilibadilika kuwa kampuni ya Serikali kwa asilimia 100.

**SPIKA:** Hapo tuko wote, pamoja kabisa. Hoja ni kwamba, huu mkataba wa upangishaji, kabla hata sijaenda kwenye *concession,* mkataba wa upangishaji ni kati ya nani na nani kwa sasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mikataba hii ilikuwa ifanyiwe mabadiliko, lakini ilivyo sasa hivi…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siyo hoja yake binafsi ni hoja ya Serikali, wala siyo yeye aliyekuwa ofisini. Kwa hiyo, msiwe mnamtaza kama vile…

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, mkataba ulivyo sasa hivi hata ukichukua mkataba ule unaona ni kati ya *KADCO* na Serikali…

**SPIKA:** *KADCO* binafsi?

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, *KADCO* binafsi, lakini ilibadilika kuwa ya Serikali.

**SPIKA:** Sawa, ahsante. Ngoja, hapo tumeshaelewa. Mkataba wa upangishaji ni kati ya *KADCO* binafsi ambaye alishakufa, lakini kwenye mkataba huu anaishi. Sawa. *(Makofi)*

Halafu *concession agreement* pia ilikuwa kati ya *KADCO* binafsi na Serikali. Niko sahihi?

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, lakini *KADCO* mpaka sasa hivi ipo, isipokuwa zile *shares* zilibadilika kutoka watu binafsi kuja kwenye Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilitaka kuyaelewa haya ili tunapoelekea kwenye maazimio tujue tunaazimia nini? Maana ni jambo la muda mrefu. Haiwezekani kila siku inazungumziwa *KADCO, KADCO, KADCO!* Lazima tufike mahali. *(Makofi)*

Jambo la mwisho Mheshimiwa Waziri, huu mkopo ambao *TAA* iliagizwa kukopa na Serikali, kwamba kwa kuwa wewe ndio unashughulika na viwanja vya ndege, kopa kalipe. Huu mkopo analipa nani? *TAA* au *KADCO* ya Serikali?

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema kwamba mkopo huu Serikali iliagiza *TAA* ikope na imelipa *TAA* kutoka Benki…

**SPIKA:** Imelipa *TAA* na siyo *KADCO*?

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, siyo *KADCO*.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumeelewa hali ya *KADCO* na tumeelewa hali ya Serikali. Kwa hiyo, tutakapofika hapa kwenye maazimio, ndiyo tutakuwa tumeazimia. Sasa Serikali mlitaka kupita wapi, kufanya nini, sijui mna-*negotiate* mpaka lini? Leo Bunge litakapofanya maamuzi, ndiyo tumeshafanya maamuzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia nafasi ya kujadiliana na kutoa maoni yetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge inaonesha nia njema ya kuisukuma nchi kuweza kusogea mbele kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nilipata maneno, nimeambiwa ni ya kiarabu, yanayosema: "*Yashukurunasu lashukurullah.*" Nirudie tena kwa ambao hawakusikia, *Yashukurunasu lashukurullah,* yaani maana yake, asiyemshukuru binadamu mwenzake kwa wema aliomtendea, hawezi hata kumshukuru Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwatendea mema sana Watanzania na kuhakikisha kwamba wanafikia katika ile nchi ya ahadi. Pili, nakushukuru na kukupongeza wewe kwa jinsi ambavyo unaliendesha Bunge letu, nasi wanafunzi wako na Wanasheria wenzako tunajivunia na kuona tulipita kwenye mikono salama kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa michango yao ambayo nimesema inaonesha kabisa kuwa *objective* na *progressive* kwa nia ya kuijenga nchi. Niongeze shukurani na pongezi nyingine kwa wale ambao pengine hawakusemwa hapa; hoja zilizopo hapa zinaihusu Serikali na Serikali inayo watendaji. Siyo watendaji wote wameoza, wameharibika, hawana weledi, ni wezi. Wapo ambao ni wazuri na wanafanya yale mazuri ambayo humu tumekuwa tukimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu niwashukuru na niwapongeze watumishi safi wa Umma na tuendelee kuwatia moyo ili wao sasa wasihamie kwenye lile kundi la wengine ambao tunakubaliana hapa kwamba mwisho wa siku tushughulike nao kisawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye maeneo matatu yaliyosemwa kwenye Wizara ya Nishati, nikikubaliana na hoja na ushauri wa maeneo mengine ambao umetolewa kwenye taarifa ya *CAG* na kwenye Taarifa za Kamati. Yale ambayo sitayasema kwa taarifa zilivyo, tunakubaliana na tunachukua ushauri na maoni na maelekezo yaliyotolewa kwenye taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye eneo la kwanza la *Symbion*. Sitakuwa na mengi sana ya kusema hapa kwenye eneo hili. Mkaguzi amekagua *objectively* na ametoa maoni yake na yalikuwa matatu. Ameshauri mikataba isimamiwe vyema kwa kuwashirikisha wanasheria; pia ameshauri kabla ya kuivunja, basi tuhakikishe kwamba tunaangalia mapato na hasara za sasa na za baadaye; na pia ameshauri kwamba zile pesa ambazo zimelipwa na Serikali zitizamwe namna bora ya kuziweka kwenye vitabu na hesabu za Serikali ili mikeka ikae vizuri. Hayo ndiyo maoni ya *CAG,* nasi tunakubaliananayo na tunayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye eneo la mazuri yaliyotokana na malipo yaliyofanywa baina ya Serikali na huyo aliyekuwa *Symbion*. Nadhani huko panaweza pakawa panafaa zaidi. Wakati kesi inapelekwa Mahakamani, ilipelekwa ikiwa inadaiwa jumla ya kama Dola bilioni moja na milioni mia tano na zaidi kidogo. Kwa majadiliano yaliyofanyika nje ya

Mahakama, imelipwa kama ilivyosemwa, milioni 153 ambazo zinakwenda kwenye bilioni karibia mia tatu na zaidi kidogo. Kwa hiyo, kwa upande wangu naweza kusema pesa nyingi iliokolewa tofauti na kama tungeendelea Mahakamani na kuwa na mafanikio yasiyokuwa chanya, yaani mafanikio hasi, kwa maana ya kushindwa katika kesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ule mtambo ambao umelipiwa zile fedha, sitaki kusema tumeununua; ule mtambo ambao umelipiwa fedha ikiwa ni maelekezo ya makubaliano, thamani yake kwa wataalamu walioifanya ni karibia Dola 120. Kwa hiyo, kwa kulipa milioni 153, maana yake ni kama tumenunua mtambo. Hizo 153 ndani yake kulikuwa kuna deni la bili za kuuziwa umeme, kuna faini ya kuchelewesha yale malipo ya kulipia umeme na gharama za uwekezaji. Kwa hiyo, ukifanya hesabu ya kawaida, inaonekana kama tulichokifanya kilikuwa ni kitu ambacho ni kizuri kwa maana ya kuokoa pesa ya Serikali, ni kama tumenunua mtambo kwa gharama ambazo zilikuwa zina uhalisia.

Mheshimiwa Spika, mtambo huu wataalamu wameuhakiki na kuukagua kuona unaweza kufanya kazi kwa miaka 15 ijayo mpaka 30 bila kuhitaji matengenezo makubwa. Kwa hiyo, bado ni mtambo ambao uko vizuri na unaweza ukatusaidia kwenye kazi zetu za kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, tangu ulipoanza kufanya kazi mwezi wa pili baada ya kuwa umelipiwa mpaka huu mwezi Oktoba mwishoni umeshaizalishia Serikali jumla ya Shilingi bilioni 73 kwa kufanya kazi za kuuza umeme katika muda mfupi huu ambao umefanya kazi. Kwa hiyo kwa

hesabu hizo ndani ya miaka kama minne kuanzia tulipolipa ile pesa bilioni 153 za *dollar* ambazo zimelipwa juzi zitakuwa zimerudi kwenye Serikali na Serikali itaendelea kutumia mtambo huu kwa faida zake.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunayo chaangamoto ya upungufu wa maji kwenye vyanzo vyetu vya maji mtambo huu wa *Symbion* unatumia gesi na hivyo sisi kama Serikali kwa kutumia gesi tuliyokuwa nayo na mtambo wetu tuliyoupata baada ya kumaliza ile kesi nje ya mahakama, tunautumia kupunguza *gap* la upatikanaji umeme kwa takriban *megawatt* 112 ambazo zinatoka kwenye mtambo huu. Kwa hiyo kwa ushauri wangu na kwa mchango wangu, nadhani yapo mazuri mengi ambayo mtambo huu unatupatia sisi kama Serikali na ni wa kwetu tunaumiliki sisi wenyewe. Kwa maoni na hoja ya *CAG* nadhani sasa itoshe tuachane na hii habari tuannze kusonga mbele kwa yale mazuri ambayo yamepatikana kwenye hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye eneo lingine la Mradi wa Mwalimu Nyerere. Kwa Nchi yetu ya Tanzania katika miradi mikubwa ambayo tunayo na tuliwahi kuwa nayo mmojawapo ni huu wa trilioni sita na bilioni 500 na zaidi. Ni faraja kubwa sana kwa nchi kuwa na mradi kama huu tunaoutekeleza kwa pesa zetu za ndani. Katika hili lazima tuipongeze Serikali.

Mheshimiwa Spika, pesa hizi zinapatikana kwa wakati katika yale maeneo ambapo Serikali ya Awamu ya Sita imehakikisha inalipa pesa kwa wakati bila kuchelewa hata siku moja madai yanapokuwa yamehakikiwa ni katika eneo hili la Mradi wa Mwalimu Nyerere. *CAG* alipokagua ameona mambo ya kushauri na kusonga

mbele na tunayachukua kwa sababu ni ya kuboresha. Nisemee mambo mawili tu kwa haraka haraka kwa sababu naona kengele ya kwanza tayari imegonga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mawili makubwa ambayo naona nichangie kidogo ni kuhusu muda wa kukamilisha mradi. Ni kweli mradi ulianza 2018 na ulitakiwa kukamilika ndani ya miaka mitatu ambayo ilikuwa ni Juni mwaka jana. Juni ilipofika mradi ulikuwa haujakamilika kwa sababu ambazo zinafahamika na zinavutana kati ya pande mbili ya Serikali na mtekelezaji wa mradi. Tulikuwa na *options* mbili sisi kama wasimamizi, tu-*abandon* mradi kwa sababu muda umeisha au tuwe weledi na wazalendo tuendelee na mradi kwa ku-*extend* muda huku tukiendelea kuvutana na kubishana kuhusiana na nani mwenye haki, kwenye nini nani kamchelewesha nani na nani kafanya nini? Busara zilituonyesha tutoe kitu kinachoitwa *ex-gratia grants of extra time* ya kufanya kazi *extension of time* wakati tukiendelea na majadiliano mengine, nani amechelewesha nini? Nani anamdai nani nini? Nani anatakiwa kumlipa nani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na wachangiaji wengi hapa Wabunge ambao wamechangia, kuna suala ambalo tunaliona labda kama huyu mkandarasi alikuwa anamaliza Mwezi Juni na amechelewesha mradi na kimsingi yule anaye chelewesha mradi ndiye anaetakiwa kuomba Serikali au

kuomba aongezewe muda. Sasa hoja iliyokuja ni kwamba mtu amechelewesha mradi halafu ameongezewa muda, ameongezewa na fedha na wataalam wetu mahiri kabisa waliofanya ule mkataba walikuwepo, Watanzania kabisa wazalendo wamefanya ile mikataba, wakakubaliana kwa ngazi yeyote kwamba mradi utaisha mwezi Juni, sasa hii ya kuongeza muda na kuongeza fedha ufafanuzi wake ukoje labda inakuaje hii? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mchangiaji hajatoa taarifa, lakini katika mchango wangu sijasema tumeongeza gharama za mradi na nimesema kuhusu kuongezeka kwa muda wa utekelezaji. Kwa hiyo sijasemea kuhusu kuhusu kuongezeka kwa gharama za mradi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani nia ni kwamba kwa sababu hii mikataba ambayo tunaingia kwa maana ya Serikali pamoja na hawa wenzetu ambao tunaingia nao mikataba kwa kutoa huduma mbalimbali, upande wa Serikali inaonekana kwenye mikataba pengine si yote, lakini mingi kuwa inalipa ile pesa ya riba kwa kuchelewesha malipo. Sasa huyu mwingine anapochelewesha yeye, Serikali kwa sababu wataalam wapo na mikataba ipo na yeye upande wake analipa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mkandarasi ana madai yake kwa Serikali na Serikali ina madai yake kwa mkandarasi na kama

tungekaa kwenye kuvutana na kubishana tu-*establish* nani mwenye haki gani kwanza ndio tuendelee na mradi mpaka sasa mradi ungekuwa umesimama. Kwa hiyo alipoomba *extension of time* kwa sababu alizozileta na akiomba kuongezewa pesa, tumekataa kumwongezea pesa, tumemwambia kwa sababu tuna madai yetu kwako na wewe una ya kwako kwetu hatuja-*resolve*. Sasa tutakuongezea muda usiokuwa na hayo masharti ya kuongezewa pesa au kuongezeka kwa kitu kingine, tuendelee kutekeleza mradi kwa sababu pesa tunazo na wakati huo tukiendelea kujadiliana nani mwenye haki ya kupata nini.? Kwa hiyo hakuna ambaye mpaka sasa amemdai na kufanikiwa kwa mwenzake kulipa hela ya ziada na sisi tunachokisema ni kwamba hatutalipa pesa ya ziada kwa sababu tunayo madai yetu kwake tukionyesha yeye ndiyo kachelewesha mradi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wawili mmesimama, hiyo taarifa inahusu ufafanuzi aliotoa? Maana ndicho kinachoendelea sasa. Mheshimiwa Mpina

**T A A R I F A**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Mkataba wetu uko *very clear*, juu ya mkandarasi kuchelewesha mradi anatakiwa kufanya nini? La pili Waziri hapa anatueleza kwamba Mkandarasi ameomba *extension of time* na Serikali ika-*grant extension of time*, *base* ya *extension of time* waliipata wapi? Kama hawajafanya tathmini ya kazi iliyofanywa na changamoto zilizopo? Utaipata wapi *base of extension of time* kama ujafanya tathmini?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimeshawaanbia anayeruhusiwa kuuliza maswali ni mimi. Mheshimiwa Naibu Waziri hoja yako imeeleweka, sasa haya maswali ya Mheshimiwa Mbunge, ni maswali, kwa hivyo siyo taariafa. Kwa hiyo endelea na mchango wako wako.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna taarifa nyingine nyuma yako. Mheshimiwa Kigwangalla.

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nilipenda kumpa taarifa mchangiaji anayezunguza kwamba wametoa *extensions* ya muda *ex-gratia* kwa *favor*, kwa huruma, lakini kule kucheleweshwa kwa utekelezaji wa Mradi kwa zaidi ya miaka miwili kumesababisha mazingira ya utekelezaji wa mradi huo yabadilike. Kwa mfano; kuchelesha tu tayari kunabadilisha *exchange rate* ya kati ya *dollar* na shilingi na hatimaye leo hii wanapomlipa pesa nyingine za kukamilisha huo mradi wanamlipa kwa *exchange rate* ya sasa na hasara ambayo imeingia ni zaidi ya bilioni 110 kwa kuchelewesha tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hili jambo nilikuwa najaribu kuangalia hapa kwenye hivi vitabu vya Kamati wameandika azimio kwa namna gani, lakini hoja hii imeshawahi kufafanuliwa hapa na Mheshimiwa Waziri na kueleza ule mradi umechelewa kwa sababu zipi? Alitoa maelezo, lakini sasa kwa maelezo

anayotoa hapa Mheshimiwa Naibu Waziri ni maelezo ambayo ni mahususi kwa zile hoja ambazo zimejitokeza hapa, lakini kwa maana ya yale maelezo ya jumla kukusu mradi Mheshimiwa Waziri wa Nishati alishawahi kusimama hapa Bungeni na akaeleza sababu.

Sasa sisi sasa hivi ili tujielekeze vizuri tuko kwenye hoja hizi hapa za Kamati na tunataka tufike mahali ambapo mchango wa Serikali kwa sasa na wao wanachangia kama Wabunge, lakini utatusaidia Bunge kuazimia kwenye yale mambo ambayo Serikali hatujaweza kujiridhisha na kile ambacho wanasema. Kwa hiyo anachoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri ni kile ambacho kimeibuliwa kama hoja, lakini yale mengine ya jumla hayajaletwa bado na *CAG* na kwa sababu mradi unaendelea *CAG* atakuja atuambie tu, halafu kwenye ngazi hiyo ndiyo tutashughulika nayo kama haya tunayoshughulika nayo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Waziri, malizia mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Eneo lingine ambalo naona nilisemee kidogo ni kwenye gharama za mradi zinazohusiana na mabadiliko ya fedha. Miradi mikubwa kama hii inapotengenezewa mikataba inawekewa *component* mbili, mara nyingi *local component* na *foreign component* kulingana na kile ambacho kitatekelezwa kitatumia gharama zipi kubwa? Kwa ilivyofanyika katika mkataba huu gharama kubwa ya utekelezaji wa mradi huu ni mambo yanayotoka nje ya nchi. Kwa hiyo ilikubaliwa kwamba itakuwa ni asilimia sabini ya malipo yatafanywa kwa *dollar* na asilimia thelathini yatafanywa kwa shilingi ya Kitanzania, kwa sababu *supply* na mambo

makubwa yanapatikana nje ya nchi. Hivyo wataalam walitafuta njia nzuri na namna bora ya kufanya haya. Walijaribu kuhakikisha haifikii sabini ili tuweze kuokoa *exchange rate,* lakini kwa mazingira na uhalisia ulivyokuwa na wote mnaufahamu mradi huu hatuna haja ya kurudi huko sana ilionekana ibaki sabini kwa thelathini kwa sababu ya uhalisia.

Mheshimiwa Spika, suala pia la kufanya utaratibu wa *aging* ni kama ku-*secure* kufanya *insurance* ya malipo ya baadaye kwenye *exchange rate* yalitazamwa yote lakini hesabu hazikuleta faida. Kwa hiyo ilikubaliwa kwamba twende na utaratibu huu. Pia kipindi tunaingia mkataba *exchange rate* tuliyoi-*commit* ilikuwa na shilingi 2,224.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimwa kengele ya pili hiyo, dakika mbili malizia mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniongezea muda. Ilikuwa ni shilingi 2,224 kwa *dollar* moja. Tangu tumeanza kazi *dollar* imekuwa ikipanda na kuna muda fulani imefikia mpaka shi2,310.93. Sasa hii pesa bilioni 113 iliyowekwa nilihakikishie Bunge lako na Watanzania haijaliwa wala haijapigwa mtu, ni gharama halisia za mabadiliko ya pesa ambayo hata kwenye biashara zetu za kawaida yanatokea.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho kwa haraka haraka, ukwasi wa taasisi zetu ya *TPDC* na T*ANESCO,* naomba nipende kutoa mchango wangu katika hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kunti Majala.

**T A A R I F A**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na yote anayotueleza, pamoja na ucheleweshaji, pamoja na hizo *exchanging rate* lakini ikumbukwe kuwa mradi huu ulitakiwa pia utoe *CSSR* kwa jamii inayozunguka ule mradi, lakini mpaka leo zaidi ya bilioni 190 na hazijalipwa mpaka leo. Kwa hiyo hilo nalo waweze kuliona kama Serikali kwa namna gani mradi huu unavyoendelea kudidimiza Taifa letu kwenye suala hilo la mradi na mradi kutokuwa na tija kwa Watanzania.

**SPIKA:** Ungelikuwa umeishia hapo kabla ya swali lako ungekuwa umetoa taarifa, sasa umeuliza swali. Haya mchangiaji malizia mchango wako.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia mchango wangu kwa kuzungumzia ukwasi wa *TPDC* na *TANESCO*. Kwa mara ya kwanza katika historia chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *TANESCO* imepewa shilingi trilioni 2.4 kama mtaji na wenzetu wa *TPDC* wamepewa shilingi trilioni karibia 2.8 kama mtaji kwa ajili ya kuweza kujiendesha. Pesa hizi zimetoka wapi? Serikali imeamua kuchukua jitihada za makusudi za kubadilisha deni lake kwenye Taasisi hizi sasa ibadilike kuwa mitaji. Kwa hiyo yale madeni ambayo Serikali ilikuwa imezikopesha hizi taasisi, lakini inaendelea kulipa yenyewe imezibadilisha sasa ili ziweze kuwa mitaji

katika taasisi hizi na hivyo zitakuwa na uwezo wa kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wa Afya ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kushukuru sana kwa fursa hii ili kuchangia taarifa hizi za Kamati tatu. Napenda kupongeza sana Kamati zote tatu, Wenyeviti na Wajumbe kwa ripoti zao nzuri sana ambazo kwa kwa kweli kama nitakavyoeleza baadaye maazimio yao, *recommendations* zao tunazikubali kwa Wizara ya Elimu na nyingine tumeanza kuzitekeleza. Napenda vilevile kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia mjadala huu na maoni yao ambayo yamegusa Sekta ya Elimu hasa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tumeyabeba na mengine nitajaribu kuyatolea maelezo kidogo. Kwa hiyo mchango wangu pengine utakuwa nia mfupi kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu vilevile kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan hasa katika Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mambo makubwa sana ambayo yamefanyika kwa kipindi kifupi ambacho amekuwa Rais wa Nchi yetu, ujenzi wa shule nyingi wote tunauona, ujenzi wa vyuo kwa mfano sasa hivi najua kila Mbunge tukiongea naye anaulizia kuhusu *VETA*, lakini makubaliano

tumeshafanya na Hazina kwa maelekezo ya Rais wetu ni kwamba fedha tuliozonazo za *VETA* zitajenga *VETA* katika kila wilaya ambayo sasa hivi haina *VETA* mradi tupate ardhi. Vilevile ujenzi wa *campus* ya Vyuo Vikuu katika mikoa 14 ambayo ilikuwa haina *campus* ya Vyuo vikuu. Kwa hiyo mafanikio haya na yenyewe ni mazuri sana yanaleta vilevile changamoto kwa sababu tunaongeza idadi ya wanafunzi ambao wanahitaji fursa ya kusoma na kazi yetu kubwa ni kupambana na hizo changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala kubwa ambalo limezungumzwa hapa ni kuhusu Bodi ya Mikopo kwa Elimu ya juu na nitajaribu kuelezea kwa kifupi yale ambayo yameelezwa na Kamati na yale ambayo tunakusudia kuyafanya. *CAG* mwenyewe ametoa *recommendation* kubwa kwamba tufanye maboresho ya Sera na Sheria ya Bodi hii na vilevile tuhakikishe kwamba Wizara inaongeza usimamizi na kuimarisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya kuimarisha bodi hii. Mambo mengine ambayo yametajwa na *CAG* ambayo yamerudiwa na *PAC* ni masuala kama vile kugundua yatima ambao waliomba mikopo ambapo kwa vigezo ambavyo vilitakiwa vitumike, walitakiwa wapate mikopo, vilevile kasi ya kushughulikia rufaa kwa mtu ambaye ameomba mikopo, lakini hakuweza kupata na nadhani kwamba kwa vigezo ambavyo vimetangazwa angeweza akapata na vilevile kuangalia wale wanaostahili.

Mheshimiwa Spika, *CAG* vilevile amezungumzia kuhusu endapo *mini testing* yaani mfumo tunaotumia kutambua nani apewe mkopo na apate kiasi gani kama kweli tunatumia taarifa za kutosha kuweza kuhakikisha

kwamba kweli tunawalenga wale ambao tunahitaji kuwapata.

Mheshimiwa Spika, taarifa vilevile ya *PAC* imepitia humo humo na maazimio ambayo wameyapendekeza yapo katika mfumo huo huo. Mambo kwa mfano ya sera na sheria, vilevile mfumo wa usimamizi na kwa sababu taarifa zote mbili zinazungumzia umuhimu wa Wizara kuhakikisha kwamba inafanya usimamizi wa bodi na kusimamia vilevile mfumo wa kitaasisi na *PAC* ina-*recommend* vilevile Msajili wa Hazina naye *a-play role* yake katika kuimarisha suala hili.

Mheshimiwa Spika, mengine ambayo yamezunguzwa na *PAC* ni pamoja na hilohilo la *mini testing* ambayo inatumika wanaona kwamba pengine inahitaji taarifa nyingi zaidi na imetambua kwamba mahitaji ya mikopo kwa kweli yanaongezeka sana na yameongezeka zaidi baada ya nyongeza kubwa ya bajeti ambayo ilifanyika mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kuna lingine moja hapa ningependa nilizungumzie kidogo, kwenye taarifa ya *PAC* nili-*clarify* kidogo tu, kwa sababu katika ripoti pameelezwa kwamba *mini testing* inaangalia *needs* kwa ajili ya kujua nani anaweza akapata mkopo na haiangalii aina ya shahada mtu anayeisoma na tutahitaji kuweka maelezo vizuri zaidi kwa sababu ziko *cluster* tatu. *Cluster* ya kwanza inapewa upendeleo zaidi; ya pili upendeleo wa pili; na ya tatu. Kwa hiyo inaangalia mahitaji ya kaya na mtoto anakotoka na vilevile ni masomo gani anaenda kuyasoma? Hivyo ndiyo vigezo vinavyotumika, tunahitaji pengine kuweka ufafanuzi ili viweze kueleweka vizuri zaidi hapa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala huku kumekuwa na masuala mengi vilevile ya kuelezea umuhimu wa kuhakikisha kwamba kuna haki katika kugawa mikopo. Kwanza nianze kusema kwamba tangu tuanzishe Bodi ya Mikopo kumekuwa na uboreshaji wa namna ya kugawa mikopo na nitatoa mfano.

Mheshimiwa Spika, hapo mwanzo taarifa zilizokuwa zinatumika zilikuwa haziingizi taarifa kwa mfano ya *TASAF,* sasa hivi Bodi ya Mikopo inaruhusu kuchukua taarifa moja kwa moja kwa mwombaji wa mkopo ambaye anatoka kwenye kaya ambayo imeonekana ina mahitaji ya kusaidiwa na *TASAF* moja kwa moja achukuliwe kama ni anatoka kwenye kaya yenye uhitaji mkubwa kwa hiyo, anapewa upendeleo hivyo hiyo ni taarifa ya ziada ambayo inatumika sasa hivi. Pia Bodi ya Mikopo sasa hivi imefungamana na *RITA* kwa mfano kwa ajili ya kutambua watoto ambao ni yatima kwa hiyo, ukitoa taarifa yako inaweza ikawa *verified* mara moja na hali ikaenda vizuri. Hivyo, kumekuwa na *improvement* mwaka hadi mwaka ikiwa ni pamoja na jitihada za kuongeza makusanyo kwa wale ambao walinufaika na mikopo kuhakikisha kwamba wanarudisha mikopo yao.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka.

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba, katika hicho anachoongelea kuhusu uboreshaji wa utoaji mikopo na amesema moja ya *improvement* yao ni kuingiza taarifa za *TASAF*. *TASAF* bado yenyewe kule kuna shida kubwa kwamba mpaka hata hao wanaopewa hiyo fedha au ule unafuu wa kusaidia kaya maskini kule kwenye *TASAF* kwamba, wapo wanaopewa ambao siyo wenyewe ama wanapewa ambao siyo walengwa. Wapo ambao wanao uwezo na bado wanaingizwa kwenye *TASAF*. Tunayo malalamiko hayo mengi, kwa hiyo, nadhani pia taarifa za *TASAF* haziwezi kufanya *improvement* kubwa kwenye mikopo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, unaipokea taarifa hiyo.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba niipokee taarifa hiyo kwa maana kwamba, Serikali tuna haja ya kuboresha maeneo yote kuhakikisha kwamba, taarifa ambazo zinakusanywa ziko sahihi, lakini hii hatua ya bodi ya kuanza kutumia Taarifa ya *TASAF* ni *attempt* ya kuhakikisha kwamba tunapata taarifa nyingi zaidi kumtambua mtoto mwenye mahitaji, lakini kwa kweli mfumo mzima unahitaji kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala lile la sera ambalo naona liko katika mapendekezo ama maazimio hapa. Kweli, kwamba, kuna haja ya kupitia sera na matokeo ya kisheria ya *higher education financing* hapa nchini pamoja na mfumo wa kitaasisi. Sasa hivi tunapitia

sera ya elimu na ninapenda kutoa taarifa kwamba ni kama tumeshamaliza mapitio ya sera sasa hivi, tunasubiri tu mfumo wa *approval* ndani ya Serikali halafu tutatoa *almost like a white paper* kwa ajili ya majadiliano ya mwisho kabla ya kwenda kufanya maamuzi kupitia Serikali nzima na suala hili la namna ya ku-*finance higher education* ni suala ambalo limezingatiwa katika mapitio ya sera na kwa hiyo, liko kwenye azimio hapa nasi tayari tumeshatangulia tunakwenda hukohuko. Hiyo, itaendana vilevile na kupitia mapitio ya Sheria ya Elimu pamoja na sheria nyingine ambazo zinahusiana na utoaji wa mikopo kwa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, vilevile suala la Wizara kuongeza *oversight* kwenye Bodi. *Progress* imekuwa ikiongezeka lakini sasa hivi tutazingatia zaidi, vilevile kupitia mfumo wa kitaasisi ambao utatuhakikishia kwamba kwa kweli tuna-*improve* kwa sababu kila siku kuna *room* ya ku-*improve*. Suala moja kubwa ambalo ningependa nilizungumzie kama ambavyo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa ni suala la kuhakikisha kwamba mikopo inagawanywa kwa haki.

Mheshimiwa Spika, wengi wamelizungumza na kwenye taarifa ya *CAG* ameeleza, watu ambao wanapewa mikopo ambao yeye alivyowaangalia kama *sample* ameona kwamba hawakustahili kupata mikopo, wengine wamepata mikopo zaidi kuliko walivyostahili, hili ni suala ambalo na sisi tunalitilia umakini sana. Wakati nilipozungumza hapa mara ya mwisho, nilizungumza kwamba tumeweka Kamati ya wataalam wa mifumo na takwimu, wanaweza wakafanya *programming* kuweza kuchukua takwimu zote na kuzichakata na kuzi-*cluster* kuangalia vigezo na kuhakikisha kwamba, tunahakiki

kweli wale waliopata mikopo kama wanakidhi vigezo ambavyo vilitangazwa. Inawezekana vigezo hivyo tusiridhike navyo, lakini madhali ndiyo vilivyotangazwa tunataka kuangalia *compliance* yake ikoje.

Mheshimiwa Spika, Pili, Kamati hii itaangalia vilevile ni taarifa zipi za ziada ambazo tukizitumia zitaongeza ubora wa *mini-testing* kama ambavyo *CAG* mwenyewe amesema tunahitaji kuboresha taarifa hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa hapa kwamba Kamati imeshaanza kazi, inaendelea na kazi kwa bidii kabisa na itafanya kazi hiyo itamaliza. Kamati hii kwa sababu ina wataalam wa mifumo, takwimu na *programing,* siyo watu wa kwenda kufanya *sampling,* ni watu ambao wanaweza wakakaa kuandika *program* na kuchakata takwimu zote za watu ambao wameomba mikopo na kuhakikisha kwamba, wanajua kama tumekuwa tukizingatia vigezo ili tuweze kupata *recommendations* tujue tunakwendaje.

Mheshimiwa Spika, sote wote kama Serikali tunajua umuhimu kwamba fedha zilizopo kwa ajili ya mikopo kila mtu anasema hazitoshi, zitaongezwa zitakuwa hazitoshi, zitaongezwa hazitoshi, basi kile ambacho tunacho kigawanywe kwa haki, anayepata mkopo awe kweli yule anayestahili na ambaye kwa kweli anajiwezaweza kama fedha hazitoshi asije akaingia kule.

Mheshimiwa Spika, suala hili tusipolizingatia malalamiko yatakuwa makubwa sana. Kwa hiyo, napenda kusema Kamati iko kazini na imeongezewa nguvu leo, vilevile itakuwa na fursa ya kutangaza kwa watu wenye taarifa za kupeleka kwenye Kamati, nje ya

takwimu zilizopo kule watazipeleka kwenye Kamati tutapata taarifa hatimae tutajua tuweze kuongeza nini katika yale tunayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ya ziada ni pamoja na kama nilivyosema pale kwamba, mikopo ya elimu ya juu kama *CAG* alivyosema ni kweli tunahitaji kutafuta vyanzo vingi zaidi. Kulikuwa na *recommendations* huko mwanzo kwamba tuweze kutoa mikopo hata kwa wale wanaofanya *Diploma.* Kwa sasa hivi tumeznza na *NMB* tumepata Bilioni 200 na masharti yake, ingawaje masharti nafuu sana kwa mikopo ya elimu, lakini tutaendelea kufanya hivyo kuhakikisha kwamba, tunaboresha *education financing* hapa nchini, hasa *higher education financing* na *financing* hasa kwa hivi vyuo vya kati kama *VETA* na vingine vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa muda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Niwakumbushe tu wachangiaji, hasa upande wa Serikali kwa sasa, kwa sababu haya maazimio yatakapofanywa na Bunge na ninyi mtakuwa mpo humu ndani. Kwa hiyo, lengo hasa la kutoa hii fursa ni ili Bunge litakapofikia haya maamuzi muwe mmeshapata nafasi, siyo kwamba ninyi mlikuwepo halafu mkanyimwa nafasi ya kutoa ufafanuzi halafu Bunge likafanya maamuzi. Kwa hiyo, ni vizuri sana mkijielekeza kwenye hizi hoja ambazo zipo mbele yenu ambazo Bunge linaenda kufanya maamuzi juu ya hizo.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya,

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi, ninakupongeza kwa namna ambavyo umeendesha mjadala huu, pia ninakupongeza kwa kazi nzuri ambayo unaifanya.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anaendelea kuliongoza Taifa letu, vilevile Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na viongozi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwashukuru Kamati, hususan ya *LAAC* pamoja na *PAC* kwa taarifa zao, zaidi kwa michango, maelekezo na ushauri mbalimbali ambao pia wameweza kuutoa, bila kuwasahau Waheshimiwa Wabunge wote walioweza kuchangia hoja hizi. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, kunakuwa na thamani halisi ya matumizi ya fedha kwa hiyo, kipekee tunawashukuru sana kwa ushauri mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze katika kuchangia hoja hizi, ninaomba niweze kuanza na hoja ya kwanza kwa upande wa *LAAC* na baadae muda ukiruhusu nitaenda hoja za *PAC*. Kwa upande wa *LAAC* kulikuwa kuna hoja za aina mbalimbali za hati za ukaguzi ambazo zimekuwa zikitolewa, ninapenda tu kushukuru kwa namna ambavyo wameeleza mitiririko mbalimbali, lakini na mimi nipende kusema kwamba, ukiangalia mwenendo mzima wa ukaguzi na hati mbalimbali

ambazo zimekuwa zikitolewa za ukaguzi utaona namna ambavyo kumekuwa na kuimarika katika nidhamu, hususan nidhamu ya mapato, matumizi, pia namna ambavyo uandaaji sasa wa taarifa zetu mbalimbali za hesabu za mwaka ambavyo zimekuwa zikiendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia nikiainisha miaka miwili ya fedha iliyopita, huko nyuma ukienda na mwaka 2021 katika hati ambazo zilikuwa zinaridhisha, ukiangalia katika mwaka 2019/2020 tulikuwa tuna hati 124 ambazo zilikuwa sawa na asilimia 67. Halmashauri 124 ndiyo zilipata hati safi, lakini ukiangalia kwa mwaka 2020/21 takribani Halmashauri 178 ambayo ni sawa na asilimia 96, unaona namba inazidi kuongezeka, ni kweli bado zipo Halmashauri ambazo zina hati zisizoridhisha, lakini walao unaona namna ambavyo Serikali inachukua hatua katika kuimarisha nidhamu ya mapato. Tunaendelea kuahidi Bunge lako Tukufu tutaendelea kusimamia kwa umakini kuhakikisha kwamba, kunakuwa na matumizi sahihi, kuhakikisha kwamba taarifa zetu zinazingatia vigezo vinavyohitajika na kwamba, tunakuwa na hati zinazoridhisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukiangalia kwa mwaka 2019/2020 kwa hati zenye mashaka. 2029/2020 tulikuwa na Hati zenye Mashaka 53 ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 29, kwa mwaka 2020/2021 utaona zimepungua hadi kufikia hati Sita ambayo ni sawa na asilimia Tatu. Kwa hiyo, utaona kutoka Halmashauri 53 kwenda kwenye Halmashauri Sita, hata hizo Sita hatutaki ziwepo, lakini walau utaona kuna maboresho ambayo Serikali imeendelea kuyafanya na hatua zimechukuliwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Halmashauri zenye Hati Mbaya. Ukiangalia katika mwaka 2019/2020 ilikuwa ni takribani Halmashauri Nane zilikuwa na Hati Mbaya, lakini kwa mwaka 2021 ni Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambayo Mheshimiwa Getere ameisemea kwa umakini na ninaamini huko mbele ataendelea kusimamia kwa umakini na yeye kwa kuwa anaingia katika Kamati ya Fedha ili kuhakikisha kwamba, tunapokuja katika miaka mingine tumetoka Nane, tuko Moja na ikiwezekana miaka ijayo basi iwe ni Halmashauri 0 kabisa na ninaamini hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapenda kusema kwamba kwa kweli mengi ya haya yametokana na kazi nzuri mnayoifanya *LAAC* pamoja na Kamati zingine. Tunaendelea kuwashukuru kwa mara nyingine tena, tunaahidi kuendelea kusimamia maelekezo yenu, pia ushauri mbalimbali na maelekezo ya *CAG* kama ambavyo yanabainishwa katika hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kujielekeza katika hoja ya matumizi yasiyofaa, hususan katika Akaunti ya Amana ambayo imesemwa sana hapa. Kimsingi ninapenda kusema kwamba, akaunti hii ya amana katika Halmashauri mara nyingi inawekwa kwa ajili ya fedha maalum. Unakuta zinawekwa fedha nyingine kwa ajili ya kulipia labda Wakandarasi au kunakuwa kuna shughuli maalum hela zimehifadhiwa hapo. Upo mwongozo tayari umeshatolewa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuhusiana na matumizi na usimamizi wa akaunti hii. Kipekee tutaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba, watu wote wanaosimamia akaunti hii wanasimamia ipasavyo na watakapokuwa wametumia fedha katika akaunti hii ya amana kinyume na utaratibu

na miongozo basi hatua stahiki zitaweza kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili suluhu ya yote tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuona ni kwa namna gani sasa fedha zote zilizoko humu ndani zinakuwa *ring fenced* na zisiweze kutolewa bila utaratibu ili kuhakikisha kwamba kweli zinatolewa kwa madhumuni yale tu yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Tatu kuhusiana na ruzuku ya miradi ya maendeleo kutolewa tofauti na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Katika hili tutaendelea kukaa na Wizara ya Fedha kuona ni namna gani bora ya kuweza kutekeleza ushauri ambao Kamati yetu ya *LAAC* imeweza kuutoa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Nne ya udhauifu katika usimamizi wa manunuzi, hasa pamoja na mikataba. Tunapenda kusema kwamba, tumeshachukua hatua mbalimbali. Ukiangalia mpaka ilipofikia Agosti mwaka huu, tuliweza kuchukua hatua kwa watumishi 116 kama awamu ya kwanza na tumezielekeza ofisi zetu za Makatibu Tawala wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kwamba, inapofika tarehe 15 Novemba, wanaleta hatua ya pili ya utekelezaji wa ni namna gani wameweza kuchukua hatua kwa wote ambao wameonesha udhaifu katika usimamizi wa mikataba, vilevile katika usimamizi wa manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa mchanganuo, ukiangalia tayari tunao watumishi zaidi ya 22 wameshafikishwa Mahakamani, tunao watumishi zaidi ya 23 wameshafikishwa Polisi na TAKUKURU. Tunao watumishi

Watatu wamefukuzwa kazi, watumishi 20 tayari vilevile wamesimamishwa kazi, tunao watumishi takribani 47 ambao kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi wamepewa barua ya onyo, vilevile tunae mtumishi Mmoja ambaye ameshushwa cheo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kutoa taarifa kwa mchangiaji kwamba, huko tunakoelekea sasa kwa maeneo anayozungumzia kumekuwa na tabia ya Watumishi wa Serikali kutoka TAMISEMI wanapokuwa wamekwapua maeneo mbalimbali, dakika mbili amepata barua ya kuhamishwa, ikiwepo Bunda sasa hivi wameagiza magari ya sensa, sensa imeisha magari hayajaja, tayari aliyekuwa anashughulika na sensa ana barua anapishana na Madiwani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, huo ulikuwa tu ni mfano wa hizo changamoto, lakini unaweza kuwa huna taarifa nayo hapo. Kwa hiyo, endelea na mchango wako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, labda nikijielekeza hapohapo tayari ukiangalia katika Manispaa ya Ubungo, Rorya, Mwanza, wako watumishi ambao walihamishiwa Makao Makuu ya Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa na tumewarudisha katika Halmashauri hizo kuweza kujibu hoja zao. Tukifuatilia pia kwa Halmashauri ya Bunda kama na yenyewe ikithibitika hatutasita pia kuwarudisha katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kuweza kujibu hoja zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumevua vyeo zaidi ya watumishi 57. Wako Waweka Hazina zaidi ya 15 vilevile tumeweza kuwavua vyeo, Wakuu wa Idara ya Utawala na Utumishi zaidi ya 14, Maafisa Mipango Watatu, Wakuu wa Vitengo vya Ukaguzi Watatu. Vilevile kwa watumishi takribani 384 ambao wamekaa kwa muda mrefu hasa Wakuu wa Idara wa *DHRO, DPMUs,* watu wa *Internal Auditor* na wengine na wenyewe pia tumewahamisha katika maeneo mbalimbali. Sasa hivi tunaandaa fedha kuhakikisha kwamba, watumishi waliokaa kwenye kituo kimoja zaidi ya miaka Saba wanahamishwa ili kuhakikisha tunaweza kuchukua hatua stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya Tano kuhusiana na udhaifu katika uwekezaji wa mitaji ya umma na katika miradi ya Halmashauri. Kwenye eneo hili kulikuwa kuna malalamiko kwamba, kumekuwa na uwekezaji ambao mwingine ulikuwa ukifanyika bila kuwa na upembuzi yakinifu, lakini bila kuwa na maandiko ya miradi. Ni kweli baadhi ya Halmashauri umekuta wengine pia wakiiga aina ya miradi hasa ya stendi na masoko, vilevile wengine wamekuwa wakipeleka hela katika uwekezaji katika benki ambazo hazina utendaji unaoridhisha na bila kufanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tu kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sasa tumeshaandaa muongozo wa namna ya uandishi wa miradi mbalimbali ya uwekezaji

katika Halmashauri zetu, vilevile tumeshirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la *UNCDF,* tayari tunayo Kamati ya Kitaifa yenye wajumbe au wataalam takribani 44, wameshapatiwa mafunzo wa kutoka TAMISEMI, Wizara ya Fedha pamoja na mamlaka zingine mbalimbali kuhakikisha kwamba, tunakuwa na mwongozo sahihi na tunaendelea kuwafundisha wataalam wa Halmashauri ili wanapoandaa miradi ya uwekezaji na mingi ni katika miundombinu, kuhakikisha kwamba wanakuwa na ubobezi na wametimiza vigezo vinavyohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuanzia Julai 2022 tunashukuru Mheshimiwa Rais aliweza kuidhinisha muundo wa kiutumishi wa Halmashauri zetu au Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na muundo huu umeshaanza kutumika na kwa sasa tunayo Idara na *Section* mpya ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Lengo kubwa la kuanzisha Idara hii ni kuhakikisha kwamba, kabla Halmashauri hazijaja au hazijaanza kutekeleza miradi ya uwekezaji katika Halmashauri zao basi mapendekezo hayo au maandiko yanapitishwa katika Idara hiyo ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuweza kupitiwa, wanapojiridhisha pia hawatamaliza wenyewe kule, wataleta TAMISEMI nasi pia kwa wataalam wabobezi waliopo, watapitia na kujiridhisha endapo kweli miradi hiyo inayopendekezwa ya uwekezaji inakidhi vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye eneo hilo pia, eneo la tatu…

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kuna taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nasi tungekuwa tunawasimamisha hivyo kila dakika nadhani tusingefika hapa.

**MBUNGE FULANI:** Aah!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Ni haki yake ya msingi Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Charles Kajege, taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa msemaji, anaonesha kutaka ku-*deal* na tatizo kwa kumfukuza nani huyu… kuwafukuza watumishi na kuhamisha watumishi wa ngazi ndogondogo badala ya ku-*deal* na tatizo kubwa ambalo tunaliona kwamba, liko Makao Makuu, Mheshimiwa Waziri atuambie kuhusu hapo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sipokei taarifa hiyo. Naomba tupeane nafasi kidogo ili tuweze kumaliza hoja hizi.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunakamilisha mwongozo wa kusimamia miradi baada ya kukamilika hasa katika kuanzisha *special purpose vehicle* katika miradi yote ya

uwekezaji. Kama ambavyo imebainishwa katika changamoto mbalimbali na Kamati, tunapenda tu kusema kwamba, tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunazifanyia kazi kwa ukamilifu na tunaamini maboresho mbalimbali tuliyoyaeleza hapa kupitia masuala ya *SPV*, kupitia uanzishwaji wa Kitengo cha Biashara, Viwanda na Uwekezaji pamoja na mambo mengine basi tunaamini hili litaweza kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya usimamizi na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Yapo mapendekezo mbalimbali ambayo tunayapokea, kulikuwa na mapendekezo ya kuanzisha akaunti maalum kwa ajili ya fedha zitakazotolewa na kurejeshwa ziwekwe katika kumbukumbu za vikundi vinavyokopa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tu kuliarifu Bunge lako Tukufu, tayari hili limeshatekelezwa. Kuanzia mwaka 2021/2022 Julai, tayari kuna akaunti mbili za Halmashauri katika masuala ya mikopo. Akaunti ya kwanza iko Benki Kuu na akaunti hii inatumiwa na Halmashauri kuweza kuchangia asilimia 10 ya mapato ya ndani, vilevile ni akaunti ambayo inatumika kwa ajili ya utoaji wa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili au akaunti ya pili ni akaunti ambayo tumeifungua katika akaunti za kibiashara katika Benki ya *NMB* pamoja na *CRDB* ambayo ndiyo tunaitumia kwa ajili ya kupokea marejesho ya mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, la pili, marekebisho mengine ambayo tumeyafanya, kwa sasa tunao Mfumo wa Kielektroniki wa *Ten Percent Loan Management Information System.* Na kupitia mfumo huu ambao tumeshaanza kuutumia tangu Mei, 2022, tumeshaanza kuona mabadiliko katika suala zima la hali ya utoaji wa mikopo pamoja na urejeshaji wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, kuna mikopo ya nyuma (mikopo chechefu), tumeshakaa na halmashauri zetu pamoja na maafisa ustawi wa jamii kuweza kupata tathmini tangu mpango huu ulipoanzishwa mpaka sasa ni kiasi gani cha fedha zimetolewa, kiasi gani kimerejeshwa na kiasi gani bado hakijarejeshwa mpaka sasa. Tumewaomba taarifa za mpaka Juni, 2022 na tumewapa muda mpaka tarehe 30, Novemba, 2022 waweze kuwa wamewasilisha taarifa hizo za *backlog* ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, tunaamini baada ya kupata taarifa hizo na baada ya kusafisha data (kufanya *data cleaning),* basi tutaweza kuchukua hatua stahiki na kuhakikisha kwamba mikopo yote iliyotolewa inaweza kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, pia tumefanya marekebisho katika Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2019. Marekebisho haya yalifanyika mwaka 2021 ambapo kwa sasa halmashauri zimeruhusiwa kuweza kutenga fedha kati ya shilingi milioni sita hadi 60 kwa mwaka ili kuzitumia fedha hizo kutoa mafunzo ya kiungozi, kiutawala, usimamizi wa fedha, uendeshaji wa miradi na utoaji wa taarifa kwa vikundi vyetu.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo pia – kati ya milioni sita mpaka 60 kwa halmashauri – zitaweza pia kutumika kufanya ufuatiliaji wa mikopo na tathmini ya namna ambavyo vikundi vinavyopata mikopo hiyo vinaendelea.

Mheshimiwa Spika, tunaona mabadiliko, tumeona hoja kwamba fedha nyingi zinatoka, na hata ukiangalia mwaka huu zaidi ya bilioni 75, na kwa kweli ni lazima fedha zote zilizotolewa ziweze kurejeshwa. Tupende tu kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba ukiangalia kuanzia mwaka 2019/2020 na 2020/2021 utaona namna kiwango cha mikopo kinachotolewa. Huko nyuma ilikuwa inaanza kutoka kwa asilimia 65, lakini kwa sasa, mwaka 2021/2022, takribani asilimia 90 ya mikopo imeweza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa marejesho, mwaka 2019/2020 marejesho yalikuwa kwa asilimia 72 na mwaka 2021/2022 marejesho sasa yamefikia asilimia 84 na tunaendelea kuimarisha suala hili. Tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wameliongea kwa hisia kali. Kwa kweli hizi fedha si msaada, zinatakiwa kweli kuwa ni mikopo na ni mikopo ambayo imetolewa kwa masharti nafuu. Kwa hiyo na sisi tunapokea hoja hiyo na tutaendelea kuimarisha mifumo kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye utoaji wa asilimia mia na hatimaye pia urejeshaji uwe kwa kiwango kikubwa kinachoridhisha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya baadhi ya stahiki za watumishi kutolipwa ipasavyo, wengine michango yao ya hifadhi ya jamii imekuwa haipelekwi kwa wakati, hali ambayo imewaathiri wakati wanapostaafu, posho za likizo, gharama za uhamisho, gharama za masomo pamoja na posho nyingine nazo pia zimekuwa hazitolewi.

Mheshimiwa Spika, nikienda katika hoja ile ya watumishi waliostaafu katika halmashauri. Unakuta wengine wamestaafu lakini wameshindwa kulipwa mafao yao kutokana na baadhi ya halmashauri kutopeleka na nyingine ni shilingi laki mbili au tatu tu.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu tarehe 01, Novemba ilituita na tuliweza kufanya kikao pamoja na makatibu tawala wa mikoa na tumeshakubaliana kuweza kuhakikisha kwamba tunahakiki madai yote na kuhakikisha kwamba wanakuja na mpango kazi wa namna watakavyolipa madai yao hayo kwa ajili ya watumishi wetu hawa wa halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho tumekubaliana na mifuko yetu ya hifadhi ya jamii, kwa kiasi kikubwa kwa madai ambayo yamesababishwa na halmashauri mbalimbali kutopeleka michango, basi waweze kulipwa fedha hizo bila ya kuleta usumbufu kwa mtumishi aliyestaafu.

Mheshimiwa Spika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja, malizia mchango wako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nije kwenye hoja ile ya uthamini wa *DART*. Nipende tu kusema kwamba kwa wale wananchi wa eneo la Gerezani

kulikuwa na maombi hapa au maelekezo ya Kamati kuhakikisha kwamba taarifa ya tathmini inaangaliwa upya na kwamba walioshiriki basi wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema kwamba *PAC* ilielekeza nyaraka mbalimbali ziwasilishwe kwa *CAG* na sisi tutafanya hivyo na kuhakikisha kwamba *CAG* anapata nyaraka hizo ili apitie kwenye *valuation report* kuona kama kweli kilicholipwa kupitia yale malipo ya usumbufu na malipo ya uthamini ndicho ambacho kilistahili kulipwa au kuna malipo ya ziada au kama kuna mapungufu basi taarifa hiyo ndiyo itakayoelekeza.

Mheshimiwa Spika, kwenye hoja ya kuungua kwa Majengo ya Shirika la Masoko Kariakoo, na kwamba alipokwenda *CAG* kuna hati mbalimbali za takribani shilingi bilioni 3.5 hazikuweza kupatikana, na kwamba hii ilitokea baada ya *CAG* kubaini tu baadaye soko likaungua.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema kwanza, mwezi Aprili, 2021, tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliunda timu; kabla hata haya hayajajitokeza, kwa ajili ya kuangalia ubadhirifu mbalimbali; na tayari kuna hatua nyingine zinaendelea kuchukuliwa. Lakini kwenye hili la kufanya *forensic audit* tunakubaliana na Kamati na tutafanya mawasiliano na mamlaka zenye dhamana ya kufanya *forensic audit* ili iweze kufanyika. Na endapo kuna jinai yoyote basi iweze kuthibitika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwenye ushiriki wa wazawa kwenye *DART*.

**SPIKA:** Sasa muda umekwisha. Hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla iko kwenye hoja za *CAG* wa ni nje ya hoja za *CAG*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, *PAC*.

**SPIKA:** Ni hoja ya *CAG* au hapana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Ehee, *CAG* kasemaje kuhusu hilo? Endelea, sekunde 30. Yaani muda wako umeshaisha, huu mwingine ni wa Mawaziri wengine tayari.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, niombe kuwasilisha.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe na kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Lakini zaidi nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninamshukuru Rais wetu; hapa Bungeni mmetupitishia trilioni 1.1 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za afya, lakini yeye kwa kutumia

mbinu nyingine tumepata nje ya bajeti zaidi ya bilioni 891.5. Siyo kazi rahisi; una trilioni 1.1 halafu nje ya bajeti inapatikana fedha karibia na hizo zilizopo kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, hizi fedha zimepunguza rufaa za nje kwa zaidi ya asilimia 97. Tulikuwa na hospitali mbili tu za mikoa ambazo mpaka mwezi Februari zilizokuwa na *CT scan,* lakini sasa hospitali zote za mkoa zitakuwa na *CT scan.* Leo kwa mwezi Oktoba na Novemba tunakwenda kugawa *X-ray machines* 174 kwa nchi nzima kwa Wabunge wote na hakuna wilaya ambayo haitaguswa. Hii ni kazi kubwa sana ambayo Rais wetu ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakumbuka Mheshimiwa Rais alikwenda pale Muhimbili akapewa ripoti kwamba kuna watoto zaidi ya 500 ambao wana ulimi mkubwa wanaosubiri kwenda nje kutibiwa India. Rais wetu aliagiza pale na vifaa vililetwa na sasa watoto wote wametibiwa ndani ya nchi, hawajaenda nje, na wapo kwenye familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye hoja. Kulikuwa na hoja nyingi lakini naomba niende kwenye tatu. Hoja ya kwanza ni bima kutorejesha gharama za matibabu. Kwa mwaka 2021/2022 kwenye halmashauri zote madai yalikuwa bilioni 29.6 na sasa zimerejeshwa bilioni 26.6, kwa maana kuna asilimia nane ndiyo bado hazijarejeshwa kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sisi tumekwenda mbali zaidi na tumekwenda kwenye maeneo mbalimbali tumeangalia tatizo hili. Nitolee mfano sehemu moja ya Mkoa wa Kigoma. Tulikwenda tukawakuta kwenye bima tu peke

yake walikuwa wanapata milioni 70 kwa mwezi, lakini tulipokaa kwa kushirikiana na Wabunge, Serikali ya Mkoa na watumishi wa hospitali husika, walifanya mabadiliko na sasa ukienda Hospitali ya Mkoa wa Kigoma wanapata zaidi ya milioni 200 kwa mwezi kupitia bima.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatukuwa tunapoteza tu pesa kwenye eneo la marejesho lakini kulikuwa na pesa ambazo hazikuwa zinadaiwa nyingi sana kwenye eneo letu. Hilo eneo tumeshaliboresha. Na kuna makubaliano yanaendelea na TAMISEMI na Bima kuhusu pesa hizi ili waweze kupelekewa vifaa na vitu vingine ambavyo vitatiokea kule upande wa bima.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni kuisimamia *MSD* kupeleka vifaa kulingana na mahitaji. Moja, kuna hatua mbalimbali zilipendekezwa, hatua zote ambazo zilipendekezwa kwa ajili ya kuchukuliwa kutokana na matatizo yaliyokuwepo kwenye mfumo wa dawa zimeshachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, baada ya kuchukua hatua hizo tukaenda mbali zaidi tukasema kwamba kuna mambo yaliyokuwa yanasababishwa na masuala ya manunuzi, ucheleweshaji ulikuwa unasababishwa na manunuzi. Tulichokifanya pale tumeweka mikataba ya muda mrefu ili kuondoa hayo mambo ambayo yanachelewesha upatikanaji wa dawa kutokana na sheria za manunuzi kuchukua muda mrefu kila hitaji linapotokea.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo la halmashauri zetu kupeleka fedha *MSD* lakini dawa hazipelekwi kule kwenye halamshauri zetu. Tulichokifanya

hapa, kwa fedha ambazo tayari halmashauri wanazo, kama *MSD* hana dawa hizo, ndani ya saa 24 atoe *OS* ili halmashauri waweze kwenda kununua dawa sehemu nyingine badala ya kuchukua fedha na kuzipeleka *MSD* na wanashindwa kupeleka dawa sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, tunakwenda kushirikiana na kamati zetu za ulinzi na usalama kwenda kufika zaidi, tushirikiane pamoja kwenye kufanya kazi kwenye *medicine audit* na kutengeneza mfumo ambao tutaona dawa inapotokea *MSD* mpaka inaposhuka halmashauri na jinsi dawa zinavyotumika. Mfumo uweze kuonekana upande wa TAMISEMI na upande wa Afya, tuhakikishe kunakuwepo na *control* kubwa ya dawa na vifaatiba.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni eneo la uteketezaji wa dawa. Moja; kwa nini kumekuwepo na dawa nyingi zilizoteketezwa. Tumeona kwamba kulikuwepo na mabadiliko makubwa ya tiba, hasa kwenye eneo la Ugonjwa wa UKIMWI, maana kwenye eneo hilo mwaka 2018 na 2021 kumekuwepo na mabadiliko makubwa sana kwenye eneo la tiba. Lakini wakati mabadiliko yanafanyika kuna dawa tayari zilikuwa zimepelekwa kwenye *site*. Hizo dawa hazikutumika kwa sababu ya hayo mabadiliko na ni dawa zenye thamani ya bilioni 16.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo kumekuwa na mabadiliko ya teknolojia ambayo nayo yamesababisha vitendanishi aina mbalimbali vyenye thamani ya bilioni sita kuharibika. Na fedha hizi ni zile za wadau, na mara nyingi wanapeleka pesa lakini wakati huohuo wanakuja

na mambo kama haya. Hilo tumekwenda nalo kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kwamba vitu hivi vyote vitafanyika kupitia Mfuko wa *MSD,* siyo kufanyika tena *direct* kwenda kwenye mikoa yetu ili tuweze kufanya *reconciliation* na kuondoa hili ambalo limeonekana hapa.

Mheshimiwa Spika, kwenye mfumo wetu wa dawa wa manunuzi ya kawaida…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30, malizia.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwenye mfumo wetu wa kawaida kumekuwa na asilimia nane kweli ya upotevu wa dawa kama hiyo. Tumeshashughulikia maeneo yaliyokuwa na shida, kama alivyosema Waziri wa TAMISEMI, kuna mabadiliko makubwa sana yamefanyika, wakuu wa idara na mambo mengine. Wakati huohuo tunataka, ndiyo maana tunasema tunakwenda kukaa na kamati za ulinzi na usalama, tumekwenda Nzega tumekuta ndani ya hospitali duka la dawa linauza dawa bei ghali kuliko maduka yaliyozunguka hospitali. Lakini ni mkakati uliotengenezwa palepale ndani.

Mheshimiwa Spika, maana yake nini; tukishirikiana kwa pamoja, dawa hazitaharibika kwa sababu watu sasa wanakwenda kununua dawa nje ya hospitali badala ya

ndani na zinabaki zinaharibika. Hayo yote tumeshayafanya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia hizi hoja za Kamati tatu zilizoko mbele yetu. Nimshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuiwezesha vizuri sana sekta yetu inayosimamia usalama wa raia. Ni matarajio yetu kwamba kwa uimarishaji huu basi vyombo vyetu pia vitimize wajibu wao kwa kuzingatia matarajio ya Watanzania kama yalivyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia hoja hizi. Nikushukuru wewe binafsi kwa namna unavyoongoza mjadala huu na uvyotu-*guide* vizuri ili tuweze kuwawakilisha vizuri wananchi waliotuleta hapa. Mwisho nizishukuru Kamati zote tatu kwa michango mizuri zilizotoa kwenye sekta tunayoisimamia, na zaidi Wabunge waliochangia kwa kiango kikubwa kwenye maeneo ya uhamiaji na eneo la Polisi, hasa eneo la tozo lililotolewa azimio na Kamati yetu ya *PAC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu haya yaliyojitokeza Uhamiaji, hizo *concerns* za Kamati, za *CAG* na za Wabunge ni *very valid,* ni za msingi kabisa. Hakuna mtu ambaye anatarajia chombo kilichoaminiwa kije kifanye

mambo ambayo yanakiuka kabisa maadili. Na kwa kweli hata Mheshimiwa Rais mwenyewe wakati akifunga mafunzo ya askari wetu wanaoingia *Immigration* alisema bayana kwamba yapo mambo ambayo lazima Wizara na *Immigration* tuyafanyie kazi, hasa yale yanayohusika na ubadhirifu kwenye sekta hiyo ya *visa* na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi kama Wizara tunaungana na wote kusisitiza haja ya uadilifu, uaminifu, uzingatiaji wa sheria, uepukaji wa wizi na ubadhirifu kwenye maeneo yote yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara (Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Idara ya Uhamiaji) tunazingatia ipasavyo maelekezo ambayo mara kwa mara yamekuwa yakitolewa na *CAG* wakati wa ukaguzi na Kamati zetu hizi ambazo zinatusimamia. Mimi niwahakikishie kwamba wakati wote Wizara itashirikiana na *CAG* na Kamati za Bunge na Wabunge kuchukua hatua stahiki pale ambapo haja ya kufanya hivyo ipo.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya maelezo haya, naomba nigusie maeneo yaliyojitokeza kwa hisia kali miongoni mwa wasemaji na kwenye Ripoti ya Kamati. Nikumbushe tu kwamba hii ni Ripoti ya 2020/2021, kwa hiyo tunayoyaongea hapa sisi kwenye sekta huku kuna hatua zimeshachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, moja ambalo nimeliona likijitokeza hasa kwenye michango ya Wabunge, inakuwa kama vile pengine kuna kutilia shaka uwezo wa Wizara na pengine taasisi yetu ya *Immigration* kuchukua hatua.

Niwaondoe shaka Waheshimiwa Wabunge, wote tuko pamoja.

Mheshimiwa Spika, jambo moja juu ya hii habari ya *visa* zilizotakatishwa hizi. Baada ya uchunguzi ule Serikali ilichukua hatua, kwa sababu kulikuwa kunaonekana kuna jinai, *DCI* alilichunguza jambo lile kwa undani sana. Lakini uchunguzi ule haukumuwezesha kuwa na ushahidi ambao ukipelekwa mahakamani wale watuhumiwa wangeweza kutiwa hatiani.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoshauri *CAG* kwenye ripoti yake, *DCI* pia alishauri kwamba mamlaka husika za kinidhamu zichukue hatua. Naomba nilitaarifu Bunge lako kwamba *Immigration* imechukua hatua dhidi ya watumishi wote 32 waliotuhumiwa kuhusika na matendo yale na hatua za kinidhamu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa, wale waliokuwa na uongozi wametolewa na wengine tumewapa siyo chini ya miaka miwili hawawezi kufikiriwa kwa uongozi wowote ule. Tumewaweka kwenye matazamio wasifanye matendo kama hayo. Hata hivyo, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu ili yeyote atakayejitokeza kufanya mambo hayo yenye mwelekeo wa kijinai wanapelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la tuzo na tozo, tumesikiliza maoni ya Wajumbe na maoni ya Kamati. Ushauri wote uliotolewa tunaukubali na maazimio yale hatuna shida nayo kabisa. Isipokuwa nina mambo machache ambayo nadhani tuyatolee ufafanuzi ambayo baadhi ya Wabunge walisema kama vile sasa

ule mfuko hauna usimamizi kabisa. Nilimuona Mheshimiwa Sangu akiongea kwa uchungu sana juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, niwaeleze kwa kifupi. Mfuko huu upo kwa mujibu wa Kifungu cha 66 cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Nchini, Sura ya 322. Sheria ile imebainisha vyanzo vya mapato, lakini hata kwenye *PGO* Na. 135 aya ya pili na *PGO* 135 aya ya 2(b) yameainishwa mule maeneo gani yanaweza yakawa vyanzo vya mapato na mamlaka ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, na vyanzo vya mapato kama vinavyofahamika kwa mujibu wa sheria ni adhabu za makato ya mishahara kwa watumishi wanaofanya makosa ya kinidhamu, asilimia 50 ya mauzo ya mali za kuokotwa zinazokuwa polisi, makusanyo kutoka benki, taasisi, viwanda na migodi inayopata huduma za ulinzi toka Jeshi la Polisi. Na kwa sasa tuna jumla ya vyanzo 55.

Mheshimiwa Spika, akaunti hii iko *BOT,* maana yake Benki Kuu, na utaratibu wa matumizi umeainishwa vizuri sana. *IGP* kabla ya kuanza kutumia, huandaa mpango unaouwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara, naye ana-*share* na Waziri. Tukishajiridhisha ngazi ya Wizara, ndiyo anapelekewa *Paymaster General* kwa ajili ya kuruhusu fedha zitoke zikagharamie mpango ule ambao uliridhiwa kabla. Haamki tu akapanga hizi ziende zikatumike huku. Fedha hizi zinapofika kwa matumizi, huhamishiwa kwenye akaunti ya *Miscellaneous Deposit Account* iliyoko chini ya Wizara ya Fedha, akaunti ambayo huwa inakaguliwa.

Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba kutokuwepo kwa kanuni ni udhaifu ambao tumeanza kuufanyia kazi

kama Wizara na kabla ya *audit* ijayo tutakuwa tayari tunazo kanuni za kusimamia mfuko huu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naona muda wangu umeisha, lakini nimalizie tu kwa kusema, kulikuwa na hoja ya kutumia fedha hizi kama msingi wa kujenga kwa haraka vituo na nyumba za wafanyakazi. Hilo tumeanza kulifanyia kazi kwa kuwasiliana na *Banks* ili tuweze kupata fedha nyingi zaidi halafu mfuko ule utumike kurejesha.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nashukuru kwa hayo, lakini tuko pamoja na haya yaliyoshauriwa nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, na Watoa hoja wajiandae.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri na maoni yaliyotolewa kwa ujumla na niishukuru Kamati ya *PAC* na Kamati ya *PIC* zote kwenye eneo linalohusu Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, la kwanza nataka kuchangia maoni ya Kamati ya *PAC* hasa kuhusu *issue* ya vihenge. Ni kweli kwamba Serikali imekuwa na mkataba na kampuni mbili; Kampuni ya *FERRUM* na Kampuni ya *UNEA*,

mkataba wenye jumla ya thamani ya Dola milioni 55. Kampuni ya *UNEA* ilipewa *site* tatu ambazo zimeshakamilika kwa asilimia 100 na tumeanza kuzitumia. Changamoto iko kwenye mradi unaofanywa na kampuni ya *FERRUM***,** lakini nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imechukua hatua, kwamba Kampuni ya *FERRUM* ilileta *intention* ya kutaka kuongezewa fedha zaidi ya Dola milioni 18 *over and above the contractual agreement.* Serikali ilikataa kutekeleza maombi hayo na mpaka sasa Serikali imeshikilia *retention* ya Dola milioni tatu.

Mheshimiwa Spika, tunafanya nao mazungumzo, kama hawataweza kutekeleza kutokana na *scope* iliyopo, tutavunja nao mkataba na tutatafuta mkandarasi mwingine kwa ajili ya kuweza kuendelea na mradi huo. Kwa hiyo, tunalichukulia *in a serious note* na ninaamini kwamba pamoja na maazimio yatakayofikiwa, tukija *next time* tutakuta jambo hili limeshaondoka kwenye meza yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili lilikuwa ni suala la pamba, ni kweli mwaka 2019 Serikali ilitoa maelekezo kwamba pamba inunuliwe kwa bei ya Shilingi 1,200/= na kulikuwa na *clear instruction* na *mechanism*. Serikali ilishalipa hasara ya Shiligi bilioni 14, na mimi mwenyewe Kamati ya Bunge iliniita tukiwa na Waziri wa Fedha, tukakutana na kuongea na Kamati ya *PIC* na kuwaeleza hatua ambazo tunachukua. Kama Serikali hatua ambayo tutachukua kuliondoa hili jambo la mwaka 2019 ni kwamba tutahakikisha tutakapokwenda kwenye mwaka ujao wa fedha hili eneo tunali-*resolve once and for good*.

Mheshimiwa Spika, nataka niliombe Bunge lako Tukufu, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge, suala la mauzo na manunuzi ya bidhaa sokoni, tukaheshimu soko. Mwaka 2018, 2019 tulichukua hatua ambazo zilitupeleka kwenye hasara kubwa na kutuumiza kama nchi, na leo Kamati ya Bunge na *CAG* wameweza kuleta mapendekezo haya yaliyotokana na *influence* iliyotoka ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nashauri huko tunakokwenda turuhusu kuchukua hatua ambazo *not more political* kwenye masuala ya kibiashara.

*(Hpa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri sekunde thelathini.

**WAIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, sawa. La mwisho, Waheshimiwa Wabunge wame-*comment* sana kuhusu suala la kupeleka mbolea za ruzuku. Ni kweli Mheshimiwa Rais amezindua, na mimi nilishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuweka *effort* kwenye eneo la kilimo na kuongeza bajeti na Serikali imeanza kutoa ruzuku. Tumetengeneza mfumo ambao una muda wa siku 60 tu.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto, lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana pamoja ili kuhakikisha kwamba tunapeleka huduma hii, wakati huo huo tukimlinda mkulima, na wakati huo huo tusiruhusu kwenda kupeleka ili mfumo huu uende kuwafaidisha watu wachache badala ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, halafu watoa hoja wote watatu wajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wote wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, kwanza kukupongeza sana kwa mwenendo na uongozi mzuri wa Bunge. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nami nichukue nafasi hii kama Mbunge ambaye nimekuwepo hapa Bungeni muda mrefu, kuwapongeza sana Wabunge. Nadhani nichomekee kidogo, kwamba Wabunge na Bunge hili asilimia kubwa ni wa Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza wajibu wao vizuri wa kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, kwa kweli nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba sisi ambao tuko kwenye *front bench* hapa, ni mawaziri ambao pia tunatokana na Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, tunawaahidi hatutawaangusha, tutayachukua yote tuyafanyie kazi na mwisho wa siku tunachotaka kwa kweli ni utendaji mzuri wa kazi za Serikali. Pia tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuliendeleza Taifa letu na juhudi hizo tunaziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakwenda moja kwa moja kwenye maeneo kadhaa yaliyojitokeza kwenye hoja ya *CAG* na vilevile yamechangiwa na Wabunge. La kwanza ni malimbikizo ya muda mrefu ya haki na stahiki za watumishi wa Umma. Malimbikizo haya yamejigawa

katika maeneo tofauti, nami nitazungumzia eneo ambalo liko ndani ya Ofisi ya Rais. Naomba Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu alipoingia tu ndani ya madaraka kwenye Serikali hii ya Awamu ya Sita, kwenye eneo la malimbikizo ameshalipa malimbikizo ya mishahara *(arrears)* kwa watumishi 113,969 na tayari Shilingi bilioni 196,083 zimetumika. Kwa hiyo, kwa kweli eneo hilo amelifanyia kazi kwa kuzingatia ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye ripoti ya *CAG* kulikuwa na hoja ya madaraja ya Watumishi. Naomba nikuhakikishie, ndani ya muda mfupi Mheshimiwa Rais na Serikali yake kupitia ofisi hii tayari watumishi 262,008 wameshabadilishiwa muundo wa madaraja; na Serikali kwa sasa kila mwezi inatumia fedha za Kitanzania Shilingi bilioni 58,253 kila mwezi kwa ajili ya madaraja hayo mapya. Kwa hiyo, Mheshimwa Rais jambo hili amelizingatia.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa sana hapa ndani kwenye hoja ya *CAG* kwamba kuna tatizo la watumishi katika sekta mbalimbali. Unakumbuka tulishatoa taarifa hapa Bungeni kwamba Mheshimiwa Rais aliridhia kibali cha ajira 44,099 na kimeshatolewa na ajira zinaendelea kutolewa katika sekta mbalimbali. Pia tumeendelea kuagiza wale tuliowakasimia madaraka ya usimamizi wa rasilimali watu katika Serikali za Mitaa na hasa *Regional Secretariat*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kifupi Mheshimiwa Rais aliridhia kufanya *recategorization* kwa watumishi zaidi ya 25,000. Tumesema kwamba, tuna tatizo kweli la Watumishi ila haingii akilini kwenye *Regional*

*Secretariat* tumewapa mamlaka ya kusimamia namna ya upangajia rasilimali watu katika maeneo yao; tuna eneo hili la *recategorization* ambalo Maafisa Rasilimali Watu wanaweza kulitumia vizuri sana; kwa mfano, kama unaona katika eneo lako labda una walimu wengi wa somo fulani waliozidi kwenye ikama, lakini una upungufu wa wataalamu katika eneo lingine, unao uwezo wa kuwachukua wale walimu na kuwasomesha wakaziba pengo la eneo ambalo halina watumishi wa kutosha. Kinachotakiwa kufanyika ni kuomba tu kibali cha *recategorization*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme, tunaendelea ku-*control wage bill.* Hii *wage bill* tunakwenda nayo kwa kuangalia kile kilichopo katika mfuko wetu wa Serikali. Tukisema tuajiri kujaza mapengo yote, hatutaweza. Kwa hiyo, ni suala tu la kujiongeza tu kwa wale tuliowapa kazi ya kusimamia na kupanga rasilimali watu nchini. Pia tuna mfumo ambao sasa hivi unafanya *Staff Auditing.*

Mheshimiwa Spika, kwenye ule mfumo ukienda kuangalia unapata taswira ya aina ya watumishi jinsi walivyopangwa kila mkoa. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri wa Afya amekuja kuomba kibali, pale walipozidi tuwahamishe wapelekwe mahali ambapo hawapo. Kwa hiyo, kama tukishirikiana kwa pamoja na hasa kwenye *Regional Secretariat,* ninaamini kabisa kwa rasilimali watu ndogo tunaweza kufanya mambo makubwa. Kwa hiyo, ni wito wangu kwa kweli tufanye kazi hiyo kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la mifumo. Waheshimiwa Wabunge na ripoti ya *CAG* ilisema hapa, bado kulikuwa na mianya ambayo iliruhusu kuendelea na watumishi ambao wamefariki lakini bado wanaonekana

kwenye taarifa za watumishi ambazo tunazo. Kipindi hicho cha Ukaguzi wa *CAG* tulikuwa na mfumo wa *LAWSON,* lakini kuanzia mwaka 2021 mfumo wa LAWSON tumeachana nao. Sasa hivi tuna mfumo mpya wa taarifa za Watumishi na mishahara.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie kwamba mfumo huu una uwezo wa kukagua taarifa za watumishi wote wa nchi nzima kila mwezi. Kila mwezi tuna uwezo wa ku-*audit* watumishi wote waliofariki, waliostaafu na ambao hawana sifa na kuwaondoa kupitia huo mfumo. Kwa hiyo, tunaamini huko tunakokwenda, kwa kuwa *LAWSON* sasa tumeiondoa na tuna mfumo mwingine mpya tunaoutumia, haya yaliyojitokeza wakati wa ripoti ya *CAG* tunaamini kabisa yatapungua kwa kiasi kikubwa na ikiwezekana yataisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia tumegundua na hapa imejadiliwa sana, kuna tatizo la uwajibikaji kwa watumishi wetu na hasa hii mianya ambayo imekuwa ikitumika ya rushwa na ubadhirifu wa fedha. Ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, tumeshakamilisha ujenzi wa mifumo miwili mipya. Mfumo ambao utachukua nafasi ya *OPRAS* ili kupima utendaji kazi wa mtumishi mmoja mmoja kila siku; kwa siku, kwa wiki mpaka kwa mwaka. Vilevile tumetengeneza mfumo mwingine ambao utapima utendaji kazi wa taasisi zote za Umma. Mfumo huu mpya wa kupima utendaji kazi wa taasisi za Umma, unatupelekea sasa kufuatilia zile *key performance indicators* zote katika kila taasisi, je, hao wanaopewa majukumu ya kusimamia utendaji kazi wa taasisi, wanazifikia?

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge alisema hapa kuhusu suala la kufanya *naming and ashaming;* kupitia mfumo huu, kila mwisho wa mwaka taasisi zitakazofanya vibaya zitaangukia kwenye utaratibu wetu wa *naming and ashaming* kwa wale ambao hawatafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, baada ya muda mfupi tutakuja na mageuzi makubwa ya kimifumo na kiutendaji itakayomlazimisha kila mtumishi kuwajibika kwa hiari yake mwenyewe, kuondoa upendeleo na kutoa haki na stahiki kwa kila mtumishi kwa kuzingatia kazi anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU tumewapa kazi ya kujikita…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, sekunde 30.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, tunakuja na mpango wa kitaifa wa kupambana na rushwa. TAKUKURU tumewapa kazi kubwa ya kuzuia, tunataka wazuie. mabilioni ya fedha yote kama tungeweza kuzuia ubadhirifu usitokee, nadhani tungekuwa tumefanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, mtazamo wetu sasa hivi ni kuzuia mianya yote ya ubadhirifu na rushwa ili angalau kila kidogo

kinachopatikana katika Serikali yetu kifanyiwe kazi vizuri na kiweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, tunayo mengi, lakini nadhani tutaendelea kutafuta muda wa kuyatolea maelezo na ufafanuzi hapa ndani ya Bunge lako Tukufu. Tunaunga mkono hoja hizi na sisi ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tutashirikiana kuhakikisha maazimio yanafanyiwa kazi na mwisho wa siku ni maendeleo na ustawi wa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita Wenyeviti wetu kuja kihitisha hoja na kuleta maazimio ya Bunge, nitoe maelezo ya jumla. Mtakumbuka kwamba kuanzia tarehe 2 Novemba, 2022, tumekuwa na mjadala wa hoja wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwa hesabu zilizokaguliwa na *CAG* na Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu uwekezaji wa mitaji ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

Waheshimiwa Wabunge, hatua inayofuata sasa ni kwa Wenyeviti wa *PAC, LAAC* na *PIC* kuhitimisha hoja zao kwa kujibu na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yaliyoibuliwa na Wabunge wakati wa mjadala. Aidha, Wenyeviti hao watapata fursa ya kusoma mapendekezo ya maazimio yanayojumuisha mapendekezo ya Kamati na yale yaliyoibuliwa na Wabunge wakati wa mjadala. Baada ya hapo, watatoa hoja ya kuliomba Bunge lipokee na kuridhia maazimio hayo yawe uamuzi wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba maazimio yanayotolewa na Kamati hizo ni sehemu tu ya maoni na mapendekezo yaliyoainishwa kwenye taarifa za *CAG,* hivyo tutakapofikia hatua ya kulihoji Bunge, kimsingi tutakuwa tunalitaka Bunge likubali kupitisha maazimio yale yaliyosomwa na Wenyeviti wa Kamati hizo pamoja na mapendekezo yote yaliyomo kwenye taarifa ya *CAG* ili yachukiliwe kama maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Nadhani hapo tumeelewana vizuri. Kwa upande wa Serikali watakapokuwa wanayachukua maazimio ya Bunge, wanachukua haya ya mfano yatakayosomwa hapa na Wenyeviti pamoja na taarifa ya *CAG* na yote yaliyoandikwa kule yanakuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya Bunge kupitisha maazimio hayo, yataelekezwa Serikalini kwa ajili ya utekelezaji. Ingawa Sheria ya Ukaguzi wa Umma haiweki muda wa Serikali kuwasilisha taarifa ya utekelezaji, Bunge linaiagiza Serikali kuwasilisha kwa *CAG* taarifa ya hatua watakazokuwa wamefikia kwa utekelezaji wa maazimio hayo ifikapo Februari, 2023. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika maazimio yale, yapo mambo ambayo ni ya siku nyingi sana, tunatamani yafike mwisho. Yale ambayo ni mapya na kwa Bunge litakavyokuwa limeelekeza yanahitaji utekelezaji wa muda mrefu, tutasikia hiyo Februari, ni yapi ambayo yamefanyiwa kazi, yale ambayo ni ya muda mfupi na yameanza siku nyingi; na yale ambayo utelelezaji wake

utakuwa unaendelea, tutapata taarifa Februari, 2023. Halafu kadri tunavyoenda huko mbele, *inshallah* Mwenyezi Mungu atuweke, tutakuwa tunayatazama. Maana pia haipendezi Wabunge kuwa wanazungumza jambo moja mara mbili, mara tatu, halafu wanaita watu hao hao, wanazungumzia hoja hiyo hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, aidha, baada ya *CAG* kufanya uhakiki wa utekelezaji wa maazimio hayo, atawasilisha taarifa hiyo Bungeni kupitia kwa Kamati za Bunge zinazohusika. Wakati wa Bunge la Bajeti Waheshimiwa Wabunge, maana hii itakuwa karibu na Bunge la Bajeti; wakati wa Kamati huko mtakuwa mengine mnayatazama kadri Serikali itakavyokuwa inawasilisha taarifa zake za Bajeti huko. Hivyo kila wizara ya kisekta itasema ya kwake. Siyo kwa maana ya utaratibu wa kawaida, lakini ndiyo ufuatiliaji wenyewe, kwa sababu watakuwa wameshasema Februari, kwa hiyo, wakati wanaleta zile taarifa zao za utekelezaji wa taarifa ya 2021/2022 mtakuwa mnatazama hiyo ya 2023/2024, mpango ukoje wa kuteleza Maazimio ya Bunge?

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ya utangulizi, sasa nitaanza kuwaita Waheshimiwa Wenyeviti ili waweze kuja kuhitimisha hoja zao na kuyasema kwa ufupi maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*Public Account Committee)* au anakuja Makamu? Ahsante sana kwa niaba yake, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, naomba kuchukua nafasi hii kutoa ufafanuzi wa hoja chache ambazo Waheshimiwa Wabunge wamechangia katika taarifa ambayo tuliwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na kwa moyo wa dhati, naomba kukushukuru wewe mwenyewe kwa kutoa muda wa kutosha kwa upande wa Bunge kuweza kuchambua taarifa ya *CAG* kwa undani. Pili, naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita Mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyoendelea kutafuta fedha na rasilimali mbalimbali ili ziweze kusaidia katika kuleta maendeleo ya nchi yetu, nampongeza sana. Tatu, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa namna mbalimbali wamechangia katika hoja hii ambayo tumeiwasilisha. Wabunge takribani 82 wamechangia, michango yao imesaidia sana kuboresha maazimio ambayo kwa kweli tutayaleta hapa Bungeni sasa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa namna mbalimbali walivyochangia hizi hoja na fafanuzi mbalimbali ambazo wamezitoa. Kwa kweli tunawapongeza sana, wametoa ufafanuzi, wamenirahisishia ili niende moja kwa moja katika kusoma maazimio.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuisimamia Serikali ni jukumu la kikatiba, kwa mujibu wa Katiba yetu ukisoma ibara ya 63(2) ndio inayoelekeza Bunge hili kama

chombo mahususi cha kuisimamia Serikali. Sambamba na hilo tunazo sheria, lakini tunazo kanuni zinazotuongoza katika kutekeleza majukumu yetu. Kamati yetu ya Hesabu za Serikali inazungumzwa pia katika Kanuni za Bunge ambapo katika Nyongeza ya Nane imeeleza mambo tunayotakiwa kuzingatia katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hili ili Waheshimiwa Mawaziri watuelewe. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge mambo tunayoyaleta ndani ya Bunge ni maeneo ambayo yana matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwa hiyo, yapo mambo mazuri ambayo yamefanywa kwa mujibu wa kanuni hatuyaleti hapa. Tunaelewa mambo mengi yanaendelea, lakini tunaleta yale yenye viasharia vya matumizi mabaya, hayo ndiyo tunayaleta humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotuongoza katika kutekeleza majukumu yetu, tunaangalia Sheria za Fedha. Sheria ya Fedha ya mwaka ya mwaka 2001, marekebisho ya mwaka 2004 mpaka marekebisho ya mwaka 2020, inatuongoza kwa namna ambavyo fedha za umma na mali zinavyotakiwa kusimamiwa katika kila eneo na huo ndio msingi wa kuchambua hoja zetu humu ndani. Pia kanuni inatuelekeza, sisi Kamati ya *PAC* tunajadili mambo ambayo yamebainishwa katika ripoti ya *CAG*. Kwa hiyo, kama hayajabainishwa hatuwezi kuyajadili humu ndani, hivyo, tunayajadili haya, zipo Sheria za Manunuzi na sheria nyingine ambazo tunaendelea kuzizungumzia.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwa kifupi sana, wengi wamechangia utekelezaji wa maagizo ya Kamati, maazimio ya Bunge na hoja za *CAG*. Katika maeneo mengi bado utekelezaji wake ni hafifu na wajumbe

wamechangia, nawapongeza sana wameliona kabisa na ndio uhalisia uliopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo yenye udhaifu katika usimamizi wa fedha za umma. Sheria zipo, taratibu zipo, miongozo ipo, lakini watu wanakiuka kwa malengo yao na kwa nia zao. Nadhani hili halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, kwa uamuzi uliouchukua kwamba sasa Bunge liisimamie Serikali, hapa maazimio, nataka niwahahkikishie Waheshimiwa Wabunge, nilisoma maazimio hapa, lakini sasa yanayokuja yatawezesha Bunge kuwa ni chombo kinachosimamia Serikali. Maazimio haya yamezingatia yale waliyoyasema ili Bunge kiwe chombo mahususi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo, yapo maeneo ya mifumo na Serikali kila siku hapa wanasema wanaenda kutengeneza mfumo mwingine. Nataka niliambie Bunge hili kuwa, eneo la mifumo ya TEHAMA linatumia fedha nyingi sana za umma na mifumo hiyo mingine wanatumia fedha nyingi halafu wanaiacha, wanakwenda tena kwenye mfumo mwingine. Ni eneo ambalo lazima litazamwe kwa mapana na marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni eneo la manunuzi. Eneo la manunuzi ya vifaa na mali linatumia fedha nyingi na ni eneo ambalo ubadhirifu mwingi umekuwa ukitokea. Kwa hiyo hili eneo lazima liimarishwe. Kuna eneo la usimamizi wa mikataba, lakini yapo maeneo ya usimamizi wa ndani. Nataka niwaambie, bila kuwa na mfumo thabiti au mfumo madhubuti wa usimamizi wa ndani *(internal controls),* hizi hela zitaendelea kupigwa. Tuiombe

Serikali waimarishe hiyo mifumo, itasaidia kupunguza ubadhirifu, rushwa na itasaidia kuhakikisha uzembe unapungua.

**SPIKA:** Mwenyekliti tuongoze vizuri hapo, umesema uiombe Serikali, ndio umeshaanza maazimio au ni jambo lingine? Maana sasa Wabunge tutakuwa hatuelewi hapa wakati tutakapokuwa tunahojiwa, kwenye hilo unalolisema azimio la Bunge ni nini? Yaani kama bado uko kwenye maelezo ya awali, sawa. Tuongoze vizuri, maana hatutaki kufika mahali tukawa hatujui Bunge linaamua nini?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, bado sijaanza maazimio. Kwa hiyo ni uchangiaji tu.

**SPIKA:** Kwa hiyo sasa unaleta maombi kwa Serikali?

**MHE. JAPHET N HASUNGA, MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

Mheshimiwa Spika, labda katika maeneo machache nataka nitoe ufafanuzi kwa dakika chache. Kuna baadhi ya Waheshimiwa akiwemo Mheshimiwa Mpina alizungumzia suala la Deni la Taifa ambalo halikuonekana kwenye taarifa hiyo. Nataka niliambie Bunge lako kwamba, Kamati ilichambua Deni la Taifa, tuliangalia vigezo vyote na tuliangalie taarifa iliyopo, hakukubainika dosari zozote katika hilo, ndio maana kwenye ripoti hatujalileta. Vinavyokuja humu ni vile ambavyo vinaonekana ni madhaifu ya muda mrefu na ambayo

yanaendelea kujirudia. Tulipoona hakuna hoja hatujaleta na ndio maana taasisi nyingi hatukuleta humu kwa sababu hatukubaini mapungufu kwenye hayo maeneo.

Mheshimiwa Spika, lipo eneo la *KADCO,* eneo hili nashukuru jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamelichambua na michango ya wajumbe imekuwa mizuri sana. Suala la Kamati lilikuwa kwamba kama wawekezaji, waliwekeza shilingi ngapi? Hapa ndiyo tulitaka Serikali watuambie, hawa wawekezaji waliokuja wakati huo wakaunda hiyo *KADCO* waliwekeza shilingi ngapi? Mpaka wakalipwa hiyo millioni 5.3, walilipwa kwa uwekezaji upi? Hilo ni suala la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, tunataka kujua baada ya Serikali kuchukua mwaka 2010 mpaka leo *KADCO* imetekeleza mambo gani na fedha hizo za umma zimesimamiwaje? Bado hatujapata majibu ya hayo yote. Yapo mambo ya *TPA* na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba niende kwenye uchambuzi na mapendekezo ya maazimio moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mahojiano na Maafisa Masuuli pamoja na majadiliano na michango ya Waheshimiwa Wabunge iliyotolewa kuanzia tulipoanza kujadili tarehe 2-5 Novemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo kwa kiasi kikubwa yatasaidia kuongeza uwajibikaji katika usimamizi

wa fedha za umma kama ambavyo Bunge linatakiwa kusimamia na kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza katika siku hizi nne za mjadala hapa Bungeni. Mapendekezo yanayoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, azimio kuhusu nakisi ya Ukusanyaji wa Mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* kiasi cha Shilingi trilioni 2.81:-

KWA KUWA taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebainisha kiasi cha Shilingi trilioni 2.81 cha mapato ambayo hayakukusanywa na Mamlaka ya Mapato *(TRA)* kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na mapungufu mbalimbali;

KWA HIYO BASI Bunge liazimie kwamba:-

(a) Serikali ifanye mapitio ya kina ya mfumo mzima wa ukusanyaji kodi (*comprehensive tax regime review)* ili kuhakikisha kodi zote zinakusanywa kama ambavyo Bunge linaidhinisha na kwa mujibu wa taratibu zetu.

(b) Serikali ifanye uchunguzi na kufanya hatua stahiki kwa watumishi wote wa Mamlaka ya Mapato Tanzania waliohusika kwa kukadiria kodi chini ya kiwango, kutoshughulikia madeni ya kodi kwa wakati, kuchelewa kusajili mapingamizi ya kodi kwa wakati, kutosimamia ushuru wa forodha kwenye bidhaa za mafuta na magari pamoja na usimamizi usioridhisha wa matumizi ya mashine za kielektroniki; hali iliyosababisha ongezeko la madeni ya kodi kwa zaidi ya 95% ndani ya

mwaka huo wa fedha hivyo kuikosesha Serikali mapato ya kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, mbili, azimio kuhusu dosari katika usimamizi wa mikataba na athari zake katika matumizi ya fedha za umma:-

KWA KUWA Kamati imebainisha upungufu katika uingiaji na usimamizi wa mikataba katika taasisi mbalimbali za Serikali hali iliyosababisha hasara kwa Serikali ikiwemo shilingi bilioni 68.7 kwa *TANROAD, TANESCO* dolla za Kimarekani milioni 153.43 na *NFRA* dola za Kimarekani milioni 33.4 na *TPA* bilioni 137.38;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ifanye uchunguzi kubaini iwapo riba zilizotokana na mikataba ya ujenzi wa barabara katika T*ANROAD* zilikuwa na uhalali na ulazima wa kuwepo? Hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi huo. *(Makofi)*

(b) Serikali ichukue hatua stahiki kwa watumishi wa Wizara ya Nishati, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango na *TANESCO* walioshiriki katika mchakato mzima wa uingiaji, usimamizi, utekelezaji na uvunjaji wa mikataba kati ya *TANESCO* na *Symbion*. *(Makofi)*

(c) Serikali ichukue hatua stahiki za kisheria kwa mkandarasi aliyechelewesha kukamilisha ujenzi wa ghati ya kuegesha meli katika Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, tatu, azimio kuhusu hali ya ukwasi kuhusu taasisi za kimkakati za Serikali *(TPDC, TANESCO na STAMICO):-*

KWA KUWA Taarifa ya *CAG* imebainisha changamoto za mtaji katika Mashirika ya Umma ya kimkakati kama *TPDC, TANESCO na STAMICO;*

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina iongeze mtaji katika mashirika ya kimkakati ya Serikali kwa kufanya marekebisho ya msingi katika madeni ya taasisi hizo ili kuyageuza kuwa mtaji *(equity)*. Pamoja na hatua hiyo, Serikali ihakikishe kuwa mikataba inayoingiwa na *TANESCO, TPDC* na *STAMICO* inakuwa na maslahi makubwa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nne, azimio kuhusu Ukaguzi maalum wa *REA,*Uhamiaji na Hombolo:

KWA KUWA Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zimebainisha mambo muhimu katika kaguzi nne zilizopitiwa na kuchambuliwa na Kamati ambazo zimebainisha upungufu katika usimamizi wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa Mkandarasi wa kampuni ya *Derm Electric* Tanzania *Limited* kwa udanganyifu na ubadhirifu pamoja na hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wa *REA* na *TANESCO* waliohusika kusimamia Mradi wa *REA,*

awamu ya pili, Mkoa wa Mara, kwa kutotimiza majukumu yao ipasavyo.

(b) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi 32 wa Idara ya Uhamiaji waliotajwa kuhusika katika mauzo ya *sticker* za *Visa* bandia katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro kwa kuzingatia uhusika wa kila mmoja na matokeo ya ukaguzi maalum.

(c) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi wawili waliojihusisha na ubadhirifu wa fedha za ada ya wanafunzi katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

Mheshimiwa Spika, kwenye ile (b), Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo kwamba wameifanyia kazi, lakini sisi Kamati hadi tunachambua, juzi wakati wanakuja kwenye Kamati ni watumishi 11 tu ambao walikuwa wamepelekwa Mahakamani na hao 11 nao wote wamesharejeshwa. Kwa hiyo Waziri kusema kwamba hatua zilishachukuliwa, sisi kama Kamati mpaka juzi ilikuwa bado hatua hazijachukuliwa. Labda Waziri kama atatuambia kwamba hatua zimechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, azimio kuhusu kutozingatiwa kwa Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348:

KWA KUWA kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Kamati imebaini ukiukwaji wa Sheria za Fedha za Umma, Sura 348 hivyo kuchangia upotevu wa fedha za Serikali;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia yafuatayo:-

(a) Shirika la Masoko Kariakoo, Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, afanye ukaguzi wa kiuchunguzi yaani *(forensic audit)* ili kubaini iwapo kuna ubadhirifu wa fedha za umma uliofanywa na kufichwa baada ya soko hilo kuungua moto. Aidha, vyombo vya dola vianze uchunguzi kwa uliokuwa uongozi wa Soko la Kariakoo ili kubaini iwapo wahusika wana jinai katika kuficha nyaraka za fedha kwa Wakaguzi.

(b) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka *(DART)*. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, aombwe kufanya ukaguzi maalum *(special audit)* wa malipo ya fidia ya kiasi cha bilioni moja na malipo ya fedha za usumbufu kiasi cha Shilingi milioni 434 yaliyofanyika *DART* ili kubaini iwapo yalifanyika kwa mujibu wa sheria.

(c) Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi, Fungu 28. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum *(special audit)* wa matumizi yote ya Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi tangu ulipoanzishwa na kisha kutoa taarifa yake kwa Bunge mapema iwezekanavyo. Aidha, Mlipaji Mkuu wa Serikali aandae kanuni za kusimamia uendeshaji wa Mfuko huo na malipo yote kutoka kwenye Mfuko yafanyike kwa kuzingatia kanuni zilizoandaliwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sita, azimio kuhusu umiliki na uendeshaji wa Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro *(KADCO)*:

KWA KUWA mkataba wa uendeshaji wa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro kati ya Serikali na Kampuni ya *KADCO (concession agreement)* unakosa misingi ya kisheria tangu mwaka 2010, wakati ambapo Serikali ilinunua hisa kwa asilimia 100 za *KADCO* baada ya malipo ya fedha za umma dola za Marekani milioni 5.3;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Serikali irejeshe shughuli zote za uendeshaji wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro *(KIA)* kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kama ambavyo inafanyika kwa viwanja vingine vya ndege hapa nchini kwa kuzingatia majukumu ya kisheria ya *TAA* na uamuzi wa Serikali uliokuwa umetolewa hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina *(comprehensive audit)* wa mapato na matumizi ya *KADCO* kuanzia mwaka 2010 baada ya kuanza kumilikiwa kwa 100% na Serikali hadi sasa na Bunge lijulishwe ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, saba, azimio kuhusu utendaji wa kifedha wa benki za Serikali *TCB* na *TIB:*

KWA KUWA Taarifa ya *CAG* imebainisha kutokuwepo kwa mtaji wa kutosha wa benki ya Serikali za *TIB* na *TCB,* hivyo kukwamisha shughuli za benki husika na kuhatarisha fedha za umma zilizowekwa kwenye benki hizo;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba *TCB* na *TIB* zikusanywe mikopo yote ikiwa ni pamoja na kutaifisha mali za dhamana zilizowekwa na wakopaji husika kwa mujibu wa sheria ili kurejesha mtaji wa benki inayohusika.

Aidha, vyombo vya dola vifanye uchunguzi wa mikopo yote chechefu iliyotolewa na *TIB* na *TCB* ili kubaini iwapo ilitolewa kwa kuzingatia taratibu za kibenki na kuchukua hatua dhidi ya watu waliohusika.

(viii) Kuhusu ubadhirifu katika upanuzi wa Bandari ya Tanga.

KWA KUWA, Kamati ilifahamishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Tarehe 14 Juni, 2021 aliomba kufanyika kwa ukaguzi wa kiuchunguzi na kuainisha tuhuma za ubadhirifu wa fedha na matumizi mabaya ya madaraka uliofanywa na Watumishi wa *TPA* katika utoaji wa tuzo ya zabuni ya uboreshaji wa Bandari ya Tanga kwa Kampuni ya *China Harbor Engineering Company Limited (Check)*. Ukaguzi huo umekamilika na kubaini ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma takribani Bilioni 65.3 ambayo ni hasara kwa Serikali; Na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 81(a) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2009, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU alipewa matokeo ya ukaguzi huo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ichukue hatua za kisheria kwa makampuni na Watumishi wote wa *TPA* waliotajwa katika taarifa ya ukaguzi maalum kwa kuhusika kwao katika ubadhirifu wa fedha za umma wakati wa utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa Bandari ya Tanga. *(Makofi)*

(ix) Kuharibika kwa dawa na kutokuwepo kwa dawa katika baadhi ya maeneo ya kutoa Huduma za Afya.

KWA KUWA, taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Bohari ya Dawa *(MSD)*, umebaini uwepo wa dawa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 23.04 zilizokwisha muda wake zinatakiwa kuharibiwa. Pamoja na hilo ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa dawa katika baadhi ya maeneo ya kutolea huduma za afya wakati ambapo kuna dawa zina maliza muda wake wa matumizi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Bohari ya Dawa wasitoe dawa, vitendanishi au chanjo ambazo muda wake wa matumizi upo chini ya Miezi Sita ya kutumika yaani *Shelf Life.* Aidha, Serikali isipokee dawa, vitendanishi au chanjo za msaada ambazo pia muda wake wa matumizi upo chini ya Miezi Sita na kupelekwa *MSD*. Aidha *MSD* ipeleke dawa kwa wakati kwa wanao hitaji kwa maeneo yote ambayo wanakuwa wamepokea fedha zao. *(Makofi)*

(x) Mapitio na tathmini ya hesabu za Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

KWA KUWA, uchambuzi wa taarifa ya *CAG* umebainisha kupungua kwa uwezo wa mifuko ya *PSSSF* kulipa mafao yake, pamoja na uwepo wa deni ambapo mifuko ya *PSSSF* na *NSSF* inadai kwa Serikali takribani Trilioni 1.5;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali iwasilishe Bungeni mpango wa malipo ya mikopo ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(Loan Repayment Schedule)* kwa madeni yote ambayo mifuko inaidai Serikali. Mpango huo wa malipo uwasilishwe Bungeni kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2022/2023. *(Makofi)*

(xi) Kuhusu mapungufu katika uzingatiaji wa Sheria za Manunuzi ya Umma na Kanuni zake.

KWA KUWA, taarifa za CAG zimebainisha kuwa baadhi ya Taasisi za Umma zimekiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma *(PPRA)* ifanye ukaguzi wa kiuchunguzi katika manunuzi yenye dosari yaliyobainishwa na Kamati katika taasisi za *TANESCO*, Fungu Na. 57 Wizara ya Ulinzi, na kisha kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi. Aidha, TAKUKURU ianzishe uchunguzi wa wahusika waliofanya manunuzi bila kuzingatia sheria katika taasisi hizo na kuchukua hatua stahiki.

(xii) Kuhusu mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani.

KWA KUWA, taarifa ya *CAG* katika Mafungu mbalimbali zimebainisha mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani, hivyo kupelekea upotevu wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia;

(a) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa watendaji na kampuni zilizohusika na ununuzi na usimikaji wa mifumo ambayo imeshindwa kufanya kazi kwa ufanisi katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*. Aidha, Kampuni hizo zifungiwe na Mamlaka ya Usimamizi wa

Manunuzi Serikalini *(PPRA)* kujihusisha na shughuli za usimikaji wa mifumo hapa nchini.

(b) Bodi ya SUMA JKT, ichukue hatua za kinidhamu na kisheria kwa Watendaji waliokuwa wakisimamia mradi wa mauzo ya matrekta kwa kuruhusu uuzaji wa matrekta bila mikataba ya mauzo.

(xiii) Kuhusu taarifa ya ukaguzi wa ufanisi.

KWA KUWA, taarifa Nne za ukaguzi wa ufanisi zimebainisha masuala kadhaa katika taasisi za Serikali yanayohusu dosari katika usimamizi wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina *(Comprehensive Audit)* katika mchakato mzima wa ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Aidha katika kipindi cha kila Miezi Mitatu Serikali ihakikishe inawasilisha Bungeni taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi yaliyotolewa na *CAG* kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Tume ya Madini, *TANROADS* na *BRELA*.

(xiv) Usimamizi usioridhisha wa taarifa na huduma katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

KWA KUWA, taarifa ya *CAG* imebainisha dosari katika usimamizi na udhibiti wa taarifa muhimu za wanufaika wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na gharama za matibabu ambapo pamoja na mambo mengine ilibaini utolewaji wa huduma za uzazi kwa upasuaji wa wanaume 731. Aidha ukaguzi ulibaini kuwa *NHIF* kukataa kulipa malipo ya Shilingi Bilioni 3.18

kwa hospitali za Serikali zilizotoa huduma kutokana na kuwa na mfumo wenye mapungufu, utambuzi na usimamizi wa taarifa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye uchunguzi wa Idara ya Usimamizi na Udhibiti wa Huduma katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kubaini iwapo inatekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha uchunguzi ufanyike kubaini watoa huduma ambao wamekuwa wakiuhujumu Mfuko kwa kuongeza gharama za matibabu kwa njia ya udanganyifu na kisha kuchukua hatua stahiki kwa wote watakaobainika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa namna ya pekee kukushukuru wewe kwa namna ulivyosimamia mjadala wa taarifa za Kamati zinazotokana na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao yenye tija na kujenga, ambayo imesaidia sana kuboresha mapendekezo ya maazimio ambayo yamewasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Kwanza kuna Wabunge mmekaa sijawaelewa, hoja yetu hii jamani! Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. *(Makofi/kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, Sasa nataka kuwahoji na kwa sababu kama nilivyotoa maelezo mara kadhaa huko nyuma, tutakapokuwa tumehojiana hapa tunahojiana kuhusu haya na yaliyoko kwenye taarifa ya *CAG* ambayo yanaangukia kwenye Kamati yetu ya Hesabu za Serikali, hilo ni moja. Pia nataka kutoa nafasi kwa sababu haya ni maamuzi ya Bunge na nimesikia Mawaziri wakitoa maelezo fulani hivi ambayo kidogo kwa maazimio yetu yalivyo hapa, kwanza ni Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi maelezo yaliyotoka kuhusu Bandari ya Tanga, nafikiri mmesikia Maazimio Bunge linaazimia nini hapa na ninyi maelezo mliyokuwa mmetoa maana, kwa taarifa Kamati yetu ya Bunge ilizonazo ni kwamba ukaguzi umeshafanyika na umekamilika na umebaini ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma.

Mheshimiwa Waziri, sasa hapa ulionesha kana kwamba ukaguzi ndiyo unaenda kufanyika ukaguzi umeshafanyika ama bado? Hili Azimio ndiyo tunataka kupitisha hapa.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, sisi hatujapata ripoti, tuliambiwa kwamba ukaguzi unaendelea *special audit* inaenda kufanyika, ripoti ya special audit bado hatujaipata.

**SPIKA:** Ninyi bado hamjaipata! Sasa Kamati imeipata ama Mwenyekiti ndivyo ama sivyo, si Kamati mmeipata na ndiyo maana mkasema kuna ubadhirifu *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Sawa. Sasa kwa sababu hiyo nyingine inayochunguza haikatazwi kuendelea kuchunguza ila Bunge leo litafanya maamuzi kuhusu jambo hili, nilitaka tuwe na uhakika tu kuhusu jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, lingine liko kwenye hili azimio Namba Tisa ambalo linazungumzia Bohari ya Dawa, kuhusu muda ule wa dawa hapa azimio linazungumzia Bohari ya Dawa wasitoe dawa, vitendanishi au chanjo ambazo muda wake wa matumizi upo chini ya Miezi Sita ya kutumika (*shelf life)*. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, sawa sasa ama Daktari aliyeko humu ndani, maana tukishaamua hivi ndiyo tutakuwa tumeshaamua.

Daktari, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais …..

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Ndugulile yupo hapa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, nataka Daktari atusaidie kwa sababu tukiweka huu muda humu hatutataka kusikia muda tofauti ambao umeamliwa na Bunge. Kwa hiyo, kwenye eneo hili haya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwenye hili azimio tunasema hivi, Bohari ya Dawa wasitoe dawa, vitendanishi au chanjo ambazo muda wake wa matumizi upo chini ya Miezi Sita ya kutumika *(shelf life)*.

Mheshimiwa Dkt. Ndungulile tuko sawasawa? Kidaktari tukitoa agizo hili kwa *MSD*.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, tuna sera ambayo ipo ndani ya Wizara ya Afya ambayo inazuia uagizaji dawa ambazo una muda mfupi chini ya mwaka mmoja. Lengo la kuweka zuio hilo ni kuhakikisha kwamba dawa zinafika nchini mapema zikiwa bado zina nguvu yake na zinaweza zikasambazwa kwa wakati na kutumika ndani ya muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa azimio hili tuko sahihi kabisa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Haya na hili ambalo tunaendelea hapohapo kwenye *MSD,* aidha Serikali isipokee dawa, vitendanishi au chanjo za msaada ambazo pia muda wake wa matumizi upo chini ya Miezi Sita, hii pia tuko sawasawa kwa sababu kule si mmesema ni mwaka mmoja?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, na hili ni sahihi na bahati nzuri nimeshawahi kuhudumu katika Wizara hii. Moja ya tatizo ambalo limeshakuwa ni kubwa ndani ya nchi yetu ni *dumping*, madawa ambayo yanakaribia kuisha huko nje ya nchi yanaletwa ndani ya nchi, muda wa kuweza kutumika kusambaza unakuwa ni muda mfupi sana, kwa hiyo Serikali inaingia gharama kubwa sana ya kuyateketeza yale madawa. Kwa hiyo hili nalo liko sahihi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Haya, kwenye azimio hilohilo Waheshimiwa Wabunge linamalizia na *MSD* ipeleke dawa kwa wakati baada ya kupokea malipo ya wateja bila kuchelewa. Sasa hii bila kuiwekea muda itakuwa ni kwa wakati, mwezi, miezi miwili, mitatu, sasa hili nalo tunahitaji kidogo maelezo ya Daktari, unasema umeshahudumu

pale ni muda gani tunaweza kuuweka hapa ili Serikali iweze kufanya kazi? *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Mbunge fulani alisimama ili kutoa ufafanuzi)*

**SPIKA:** Nitakupa nafasi. Mheshimiwa Daktari Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, ni vizuri na sisi kama Bunge tukaweka muda maalum, nalisema hili kwa sababu gani? Kuna Vituo vya Afya ambavyo tumevijenga mpaka sasa zaidi ya mwaka mmoja fedha za malipo ya vifaa vile viko *MSD* na vifaa vile havijanunuliwa mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, ni sahihi vilevile kuweka muda wa ukomo ili basi kama *MSD* haina vile vifaa watoe ruhusa kwa sekta binafsi ili waweze kwenda kununua kule *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. sasa *MSD* ikishapokea pesa kutoka kwenye Halmashauri ambazo ziko chini ya TAMISEMI ipeleke dawa ndani ya muda gani? Mwezi mmoja?

**WABUNGE FULANI:** Mwezi mmoja.

**SPIKA:** Ngoja nitarudi kwa Serikali. Haya Mwenyekiti wa Kamati kasimama, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii anayesimamia sekta hii.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Tatizo la *MSD* ni kwamba kimsingi hana mtaji, anachukua fedha kutoka hospitalini ndipo anachakata manunuzi na kurudisha. Tukimwekea mwezi mmoja kwa

*process* hiyo ndefu tunaweza tukawa hatujamtendea haki. Naomba nitoe ushauri..

**SPIKA:** Ngoja, kabla hujaenda huko kwenye mtaji, tunazungumzia Halmashauri ya Maswa imelipa pesa *MSD* kwa ajili ya dawa ambazo imetaja inazihitaji, *MSD* apewe muda gani kuipa dawa Halmashauri ambayo yeye kashapokea pesa zao.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa dawa ambazo anazo, amepewa fedha na dawa anazo, ndani ya mwezi mmoja inatosha.

**SPIKA:** Haya. Sasa huyu ameongeza jambo jipya, kama hana pesa anapokea za nini? Au anapokea pesa ili aagizie nje dawa?

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, hapo ndipo palipo na tatizo. tatizo lilopo ni kwamba fedha *MSD* anazipokea kutoka kwa wahitaji, Wilayani na hospitali yoyote anapokea, anakuwa na *account* ya kutunza fedha hizo kwa muda, sasa huyu anapopokea hizi fedha ndipo anapoanza mchakato wa manunuzi, hilo ndilo linaloleta tatizo kubwa.

**SPIKA:** Mwenyekiti kama ndivyo hizi dawa tunazoteketeza zinatokana na nini? Hizi dawa zinazoteketezwa zinatokana na nini kama unaagiza dawa baada ya mimi kusema ninataka dawa fulani na siyo kwamba ulinunua zikawepo?

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, tatizo linapotokea sasa anakuwa ana mlolongo mrefu wa maagizo ya dawa na nadhani hapo ndipo palipo na tatizo, mpaka zinapokuja kufika kwa ajili ya kuzigawa muda unakuwa umekwenda.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hapa naomba kuazimia…

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mhehimiwa Spika, taarifa….

**SPIKA:** Ngoja kabla ya taarifa. Hapa hili azimio linataka kumwagiza *MSD* baada ya kupokea pesa kutoka kwenye Vituo vya Afya, kutoka kwenye Zahanati, kutoka kwenye Hospitali za Wilaya, dawa zile wale wazipate lini? Maana yake kama ndani ya muda huo hawezi kupeleka hizo dawa awape pesa zao wakanunue dawa huko zinakopatikana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Maana kwenye ngazi hii tukianza kujadili bajeti ya *MSD* ile tutakutana nayo wakati wa Bajeti. Kuna taarifa inataka kutoka hapa, malizia Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja Mheshimiwa Naibu Waziri nitakupa nafasi.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kurahisisha kabisa alichokisema Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, *MSD*

akiwa hana dawa atoe taarifa haraka kwa wahusika ili waweze kupata nafasi ya kwenda kununua dawa kwa *suppliers* binafsi.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ulitaka kutoa taarifa na naona Wabunge wawili mmesimama. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama mlisikiliza wakati tunatoa mrejesho wetu tulisema kwamba sasa tunataka kwamba MSD; kwa sababu hapa ni maisha ni kuokoa maisha ya watu na dawa haina Subira; tunachotegemea na tunapoelekea ni kwamba *MSD* awe na dawa na ndiyo maana tumeweka mikataba ya muda mrefu,ili akienda kama hana dawa hiyo, ndani ya masaa 24 aruhusu wilaya na mikoa wanunue dawa sehemu nyingine inayotakiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani hamjampigia makofi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya ametowa taarifa nzuri sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tanachokisema sasa… *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE**: Mheshimiwa Spika, *no, no, no*, taarifa.

**SPIKA:** Sasa ngoja, mliosimama hamuwezi kuwa mnanipa mimi taarifa ila nadhani mnataka kutoa maelezo ya ziada ili tuboreshe.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE**: Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, suala la dawa ni suala la muhimu sana. Tukisema kwamba kama hawana watoe taarifa, je, taarifa zikichelewa? Iwe ni *tit for tat*, hawana dawa wale wanunue dawa, lakini si tena mpaka hawa watoe taarifa, wanaweza kufanya urasimu wa kuchelewesha kutoa taarifa, tatizo litabaki pale pale. Kwa hiyo kama hakuna wanunue dawa, bila kungojea taarifa yao kwa sababu ni suala la dawa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya limeshaeleweka hilo, Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, mimi nimeshawahi kumiliki *health center* kwa miaka mitatu na tulikuwa tunakwenda kuagiza dawa *MSD*. Kinachotokea katika nchii hii ni kwamba kuna magonjwa maalum yanayojulikana na dawa zake ziko katika *kit*. Kwa hiyo unavyoona *MSD* akisambaza dawa huko katika wilaya ndani ya *kit* kuna dawa maalum kwa magonjwa yaliyoko Tanzania. Habari ya kutueleza kwamba kuna dawa zinaagizwa si kweli. Ndio maana unapokea dawa sasa zinakuwa zime - *expire*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namna tunavyotakiwa kufanya katika Bunge lako ni kutoa maelekezo, kwamba kama hakuna nunua sehemu nyingine. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri sasa tupo kwenye maazimio. Mimi nilichokiona hapa turekebishe tu hilo azimio, kwamba sijui sehemu ya mwisho. Kama *MSD* hawana dawa waweke kwenye tovuti yao. Mkurugenzi anaopoingia pale kwenye tovuti ya *MSD* akiona hii dawa haipo anaenda anaagiza moja kwa moja badala ya kubaki hivyo.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru; na mimi nilitaka nishauri kwamba, malipo yafanyike baada ya *MSD* ku-*confirm* kwamba dawa zote ninazozihitaji zipo zinapatikana ndipo walipwe.

**SPIKA:** Haya ahsante, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Spika, na mimi nasisitiza tu kwamba, daktari au mganga wa kituo cha afya au zahanati anaagiza wale wa vituo vya afya, anaagiza dawa baada ya ku-*confirm* kwamba *MSD* wana dawa hizo. Sasa anapelekaje hela wakati dawa zile haziendi kuagizwa kutoka nje halafu ndiyo zije kutibu mgonjwa. Kwa hiyo, nafikiri masaa 24 wakubaliane na *MSD*. Kwamba, kama nakuletea hela na una dawa unipe, na kama huna uniambie nisikuletee.

**SPIKA**: Haya, ahsante, Mheshimiwa Jerry Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Spika, mimi siko mbali sana na wachangiaji waliotangulia. *MSD* ni shirika la umma, na lazima Bunge hili liazimie mashirika haya yawe *serious*. Unapoongelea dawa unaongelea maisha ya

Watanzania. Lazima shirika hili, na ndiyo haya matatizo Wabunge wengi wamechangia, la mifumo. Huwezi ukawa unashindwa kuwa na mfumo himilivu ambao unafanya wakati wote ujue bohari ina dawa gani ili Kituo hiki cha Afya cha Maswa kabla hakijatuma fedha kijue kinatuma fedha kwa dawa gani na dawa gani hakuna ili wanunue sehemu nyingine wananchi waweze kupata huduma. Kwa hiyo nadhani siku 30 zinatosha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge nadhani tumemsikia. Mheshimiwa Lusengekile.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE**: Mheshimiwa Spika, kuwepo na uboreshwaji wa taarifa kwenye mfumo. Kwa sababu *MSD* unaweza ukaingia kwenye mfumo sasa hivi, wanakuambia dawa zipo na uka-*press* oda na ukalipa, ukienda stoo dawa hazipo. Mimi nimeyaona haya kwa sababu nilikuwa kwenye *field* hiyo. Hata hivyo pia ukishalipa hawarudishi fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, sasa hiyo ndiyo inayotupelekea tuwe na azimio hapa. Sasa tunataka kuweka siku thelathini kwa sababu kuna maeneo ya mbali kidogo, kuwapa muda wa kuzifikisha zile dawa kwenye hayo maeneo. Kwa hiyo, haya yote mliyoyasema ni ya muhimu lakini hatuwezi kuyaweka hapa kwenye azimio. Kwenye azimio hapa tutakachoboresha ni kwamba *MSD* ipeleke dawa ndani ya siku thelathini baada ya kupokea malipo ya wateja. Si ndivyo? Halafu tunaongeza hapo, *MSD* ikiwa haina dawa itoe taarifa ndani ya saa 24. *(Makofi)*

Japo hili suala la mifumo, nadhani haya mengine yatajitengeneza yenyewe, kwa sababu pia haya tunayoyasema kuna wengine huko mifumo kidogo ni

vijijini kwa hiyo inawezekana ni ngumu kidogo wao kuweza kutazama ule mfumo, dawa zipo ama hazipo. Kwa hiyo yeye akaamua kutuma hizo taarifa zake *MSD* na hela kwa sababu zianenda kwa *control number* siku hizi, kwa hiyo, kunaweza kukawa na hiyo changamoto.

Kwa hiyo hili la kutoa taarifa na dawa kutoa ndani ya siku thelathini nadhani tukakuwa tumeweka vizuri upande wa *MSD* ili waweze kufanya kazi yao vizuri. Hilo limekaa vizuri. Na la saa 24 tunaliongeza hapa Mheshimiwa Naibu Waziri kasema ndiyo hiyo.

Kwa hiyo wakipokea fedha hawana dawa, sijui watarejeshaje na *control number* nadhani mifumo inao uwezo huo. Kama benki wakichukua hela zako ghafla ukawaambia mmekosea wanarejesha, na nyie *MSD* mnaweza, si ninyi pekee yenu. Kwa hiyo kama hamna dawa rejesheni fedha zao wakanunue sehemu nyingine. Nadhani…

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nadhani sasa azilimio letu tutakuwa tuumeelewa namna itakavyokuwa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, taarifa, labda naomba ruhusa ya ku - *clarify* jambo.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kuna *sources* mbili ambazo *MSD* inapata fedha kutoka kwenye

vituo. Kuna fedha ambazo zinatoka *direct* kutoka hazina zinakwenda *MSD* ambazo ndizo hizi tunazogawa huku ndani. Pia, kuna *sources* zingine ambazo ni makusanyo ya ndani ya hospitali zetu na halmashauri, kwa hiyo zile fedha zinakuwa kule. Kwa hiyo, sasa kuna hizi ambazo zinakuwa zimepelekwa kule wanatakiwa wanunue dawa na wawe nazo *stock* mapema na wahahakikishe wamepeleka kwa sababu tunajua ni magonjwa gani yapo na ni dawa gani na tuna-*request*

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna hizi fedha sasa ambazo halmashauri imekusanya fedha zake, hospitali ya Wilaya imekusanya fedha zake au ya mkoa. Wanapotaka kuagiza basi kama hawana dawa wawe -*fast* mara moja ndani ya masaa 24 kuwapa taarifa kwamba hatuna ili wakanunue sehemu nyingine, ieleweke namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Sawa, sasa hayo mengine yatakuwa ya utendaji kwa kweli. Sisi tunataka tu hapa anapopokea fedha, amepokea kutoka hazina ama kutoka kwenye kituo, yeye ndani ya siku thelathini apeleke dawa. Sasa hayo mengine yatakuwa ni ya kiutendaji, mtajipanga vizuri. Na kwa taarifa kwa zile dawa atakazokuwa amepokea fedha halafu akajikuta stoo hazipo, kama anavyosema Mhesimiwa Lesengikile, ndani ya saa 24 atoe hiyo taarifa fedha zirejeshwe ili Waziri wa TAMISEMI tusianze kumsumbua hapa kwamba hakuna dawa kule.

Waheshimiwa Wabunge, hilo nalo limeeleweka, sasa nitawahoji…

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, …

**SPIKA:** Ni kuhusu hoja hii ama nyingine kwenye haya maazimio?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, hiyo hiyo.

**SPIKA:** Unapendekeza siku ngapi?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa napendekeza ziwe siku tisini na nina sababu.

*(Hapa, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipaza sauti)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangwalla utakuwa na sababu kubwa sana, lakini kama Naibu Waziri amekubali siku thelathini, nadhani twende na hizo. Kwa sababu siku tisini, hapa tumetoa katazo la pungufu ya miezi sita. Kwa hiyo, tukiongeza tisini ni mwaka mzima sasa huo tayari. Kwa hiyo, tutakuwa sisi wenyewe tena tuongeze pale juu muda, kwa sababu ndani ya siku tisini atakuwa amebaki na miezi mitatu tu ya hizo dawa. Sasa tena si tunaendelea kuziharibu tu huko mtaani. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA**: Mheshimiwa Spika, ndo maana ulisema kama kuna madaktari humu ndani wasaidie kikao na mimi ni daktari. Nina sema hili…

**SPIKA:** Wameshasaidia wawili tayari, Dkt. Mollel na Dkt. Ndugulile, wameshasaidia hawa wawili, kwa hiyo na

wewe ulikuwa uongezeke uwe wa tatu. Nadhani twende na siku thelathini Waheshimiwa Wabunge. Haya ahsante sana. *(Makofi)*

Barabara zinaendelea kutengenezwa, kwa hiyo sidhani kama kutakuwa na eneo nchii hii ambalo litakuwa halifikiki ndani ya siku zote hizi. Baada ya hayo Waheshimiwa Wabunge, sasa maazimio yetu hayo ambayo tumesomewa na Mwenyekiti pamoja na yale ambayo yapo kwenye taarifa za *CAG* yanayoangukia chini ya Kamati hii ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Waheshimiwa Wabunge nitawahoji. Wabunge wanaoafiki sasa…

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA**: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangala utaratibu kwamba nani amekosea kanuni? Mimi? Au nani?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA**: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba muongozo wako kuhusu utaratibu…

**SPIKA:** Hebu kaa, kaa kitako.

Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za ufanisi kwa Mwaka wa Fedha unaoishi tarehe 20 Juni 2021 waseme ndio, wasio afiki waseme siyo, hakuna, Bunge zima limeafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa ili iafikiwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mwenyekiti wa *LAAC*, kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nitumie nafasi hii kwanza kukushukuru sana kwa uamuzi wako uliopelekea Bunge lako kuifanya kazi hii kwa siku takribani nne ambazo hakika Wabunge wameisaidia sana Seriakli kuonesha namna ambavyo usimamizi, changamoto na mapungufu yaliyopo katika utendaji wa halmashauri zetu nchini. Ni mategemeo yetu kwamba mambo mengi yatazingatiwa leo baada tu ya maazimio haya ili yakaweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kabla sijaenda kwenye maazimio ya Bunge lako, yako mambo mawili ambayo nilitamani niyaseme. Moja ni lile la asilimia 10 ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamelizungumza, na wamelizungumza kwa sababu wanaamini kwamba fedha hizi ni nyingi sana; zingeweza kulisaidia sana Taifa kama malengo yake yalivyo.

Mheshimiwa Spika, msingi mmoja ambao umetushangaza sana Kamati, kwa sababu, ipo Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, katika Sura 209 imeeleza wazi, na bahati nzuri sana imeitaja Kamati ya Huduma za Mikopo. Kamati hii kwenye kanuni ya 14 (1) inaundwa na Mkurugenzi mwenyewe wa Halmashauri, Muweka hazina wa halmashauri, Afisa Mipango, Afisa Ushirika, Afisa

Ustawi na Afisa Maendeleo. Maana yake ni nini? Watu wote hao ni Wakuu wa Idara wenye weledi na wenye sifa za kusimamia kazi hii. Kwa hiyo tulitegemea sana kuona kwamba tunapozungumzia mapungufu kwenye eneo la asilimia kumi ambayo tunatarajia iende kwenye jamii na ikalete matokeo chanya haifanyi kazi yake sawa sawa. Tafsiri yake ni kwamba, inawezekana tuna watu ambao hawana uwezo wa kusimamia majukumu waliopewa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo lilitutafakarisha sana ni suala la matumizi ya *POS*. Hizi *POS* zililetwa ili zisaidie, na mfumo huu umeletwa ili uisaidie Serikali katika ukusanyaji wa mapato na uirahisishie, lakini kumekuwa na mchezo ambao unaendelea kwenye matumizi ya *POS*, unakuta *POS* imezimwa kati ya siku 1000 mpaka 4,000. Maana yake ni kwamba, ikizimwa *POS* kwa siku 4,000 unazungumzia miaka zaidi ya mitatu mbele. Nyingine imezimwa zaidi ya siku 1,000 nyuma. Yaani hata kabla ya mfumo wa *POS* haujaanzishwa, *POS* imeshakuwepo na imezimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni kwamba watu wanazima mashine na kurudisha mfumo nyuma wakati hela inayokusanywa haitoonekana popote pale. Na ile iliyopelekwa mbele maana yake ni kwamba ile fedha hautaiona wewe ambaye ni msimamizi pale. Kwa hiyo tunadhani yapo majukumu na ulazima kabisa wa Serikali kusimamia hili jambo na kuweka mifumo ambayo itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kabla sijasoma maazimio ya Bunge lako, nijielekeze kwenye maelezo mafupi sana ya utangulizi. Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 kinatamka bayana kwamba

ukaguzi unaotekelezwa na *CAG* ni kwa niaba ya Bunge. Naomba kuliarifu Bunge lako kwamba *LAAC* imejiridhisha kwamba kuwa ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021 ulizingatia misingi ya Katiba na Sheria za nchi na viwango vya Kimataifa na Kitaifa. Katika kufikia hoja za ukaguzi zilizojadiliwa na Kamati. Aidha, kifungu cha 16 cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 kimeweka Sharti la kwamba msingi wa kazi za *LAAC* ni taarifa ya ukaguzi uliotekelezwa na *CAG*.

Mheshimiwa Spika, Kwa sababu hizo, mapendekezo ya maazimio ambayo nitayawasilisha hivi punde yanatokana na uchambuzi wa Kamati kuhusi ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wa Hesabu za Serikali kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha ulioishia Juni 2021. Aidha, maazimio haya pia yamezingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge mbali mbali ambayo imetolewa hapa Bungeni kwa kujadili taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Wabunge zaidi ya 82, miongoni mwao Wabunge 71 wamechangia juu ya taarifa ya Kamati ya *LAAC,* na uchangiaji wao umetusaidia sana kuboresha maazimio yetu tuliokuwa tumeyatengeneza na kuyatoa awali. Ni matumaini ya Kamati ya kwamba maazimio haya yatasaidia katika kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu nijielekeze kuwasilisha mapendekezo, hasa nijielekeze kuwasilisha maazimio kumi na moja kama ifuatavyo: -

(1) Mheshimiwa Spika, azimio la kwanza ni kuhusu mfuko wa mikopo kwa vikundi vya kina mama, vijana na wenye ulemavu. Ukaguzi uliofanywa na *CAG* umeonyesha kasoro mbalimbali za uendeshaji wa mfuko huu ikiwemo: -

(a) Halmashauri 155 kushindwa kukusanya shilingi bilioni 47.01 zilizotolewa kwa vikundi mbali mbali.

(b) Halmashauri 11 kushindwa kuhamisha shilingi bilioni 1.24 kutoka Akaunti ya Amana kwenda akaunti ya mifuko.

(c) Halmashauri 17 zilitoa mikopo ya shilingi bilioni 3.26 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu bila kuzungatia uwiano ulioanishwa.

(d) Halmashauri 83 kutokuchangia jumla ya shilingi bilioni 6.68 kwenye mfuko kutoka kwenye mapatao yake ya ndani.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Bunge linaazimia ya kwamba, Mamlaka ya nidhamu ya Wakurugenzi ichukue hatua dhidi ya Wakurugenzi wote waliobanika kushindwa kwa uzembe kusimamia kikamilifu utoaji na usimamizi wa mikopo hii kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni ya 24(2) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

(2) Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa ruzuku ya maendeleo katika mamlaka za Serikali za Mitaa. Bunge linaitaka Serikali kutekeleza yatuatayo: -

(a) Kuzingatia matakwa ya sharia ya matumizi ya fedha zinazopitishwa na Bunge katika kila Mwaka wa Bajeti ili kuendelea kujijengea imani Bungeni na kwa wananchi.

(b) Kuweka angalau karibio kwa kiasi cha ruzuku endapo itabidi baadhi ya halmashauri kuzidishiwa kuliko vile inavyotokea kwamba halmashauri zingine hupewa kiasi kidogo mno wakati zingine hupewa zaidi ya asilimia hamsini.

(c) Kutorejesha Hazina fedha zinazokuwa zimepelekwa katika halmashauri kwa madai kuwa mwaka husika wa fedha umeisha ili kukamilisha miradi inayohusika.

(3) Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji wa tija, kuhusu uwekevu na tija katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Ukaguzi umebainisha dosari zinazohusu uwekezaji wa mitaji ya umma katika baadhi ya halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, dosari hizo ni pamoja na uwekezaji unaofanyika bila upembuzi yakinifu wala andiko la biashara. Bunge linaitaka Serikali, kuhakikisha kuwa halmashauri zote zinazofanya uwekezaji, unazingatia fursa za uwekezaji na tija katika maeneo mbalimbali ya halmashauri kuliko hali ilivyo sasa ambapo kila halmashauri inataka kuwekeza kwenye soko na kituo cha mabasi tu. Aidha, Serikali iandae muongozo na kanuni inayoelekeza namna bora ya uwekezaji kwa ngazi za halmashauri na kuzingatia umuhimu wa maandiko miradi kabla ya kuanza miradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu manunuzi na mikataba ya upatikanaji wa huduma na bidhaa. Ukaguzi umebaini udhaifu katika ununuzi na upatikanaji wa huduma na bidhaa katika halmashauri bila kufuata taratibu zinazohusika. Hali hiyo inaweka mwanya wa upotevu wa fedha za Umma. Hivyo basi, Bunge linaiagiza Serikali kusimamia ipasavyo manunuzi yote ya Umma kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na kwa kuridhiwa na Bunge. Aidha, Maafisa Masuuli wote watakaobainika kutosimamia ipasavyo agizo hili, wachukuliwe hatua kali za kisheria kwa nia ya kukomesha ubadhirifu na kulileteа Taifa manufaa stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu upatikanaji wa stahiki za watumishi kwa mujibu wa sheria. Bunge linaitaka Serikali kushughulikia mara moja madai yote ya stahiki za watumishi wa halmashauri kwa mujibu wa sheria ambazo hazijatolewa na kuchukua hatua kali kwa waajiri wasiozingatia matakwa ya sheria zinazohusika na stahili za watumishi.

Mheshimiwa Spika, sita, kuhusu ukusanyaji wa mapato ya ndani ya halmashauri. Imebainika kwamba halmashauri zilizo nyingi zina udhaifu katika eneo la ukusanyaji wa mapato ya ndani kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo upotevu wa mapato kwenye mifumo ya kielektroniki, rushwa na kutosimamia ipasavyo sheria, kanuni na taratibu za kifedha; hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kuwa mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato, yaani *TAUSI*, unaanza kutumika katika halmashauri zote za Serikali nchini ndani ya mwaka wa fedha wa 2022/2023;

(b) Kuchukua hatua kali za kisheria kwa watendaji wote ambao wanakusanya mapato nje ya utaratibu wa kisheria na ambao hawapeleki makusanyo hayo benki kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, saba, kuhusu matumizi yasiyofaa ya fedha katika Akaunti za Amana. Imebainika ya kwamba katika halmashauri mbalimbali fedha zilizomo katika Akaunti za Amana zinatumika kwa shughuli ambazo hazikutarajiwa. Ripoti ya *CAG* ilibainisha matumizi mabaya ya Shilingi bilioni 9.74 kutoka katika Akaunti za Amana kutokana na kutosimamiwa ipasavyo. Matumizi hayo yalibainika katika halmashauri 81 nchini na hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinazowekwa katika Akaunti za Amana zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kuliko hali ilivyo sasa ambapo akaunti hizo zinaonekana kutumika kama maficho ya fedha ambazo baadaye hutumika kibadhirifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Maafisa Masuuli wote waliotumia fedha hizi kinyume na uataratibu wachukuliwe hatua kali za kinidhamu. Mifano ipo kama ambavyo tuliitaja, kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ilitumia zaidi ya Shilingi milioni 90 bila utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, azimio la nane, kuhusu upotevu wa mapato katika mifumo ya kielektroniki ya kukusanyia mapato. Imebainika kuwepo kwa upotevu wa mapato kupitia katika mifumo ya kielektroniki katika halmashauri zetu. Katika mwaka wa fedha 2021, halmashauri 27 zilifanya marekebisho ya miamala yenye jumla ya Shilingi

bilioni 1.6 kwenye mfumo bila uthibitisho wa ulazima na uhalali wa marekebisho hayo kufanyika. Hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watumishi wote waliohusika na upotevu, mathalan watumishi walio katika halmashauri ambazo miamala ya mapato ilibadilishwa au kufutwa bila uthibitisho wa ulazima wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tisa, kuhusu hasara ya kifedha kutokana na vitendo vya taasisi za Serikali dhidi ya halmashauri. Imebainika kuwa, jumla ya Shilingi bilioni 2.34 hazijalipwa katika mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa nchini kutokana na huduma za tiba zilizotolewa kwa wanufaika wa mfuko huo. Hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kushughulikia mara moja suala la *NHIF* kutorejesha gharama za matibabu na vifaatiba vinavyotolewa na halmashauri kwa wanufaika wa bima ya afya chini ya mfuko huo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Mheshimiwa Spika, Bohari ya Madawa *(MSD);* Halmashauri nyingi zimekuwa zikilipa fedha kwa bohari ya madawa nchini *(MSD)* pasipo kupelekewa dawa na vifaatiba kwa wakati. Zaidi ya Shilingi bilioni 1.17 hazijawahi kupelekwa kwenye vituo dawa za gharama hiyo. Hivyo Bunge linaitaka Serikali kuisimamia ipasavyo *MSD* ili iwe inapeleka dawa na vifaatiba katika halmashauri kwa muda usiozidi mwezi mmoja kulingana na mahitaji ya halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini *(GPSA)*. Imebainika kuwa halmashauri mbalimbali zimekuwa zikiamrishwa au zikihimizwa kupeleka fedha kabla ya kupata huduma au bidhaa husika kwa upande wa uagizaji na manunuzi ya magari.

Wameshindwa kufanya vizuri kwani wamekuwa na tabia ya kurudisha fedha kwa wateja pasipo kukamilisha manunuzi ya magari hayo kwa muda uliopangwa. Hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kuisimamia *GPSA* ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi zao ili kuzisaidia halmashauri katika utekelezaji wa mipango yao kuliko hali ilivyo sasa ambapo *GPSA* huchangia kuzizorotesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)*. Bunge linaitaka Serikali kuimarisha *TEMESA* ili iweze kuzisaidia halmashauri na taasisi nyingine za Serikali ili kupunguza malalamiko ya udhaifu wake katika eneo la ukaguzi na utengenezaji wa magari na mitambo katika halmashauri.

Mheshimiwa Spika, azimio la kumi, kuhusu uteketezaji wa dawa za binadamu katika halmashauri na vituo vya afya. Taarifa ya *CAG* ya mwaka wa fedha 2021 inaonesha kuwepo kwa wimbi kubwa la uteketezaji wa dawa za binadamu zenye thamani kubwa ya fedha. Kwa miaka mitatu tuliyotolea mfano, zaidi ya Shilingi bilioni 12.3 katika halmashauri 91 dawa zake ziliteketezwa. Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa hazipokei dawa zilizobakiza muda wa matumizi unaopungua miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, azimio la 11, upungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Uchambuzi wa Kamati kutokana na taarifa ya *CAG* umebainisha kuwa, baadhi ya halmashauri hazina watumishi wenye taaluma unaohitajika na kulazimika kutumia watumishi wasio na sifa kwa kazi zinazohitaji utaalamu. Kitendo hiki

kinasababisha kufanyika kwa maamuzi yanayosababisha hasara kubwa katika halmashauri zetu. Hivyo basi, Bunge linaitaka Serikali kupeleka katika kila halmashauri wataalamu wa kutosha kwenye sekta zote muhimu zinazohitajika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuwatumia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa mijadala mizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana.

Makamu Mwenyekiti, kabla hujatoka hapo, hili azimio la tano, hii sehemu ya kwanza ya uchambuzi wa Kamati, maana ni jambo muhimu sana kuhusu stahili za watumishi. Kabla haujasoma hilo azimio, hebu tusomee hapo uchambuzi wa *CAG* kama uko nao hapo mbele.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa stahili za watumishi kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Eh, tusomee yote.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya *CAG* umebaini malimbikizo ya muda mrefu ya mishahara yenye thamani ya Shilingi bilioni 63.83 kwa watumishi 33,405 ambayo hayakulipwa. Vile vile kuna madai mengine ya watumishi 71,670 yenye thamani ya Shilingi bilioni 96.65 ambayo yalikuwa hayajalipwa yakiwa ni posho za likizo, gharama za uhamisho na posho nyingine. Kwa hiyo basi, Bunge linaitaka Serikali kushughulikia mara moja madai yote ya stahiki za watumishi kwa halmashauri zilizoko nchini kwa mujibu wa sheria ambazo hazijatolewa na kuchukua hatua kali kwa waajiri wasiozingatia matakwa ya sheria zinazohusika na stahiki za watumishi.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hoja ilikuwa imeshaungwa mkono. Sasa kabla sijawahoji, hoja hii kwa sehemu kubwa sana ukiacha hii sehemu ya utumishi ambayo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wote wanahusika. Mheshimiwa Waziri haya yatakuwa ni maagizo pamoja na mengine yaliyo kwenye taarifa ya *CAG*. Kuna agizo lolote ambalo hapa unaona kwamba halitekelezeki?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hiyo ya kusema Mamlaka ya Nidhamu ya Mkurugenzi, nadhani tumwachie Mheshimiwa Rais maana unakuta yeye ndiye anayewateua, sisi tunapeleka tu mapendekezo. Lugha iliyotumika hapo nadhani tunaingilia mamlaka ya Rais.

**SPIKA:** Eh, si ndiyo wamesema mamlaka inayohusika! Kwa hiyo, anayehusika, Mheshimiwa Rais atapelekewa yeye mwenyewe. Sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ulikuwa na jambo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nadhani kwa sababu azimio linatutaka tutekeleze na hasa malimbikizo ya mishahara; na bahati nzuri tumeshatekeleza; na kama nilivyotoa taarifa, Mheshimiwa Rais toka ameingia madarakani, hayo yalikuwa ni malimbikizo ya muda mrefu kwa ripoti ya 2020/2021; na mpaka sasa *arrears* za mishahara tumeshalipa zaidi ya Shilingi 196,083,000,000/=. Kwa hiyo, agizo linaweza kubaki, lakini kwa taarifa ijayo ya *CAG* itaonekana hii *progress report* ambayo tayari Serikali imeshafanya mara tatu zaidi ya kile ambacho kimejionesha kupitia kwenye utendaji kazi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia lipo agizo la kuitaka Serikali ipeleke watumishi. Wakati nachangia nilikuwa pia nimeomba, kwa sababu kadiri tunavyoajiri na mmeona nia ya Serikali ya kuajiri, tunaenda pia na *wage bill* ya

Taifa. Hata hivyo tunao uwezo wa kuangalia *human resource* tuliyonayo na wakati mwingine mamlaka tulizozikasimia. *Regional Secretariat* wana uwezo wa kufanya *recategorization* ili kuondoa tatizo la watumishi kwa haraka, yaani hiyo ni *solution* ya muda mfupi. Wana uwezo wa kuweka kwenye bajeti na kuwasomesha watumishi. Wakati tunaendelea kuajiri, lakini watumishi wale wale walioko kwenye maeneo yao wanao uwezo pia wa kusomeshwa.

Mheshimiwa Spika, tumegundua lipo tatizo moja kubwa ambalo ndiyo tunali-*address* sasa hivi, kwamba waajiri wengi, ama tu kwa kutokutaka, wakati mwingine kwa roho mbaya, wakati mwingine kwa tabia tu iliyojengeka, hawataki kutenga bajeti na hawataki kuwasomesha watumishi wao. Wangetenga bajeti na kuwasomesha, kwa namna fulani ingawa siyo kwa kiasi kikubwa, tungeondoa tatizo na wakati huo huo tuna-*control wage bill*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria haya yote mawili yaende sambamba; la kuajiri na kufanya *recategorization* kwa kuzingatia mahitaji na hasa kwa waajiri waliokasimiwa madaraka kuangalia ni nini wanaweza kufanya kwa ikama iliyozidi ndani ya maeneo yao.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Hili nadhani Waheshimiwa Wabunge linaenda vizuri kabisa kwa sababu na sisi tumeshapendekeza watu wachukuliwe hatua. Kwa hiyo, wale watakaochukuliwa hatua, pale watakapopungua watakuwa wamepunguza mzigo kwenye *wage bill,* kwa hiyo, waajiriwa wapya wapelekwe kwenye hayo maeneo. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Zuberi M. Kuchauka, alisimama)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, umesimama kwenye hoja gani?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nina hoja kwenye azimio la tisa, sehemu ya tatu, kuhusu *GPSA*. Naona kama azimio haliko *complete enough* kwa sababu nilikuwa nafikiria twende kama tulivyoazimia kwa watu wa *MSD*.

**SPIKA:** Kuhusu *GPSA*, ehe!

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hoja hapa kwamba azimio letu naona kama haliko *complete enough,* kwa sababu hawa *GPSA* bado wamepewa *room* tena na Serikali kwamba waendelee kusimamia, *GPSA* yaani ni mambo yanajirudia yale yale. Mimi nafikiri tuwape azimio *concrete issue* kwamba bwana, kama *GPSA* wameshindwa kuihudumia halmashauri; labda wameagiza gari, kama wameshindwa warudishe fedha na wapewe *option* kwamba halmashauri wakanunue sehemu nyingine.

**SPIKA:** Tatizo linalojitokeza hapo ni kwamba wakati fedha hizo zikirejeshwa, hata hiyo bei ya hivyo vifaa itakuwa imeshapanda tayari. Kwa hiyo, ni tatizo kubwa zaidi.

Nadhani tumezungumzia *GPSA* kwenye *PAC,* si ndiyo! Kwa hiyo, hii ilikuwa ni *GPSA* kwenye eneo la halmashauri. Kwa hiyo, kwa kuwa tumeiazimia kule kwenye *PAC,* tunaweza kubaki na lile azimio. Hawa

kidogo tumechelea kuipangia muda mahususi, lakini tatizo kubwa linajulikana na nadhani watakuwa wametusikia. Kwa hiyo, nao wakajitazame huko, wasizoroteshe shughuli za wananchi kwa hiyo, hoja yako imeeleweka, ila hapa ilikuwa mahususi kwa ajili ya halmashauri. Nadhani huko mbele tunakoenda, Kamati mwendelee kutazama namna bora ya kushughulika nayo hii *GPSA,* kwa sababu ukirudisha fedha baada ya miezi sita, umeshawacheleweshа hawa watu na pia hoja ile ya kwamba fedha nyingi zimeenda na bado haijatekeleza, nadhani ni jambo endelevu, kwa sababu kuna fedha nyingine zilizotolewa mwaka 2021. Sasa ile 2021/2022 nadhani ndiyo *GPSA* itakuwa na maswali mengi zaidi kuliko hata sasa hivi.

*(Hapa Naibu Waziri wa Afya na Mheshimiwa Subira K. Mgalu walisimama)*

**SPIKA:** nawaona Waheshimiwa wawili mmesimama, sijui unatoa ufafanuzi! Tuanze na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, tutamalizia na Mheshimiwa Subira.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, mimi nilitaka tu nizungumzie kwenye hili eneo la kusema kwamba tusipokee dawa ambazo ziko chini ya miezi sita; tunakubaliana na ndiyo tunataka iwe hivyo, lakini naomba tuongezee hapo; pamoja na kwamba tunakubaliana kabisa isiwe chini ya miezi sita, tuongezee *phrase* ya kuonyesha kama kuna sababu za kisayansi na kitiba ambazo zitaruhusu chini ya muda huo, iruhusiwe, kwa sababu tuna dawa hizi za wadau hasa kwenye eneo la UKIMWI. Wakati mwingine wanaleta, hazina shida, lakini ziko chini ya miezi mitatu kama ziruhusiwe ziingie ili tusipoteze, kama Bunge litakubali.

Mheshimiwa Spika, tunaomba hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa hilo kwa sababu tulishapitisha kule kwingine, hatuwezi kuja kulibadilishia hapa. Kwa sababu tulishahojiana kule. Walichokifanya Wenyeviti ni kwamba taarifa ile ya *PAC* isipingane na *LAAC* kwa maana ya muda. Sasa ile tulishahoji, kwa hiyo, hatuwezi kurekebishia hapa. Kama kutakuwa na marekebisho, basi yatakuja kufanywa wakati wa baadaye. Ila hili ulilosema ndiyo linalotutishia zaidi, hao wahisani wasituletee dawa; wanatuongezea gharama tu za kuharibu hizo dawa. Wasituletee ambazo muda umekwisha, kwa sababu sasa ni kama hili eneo linakuwa la kutupia dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Subira.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, kwenye azimio linalohusu mapato ambayo yalifutwa kwenye mfumo, naomba Makamu Mwenyekiti, *figure* ambayo aliitaja kama bilioni moja lakini ripoti ya *CAG*…

**SPIKA:** Ni namba ngapi?

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, nadhani ni azimio namba saba au nane la kuhusu mfumo wa kukusanya mapato.

**SPIKA:** Upotevu wa mapato katika mifumo ya kieletroniki.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, hoja ilisema kwamba, mapato ambayo yamefutwa kwenye

mfumo bila kuzingatia taratibum ripoti ya *CAG* hapa inasema bilioni 28.33, badala kama ya bilioni moja, kama sikosei ,kama nimesikia vizuri…

**SPIKA:** Bilioni ngapi?

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, inasoma bilioni 28.33.

**SPIKA:** Bilioni 28.33.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, samahani naomba nisome. Aidha, nilibaini kuwa halmashauri 16 zilifanya marekebisho ya miamala katika mfumo wa mapato kwa kufuta mapato yenye jumla ya shilingi bilioni 28.33 bila kuzingatia taratibu zilizowekwa. Hivyo kusababisha uwezekano wa uwepo wa ubadhirifu na hii ipo chini ya matokeo ya ukaguzi maalum.

Mheshimiwa Spika, sasa kama nimesikia vizuri alitaja bilioni moja ambayo hiyo pia ipo chini yake kwamba, halmashauri saba hazikuwasilisha kwangu hati za malipo zenye thamani ya bilioni 1.37. Sasa nikaona kwa sababu kuna *figure* kubwa ambayo inaoneka mapato yalifutwa kwenye mfumo bila sababu za msingi.

**SPIKA:** Ni Azimio la nane kama ulivyosema na hapa ilikuwa inasomeka bilioni 1.6, kwa hivyo ni bilioni 28.33, Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ukiendelea hapa chini, hizi fedha zimegawanywa kwenye

maeneo mbalimbali hasa wakati wa uchambuzi kwa sababu sisi tumekutana na halmashauri mbalimbali ili kupata hiki, mbali ya kuwa ripoti ya CAG ina ukubwa wake. Kwa hiyo ukienda chini pale anasema halmashauri 27 zilifanya marekebisho ya miamala yenye jumla ya shilingi bilioni 1.6, marekebisho. Kwa hiyo kwenye kipengele cha marekebisho peke yake ambacho sisi ndio tumekizungumzia, ndio kimeeleza huo upotevu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ile ripoti yetu ya kwanza ilikuwa na mlolongo mwingi sana. Nashukuru.

**SPIKA:** Kwa hiyo Mwenyekiti, kwa maelezo yaliyoko hapa kwenye hili Azimio inabidi tubaki na 1.6.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA-MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ibaki hiyo hiyo, kwa sababu hoja niliyoizungumzia na ukiangalia kuna nyingine naiangalia hapa, ziko mbili na yenyewe ina moja pointi, ni zile ambazo zilikuwa zinabadilishwa kwenye mifumo bila idhini ukiachilia kabisa kwa ujumla ya zile zilizopotea kwa ujumla wake. Nakushukuru.

**SPIKA:** Sawa, Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumeelewana, hii ni mahususi ya upotevu wa mapato katika mifumo ya eletroniki, lakini wanazungumzia ile miamala ambayo ilirekebishwa. Kwa hiyo hiki ndio kiasi mahususi, lakini kile kiasi alichotaja kwenye taarifa ya CAG maana yake ni kile ambacho huenda kimetawanyika kwenye hizi taarifa nyingine pia ama maazimio mengine ambayo Kamati imeyaleta.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kupata ufafanuzi kutoka upande wa Serikali sasa nitawahoji kuhusu Taarifa ya Kamati yetu ambayo imesomwa hapa na Mwenyekiti, kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na yale ambayo yako kwenye Taarifa sasa ya *CAG* yanayoangukia chini ya Kamati yetu ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Bunge zima limeafiki, ahsante sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Mheshimiwa Jerry William Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na wenzangu kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kutoa muda wa kutosha wa ripoti za Kamati hizi tatu, kujadiliwa na Bunge kwa kipindi cha siku nne, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, niwashukuru sana Wabunge kwa michango yao. Tumepata michango ya jumla ya Wabunge 83. Katika hao Wabunge 19 wamechangia hoja mahususi ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma tokea Novemba mpaka leo. ukiondoa waliochangia Taarifa ya Hesabu za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa pekee, wachangiaji Taarifa ya *PAC* waliyagusa mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, wakati nawasilisha Taarifa ya Kamati, Kamati ilikuwa na mapendekezo nane, baada ya majadiliano Kamati imeboresha mapendekezo kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge jumla ya mapendekezo matano hivyo kupelekea jumla ya mapendekezo kufika 13.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu ya Kamati yetu ya *PIC* ya kuangalia ufanisi na tija ya uwekezaji na pamoja kwamba ripoti za ukaguzi zinawasilishwa ila tunazitumia tu kwa ajili ya kukokotoa vigezo vya uwekezaji. Wenzetu wa *PAC* wana majukumu ya hoja za ukaguzi wa mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, mashirika yafuatayo ambayo tunayasimamia uwekezaji wake, yametajwa na yameonekana yana hoja za ukaguzi wa mabilioni ya shilingi. Mashirika hayo ni pamoja na *NHIF, TRA, DART, KADCO, TANROADS, MSD, TPA, TRC, TAMESA, GPSA,* Bodi ya Mikopo, Ngorongoro *Conservation*, *REA, DUWASA* na *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hoja za ukaguzi kwenye ripoti ya *CAG* ya mwaka wa fedha 2020/2021 ndio yamepelekea kutofikia lengo la makusanyo ya Msajili wa Hazina kwa maana katika lengo la kukusanya gawio la shilingi bilioni 308.82 sawa na asilimia 75 ya lengo ilikusanywa. Katika michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi, ni jumla ya shilingi bilioni 202.2 tu sawa na asilimia 51 ya lengo ilikusanywa. Kama mashirika haya yangesimamia fedha vizuri, basi wangeokoa fedha za

walipakodi, faida ingeongezeka na mchango kwenye Mfuko Mkuu wa Taifa ungeongezeka.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kusoma maoni na mapendekezo ya maazimio ya Kamati, naomba kuzungumzia mambo mawili ambayo yamechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge, ili kama yataboreshwa inawezekana ile mianya ya uvujaji wa mapato, katika hela za umma na matumizi yasiyo ya lazima yanaweza kufikiwa. Maeneo hayo mawili la kwanza ni la mifumo. Wachangiaji wengi wamechangia mifumo mbalimbali na kwenye mifumo nimeona kuna maeneo mawili. Kwanza mifumo mingi ni dhaifu, utasikia *POS* inaongezwa muda fedha zinafutwa, labda *GPSA* wanakuwa hawana mifumo mizuri ya uwagizaji, *TANePS* haijibu majibu ya manunuzi. Kwa hiyo mifumo mingi iliyopo kwenye nchi yetu ni dhaifu.

Mheshimiwa Spika, mifumo inakuwa dhaifu kwa mambo mawili tu, moja, aidha, inapewa udhaifu kwa makusudi katika kutengeneza mianya ya upigaji wa fedha za umma. Kwa sababu mfumo unapokuwa madhubuti kama ilivyo mifumo yetu ya miamala ya simu, sijawahi kumsikia hata Mheshimiwa mmoja huku anasema hela zake zilizopo kwenye miamala ya simu zimepotea, zimevuja, zimefutwa au salio halionekani. Kwa hiyo mifumo inapokuwa dhaifu inawezekana ni kwa makusudi katika kutengeneza utaratibu wa uvujifu wa mapato na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, tuliwahi kulizungumza hapa Bungeni, ni Serikali kushindwa kufika mwisho wa mambo mawili. Moja, ni ujengaji wa mfumo wa *public infrastructure* kwa maana ya *PKI* ambao ndio mfumo

unaweza kusaidia *authentication* ya *transactions* zote za kieletroniki kwenye mifumo hii ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, la pili, kutokuwa na *centralize ledger,* kwa sababu ukisikia hapa kuna mtumishi ana malimbikizo ya mshahara na kuna mtumishi amestaafu amelipwa na kuna mapato yamekusanywa ghafi yameliwa, maana yake hakuna sehemu ya pamoja ambapo Taifa la Tanzania, nchi yetu, tunakuwa na *centralized system* ambayo inaweza kuona, vitendo kama hivi havifikiwi na kama vinafikiwa vinaweza kuonekana ni nani kafanya nini na lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimesema niyaseme haya kwa utangulizi kwenye mifumo na tutakuwa na maazimio mahususi. La pili, ni Bodi za Wakurugenzi. Nadhani nilichangia pale nyuma siyo vyema kwa kuokoa muda, lakini Kamati inaomba kidhati kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa nia yake na vitendo vyake ambavyo anaonyesha wazi, anaunga mkono si tu uwekezaji kwenye mashirika ya umma lakini sekta nzima ya uwekezaji kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pale awali nilieleza kwamba kwenye uteuzi wa bodi Mheshimiwa Rais amewahi kunukuliwa hadharani akieleza ni jinsi gani anatimiza wajibu wake pale tu anapopelekewa uteuzi wa bodi. Kama nilivyoeleza pale awali jumla ya mashirika 23 kufikia Octoba 31, yalikuwa yana bodi zilizomaliza muda wake na hazijateuliwa. Kwa kudhibitisha kauli ile ya Mheshimiwa Rais, yako mashirika 12 yaliyopo kwenye Wizara tisa (9) ambayo tayari Mheshimiwa Rais ameshateua Wenyeviti wa Bodi na Wajumbe ambao ni mamlaka ya uteuzi wa Wizara kuteua, hawajateuliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa mapendekezo 13 na kati ya hayo kama nilivyosema pale awali nane yalipendekezwa na Kamati na matano yametokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Taasisi kutokuwa na bodi za wakurugenzi kwa muda mrefu kutokana na kuchelewa kuteuliwa kwa Wajumbe wa Bodi:-

KWA KUWA mashirika mengi yanayotumia mitaji ya umma yameendeshwa bila kuwa na Bodi za Wakurugenzi kutokana na bodi zilizokuwepo kumaliza muda wake;

NA KWA KUWA hadi sasa kuna taasisi na mashirika 12 ambayo yana Wenyeviti wa Bodi na bila wajumbe na taasisi za mashirika 23 ambayo hayana kabisa Wenyeviti wala Wajumbe wa Bodi, jambo ambalo ni ukiukwaji wa misingi ya utawala bora katika uwekezaji wa mitaji ya umma na kwamba ni jambo linalokwamisha upatikanaji wa tija uwekezaji unaofanywa na Serikali;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ikamilishe uteuzi wa wajumbe wa Bodi 12 kwenye Wizara tisa ambazo Mheshimiwa Rais ameshateua Wenyeviti ndani ya miezi 3. *(Makofi)*

(b) Serikali ikamilishe uteuzi wa Wajumbe wa Bodi 23 kwenye Wizara 12 ambazo hazina bodi ndani ya miezi sita.

(c) Serikali ihakikishe inatimiza utaratibu wa kuanza maandalizi ya uteuzi wa bodi miezi tisa kabla bodi hazijamaliza muda wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, changamoto ya kupata vibali vya kuajiri:-

KWA KUWA mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara yanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi katika kujiendesha kwake kutokana na kutegemea mchakato wa ajira unaoendeshwa na Sekretarieti ya Ajira ya Utumishi wa Umma katika kupata watumishi;

NA KWA KUWA changamoto hiyo inaathiri tija ya uwekezaji na manufaa yaliyotarajiwa kupatikana kutokana na kukosa watumishi wanaostahili kwa wakati, hata pale ambapo Shirika la Umma linakuwa na uwezo wa mapato wa kuwalipa mishahara;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Serikali iweke utaratibu maalum wa kutoa vibali kwa taasisi zinazojiendesha kibiashara ili ziweze kuajiri zenyewe ajira ya moja kwa moja na kuweza kuendana na soko la ushindani kibiashara.

Mheshimiwa Spika, tatu, uwezo wa *SGR* kuzidi uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam:-

KWA KUWA Bandari ya Dar es Salaam ina uwezo mdogo wa kupokea mizigo kulinganisha na uwezo wa *SGR* iliyoigharimu Serikali kwa uwekezaji mkubwa ilihali bandari hiyo ndio chanzo kikuu cha mizigo. Hii itachangia

*SGR* isipate mzigo wa kutosha kwa ajili ya kusafirishwa pindi itakapokamilika;

NA KWA KUWA changamoto ya *SGR* kutopata mzigo wa kutosha kusafirishwa ni jambo linalokwamisha kupatikana kwa tija ya uwekezaji uliofanyika na kwamba mkwamo huo unaweza kutatuliwa kwa kuongeza Bandari ya Dar es Salaam na kujenga Bandari ya Bagamoyo;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

(b) Serikali iharakishe zoezi la kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kuongeza gati za kisasa katika Bandari ya Dar es Salaam na zoezi hilo likamilike kabla ya ujenzi wa reli ya *SGR* kukamilika. Hatua hii itasaidia *SGR* kupata mzigo wa kusafirisha na hivyo tija iliyokusudiwa kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, nne, umuhimu wa Shirika la Maendeleo *(NDC)*:-

KWA KUWA manufaa ya mradi wowote wa uwekezaji yanategemea kuanza kwa mradi lakini Mradi wa Mchuchuma na Liganga umechukua muda mrefu katika hatua za majadiliano ambayo kwa sasa yanaratibiwa na Kamati ya Majadiliano ya Serikalini *(GNT);*

NA KWA KUWA kutokukamilika kwa majadiliano hayo yanayoendelea kwa muda mrefu tangu kuanza

kwake ni jambo linalochelewesha upatikanaji wa manufaa ya mradi huo;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe kuwa mazungumzo yanayoendelea katika Kamati ya Majadiliano ya Serikali *(GNT),* yanafika mwisho ndani ya miezi mitatu au yapelekwe *NDC,* lengo ikiwa kuyamaliza na kupata tija inayokusudiwa katika miradi, kwa sababu Serikali imefanya mabadiliko makubwa katika taasisi hii ikiwemo kuipatia Bodi mpya ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti.

Mheshimiwa Spika, tano, mikopo chechefu *(non-performing loans)*:-

KWA KUWA imebainika kuwa baadhi ya taasisi kama vile Benki ya Maendeleo *(TIB)* na Benki ya Biashara *(TCB)* zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na kiasi kikubwa cha mikopo chechefu *(non-performing loans);*

NA KWA KUWA hali hiyo inaathiri mizania ya vitabu vya taasisi hizo jambo ambalo ni hatari kwa misingi ya kibiashara na uendeshaji wa taasisi zinazotumia mitaji ya umma;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ifanye tathmini ya madeni hayo na kuhakikisha wanayaondoa kwenye vitabu vya benki hizo bila kuathiri ulipaji wa mikopo inayolipika *(performing loans)*. Hatua hiyo itasaidia benki hizo kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija inayokusudiwa.

(b) Serikali itengeneze mfumo fungamanishi kati ya Bodi ya Uhasibu *(NBAA),* Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* na Taasisi za Fedha na wafanyabiashara ili chanzo cha hesabu zote zinazotumiwa na wafanyabiashara kiwe kimoja. Hii itasaidia kukadiria kiwango halisi cha mkopo kinachoweza kulipika na mkopaji ili kupunguza mikopo chechefu.

Mheshimiwa Spika, sita, upungufu wa mtaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)*:-

KWA KUWA Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* inakabiliwa na changamoto ya mtaji hasi na changamoto ya uendeshaji wa biashara kutokana na utaratibu wa kukodisha ndege kutoka Wakala wa Ndege za Serikali *(TGFA);*

NA KWA KUWA utaratibu huo unaongeza madeni wanayodai yaani *payables* katika vitabu vya *TGFA.*

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania *(TGFA)* ikamilishe taratibu za kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alipokuwa anapokea Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tarehe 30 Machi, 2022 la kurudisha umiliki wa ndege kwa *ATCL* kwani ukiondoa tatizo hili *ATCL* ina uwezo wa kujiendesha kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, saba, kuiwezesha Benki ya Maendeleo ya Kilimo*(TADB)*:-

KWA KUWA *TADB* ambayo ndio benki pekee inayohusika moja kwa moja na shughuli za kilimo, lakini haijapatiwa mtaji wa kutosha na kuendana na nia ya Serikali ya kuongeza tija kwenye kilimo, kuleta mageuzi ya kilimo na kulisaidia Taifa kufikia usalama wa chakula;

NA KWA KUWA pamoja na jitihada za Serikali kuipatia *TADB* kiasi cha shilingi milioni 208 mwaka 2021, bado kuna ahadi ya Serikali ambayo kama ingetekelezwa benki hii ingekuwa na mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 760. Kutofikiwa kwa mtaji huu kunaathiri ufanisi na tija katika sekta ya kilimo;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze ahadi yake *(commitment)* waliyoitoa kwa *TADB* ya kuiongezea mtaji kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa kila mwaka wa fedha, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nane, kuathirika kwa kilimo cha pamba kutokana na maelekezo ya Serikali ya mwaka 2019 ya kuuza pamba kwa bei ya juu zaidi ya soko la dunia:-

KWA KUWA agizo la Serikali inayoitaka pamba kununuliwa kwa bei ya juu zaidi ya soko la dunia imeathiri uwezo wa wanunuzi wa pamba kwa kiasi cha shilingi bilioni 21.8, kiasi ambacho Serikali iliahidi kufidia deni hilo;

NA KWA KUWA deni hilo limeathiri taswira ya Bodi ya Pamba kwa wakulima na kuongeza changamoto katika biashara ya kilimo cha pamba;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba, Serikali iharakishe utekelezaji wa ahadi yake ya kulipa deni la pamba. Hatua hiyo itasaidia kuongeza ufanisi wa sekta hiyo na kurudisha taswira chanya ya Bodi ya Pamba.

Mheshimiwa Spika, tisa, mwingiliano wa majukumu kwa baadhi ya taasisi za umma:-

KWA KUWA mwaka 2017 Serikali iliamua majukumu ya Tanzania *Air Port Authority* ya kujenga viwanja vya ndege yahamie *TANROADS*;

NA KWA KUWA jambo hili ni kinyume cha viwango vya kimataifa na ni kinyume cha matakwa ya *International Civil Aviation Organization (ICAO)* ambayo Tanzania *Air Port Authority* ni mwanachama wake na *ICAO* inazitaka Mamlaka za Viwanja vya Ndege kusimamia shughuli zote za viwanja vya ndege ikiwemo ujenzi wa viwanja vyao;

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Serikali itekeleze haraka agizo la kurejesha jukumu la ujenzi wa viwanja vya ndege kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* pamoja na rasilimali zake zote ikiwemo watumishi waliohama mwaka 2017. Hii ni muhimu kwa ajili ya kukidhi viwango vya kimataifa katika uendeshaji wa viwanja vya ndege. *(Makofi)*

(10) Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

KWA KUWA, katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano, Serikali inatekeleza mageuzi ya

kidigitali yanayojumuisha teknolojia ya TEHAMA, kuwa nyenzo muhimu katika kuongeza ufanisi kwenye mifumo ya uzalishaji huduma na utawala;

NA KWA KUWA, mashirika mengi ya umma hayazingatii matumizi sahihi ya TEHAMA hali inayopelekea upotevu wa mapato na udanganyifu katika utoaji huduma zake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ikamilishe mchakato wa *public infrastructure (PKI)*

(b) Serikali iunde mfumo wa taarifa ya pamoja *(centralized ledger)* kuondoa udanganyifu wa mifumo ya taasisi.

(c) Serikali ihakikishe inasimamia kikamilifu taasisi na mashirika ya umma kuimarisha mifumo ya TEHAMA. Hatua hizi zitasaidia kuongeza ufanisi wa utoaji huduma, ukusanyaji wa mapato, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kudhibiti udanganyifu kwa lengo la kupata tija inayokusudiwa.

(11) Changamoto ya uendeshaji wa Kampuni ya Meli (*Marine Services Company)*.

KWA KUWA, Kampuni ya Meli *(MSC)* iliyokuwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari kwa sasa imekuwa Kampuni huru inayojitegemea;

NA KWA KUWA, kitendo cha Mamlaka ya Bandari kuendelea kumiliki baadhi ya mali za *(MSC)* kunaathiri

utendaji wa *(MSC)* ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa mtaji wa umma uliowekwa *(MSC)*;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali iharakishe mali zote za *(MSC)* zilizopo *Tanzania Port Authority* zirejeshwe haraka sana *(MSC)* zikiwemo chelezo, karakana na nyinginezo.

(12) Matumizi ya TEHAMA katika Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya *(NHIF)*.

KWA KUWA, Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa *(NHIF)* umeonesha udhaifu katika utoaji wa huduma zake jambo ambalo limepelekea Mfuko kupata hasara;

NA KWA KUWA, changamoto zilizojitokeza katika uendeshaji wa *(NHIF)* kwa kiasi kikubwa imetokana na kutokakuwa na mfumo thabiti wa TEHAMA inayotoa mianya ya kufanya udanganyifu kwa urahisi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihakikishe *(NHIF)* inaandaa mfumo madhubuti wa TEHAMA na kuanza kuutumia haraka iwezekanavyo kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma wa mfuko na kuziba mianya ya udanganyifu. *(Makofi)*

(13) Matumizi makubwa ya gharama za bima za Ndege kwa Shirika la Ndege la Taifa - *ATCL.*

KWA KUWA, Shirika la Taifa la *ATCL* linalazimika kununua Bima kutoka Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* ambapo *NIC* ananunua Bima hizo kutoka kwa Wakala wa Nje ya Nchi kwa mfumo wa moja kwa moja *single source;*

NA KWA KUWA, changamoto zilizojitokeza ni kwa Shirika la Ndege kujikuta linanunua bima hizo kwa gharama kubwa hali inayopelekea kupunguza faida na tija kwa Shirika;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ielekeze *ATCL* na *NIC* kufanya zabuni shindanishi ili kupata wakala mwenye bei nafuu, huduma bora na ambaye atazingatia uwiano wa ndege, shirika anazomiliki, hii italeta ufanisi, tija na kupunguzia shirika gharama za matumizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Serikali mmesikia maazimio hayo ambayo Bunge linataka kufanya maamuzi sasa? Kabla sijalihoji Bunge kuna Waziri ana jambo katika hayo maazimio? Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika naomba kwanza niseme tumepokea maazimio haya hatuna shida. Nilikuwa naomba tu kwenye azimio ambalo linaomba Serikali kukasimu madaraka kwa taasisi

zinazojiendesha kibiashara kuajiri ajira za moja kwa moja, taasisi zenyewe nilikuwa naomba tuongeze tu kwenye azimio hilo kwamba pamoja na kutoa kibali hicho, Serikali iweke utaratibu wa usimamizi wa mwenendo mzima wa utaratibu wa ajira hizo.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwanini? Sababu ni moja tu, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndiyo imepewa jukumu la kuratibu Utawala wa Utumishi wa Umma nchini ikiwa ni pamoja na kutengeneza bajeti ya mishahara kwa mwaka mzima kwa watumishi wote. Kwa hiyo, katika utekelezaji wa agizo hilo ni lazima sasa tu-*centralized* mahali ambapo tutaweka jukumu la usimamizi wa kuangalia mwenendo mzima sasa wa utekekelezaji wa maagizo na maelekezo hayo ambayo yatakuwa yamepata mamlaka taasisi hizo kuweza kuendelea kuajiri ili kusudi tuwe ndani ya mfumo mzima wa kisheria tulio nao wa kusimamia utumishi wa umma, vilevile ku-*manage wage bill* na mambo mengine ambayo yanahitajika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, azimio liliopo hapa linalohusu hivyo vibali vya kuajiri linasomeka hivi; Bunge linaazimia kwamba Serikali iweke utaratibu maalum wakutoa vibali kwa taasisi zinazojiendesha kibiashara ili ziweze kuajiri zenyewe, ajira za moja kwa moja na kuweza kuendana na soko la ushindani wa kibiashara. Hii sehemu ya kwanza imesema Serikali iweke utaratibu, kwa hiyo naamini ni Serikali ninyi wenyewe mtaweka utaratibu ndiyo linavyosomeka hapa kwangu, ama mimi sijaelewa hoja Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa

Spika, utaratibu mpaka sasa upo. Kwa mfano, TAMISEMI, Wizara ya Afya na mliona tulipotoa kibali cha ajira 44,000. TAMISEMI, Wizara ya Afya walipewa majukumu lakini kwa kuzingatia utaratibu uliopo Serikalini, Serikali yenyewe ilikuwa inasimamia na lengo ni ku-*control* yale mambo ya kimsingi.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu kwa dakika moja. Uwepo wa Sekretarieti ya Ajira ulitokana na ripoti ya Warioba ambayo ili-*insist* ku-*centralized* mchakato wa ajira ili kuzuia *nepotism* na mambo mengine, sasa sitaki kwenda huko. Azimio hili la Bunge la leo lina *logic* kubwa, *logic* yake ni kurahisisha taasisi hizi zinazojiendesha kibiashara ziweze kufanya kazi zake vizuri. Kwa kuwa tayari utaratibu upo wa kusimamia, nilikuwa nafikiria tuongeze neno fulani ambalo litasaidia kuzifanya taasisi hizo ndiyo ziendelee lakini zikiwa *supervised* na utaratibu ambao tayari upo unaoendelea kusimamia michakato.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ndani ya Serikali sasa hivi baada ya kugundua na sisi kwamba kuna hilo tatizo la taasisi hizo zinazojiendesha kibiashara wakati mwingine kucheleweshewa watumishi kwa kufuata *bureaucracy* ambayo inatakiwa ifuatwe na Sekretarieti ya Ajira. Tumeanza ndani ya Serikali kutafuta namna ama kuwa na utaratibu tofauti ama kuwa na chombo fulani ama kutengeneza mfumo fulani utakaorahisisha jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nakubaliana na hii lakini nilikuwa naomba kwenye azimio hilo ni lazima tuingize…..

**MHE KENNETH E. NOLLO**: Mheshimiwa Spika taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth subiri kidogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, azimio hilo ni lazima tuingize kitu ambacho kitatusaidia kuifanya Serikali iendelee pia kuwa na wajibu wa kusimamia michakato hiyo yote na *procedures* hizo zote kuikoa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hoja yako imeelewaka. Hapa kwangu inasomeka Serikali iweke utaratibu maalum, kwa hiyo ule umaalum nadhani unaweza ukaongeza sasa kwenye ule utaratibu ulipo mkaongeza hicho cha maalum ya kwamba Serikali iendelee kufanya hivi na hivi na hivi. Sisi tunachotaka wawekewe utaratibu kwa sababu wanao uwezo wa kulipa.

Wakati mwingine anaweza akafariki Mhasibu wa Taasisi fulani ambayo inao uwezo wa kumlipa na pesa zake huyo Mhasibu kimsingi zilikuwepo kwenye ile bajeti, lakini sasa kwa utaratibu huu uliopo unaleta changamoto kwa hilo shirika kuendelea kufanya kazi zake kwa ufanisi. Ndiyo maana sasa Bunge linataka kusema hivi Serikali iweke utaratibu maalum, kwa hiyo kule kwenye maalum ninyi mtajaribu kuweka mazingira ambayo mnataka bado kuendelea kuwa na jicho huko muweke, lakini muweke utaratibu mzuri ambao utapunguza ule mlolongo hawa watu kupata hao watumishi, kwa sababu unapunguza ufanisi wa kazi.

Hapa sasa kama ndiyo neno maalum halitoshi labda sasa ndiyo tuongeze, lakini sisi tunavyoona ukiweka neno Serikali iweke utaratibu maalum bado ni Serikali na

ikaweke huo utaratibu maalum unaotakiwa, sisi hatuwawekei. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, tunapokea. Kwa kuwa, nimesema tunaendelea pia na mchakato huo ndani ya Serikali ya kuondoa hiyo kadhia na kufanya hizi taasisi ziweze kufanikiwa katika mipango yake na hasa kwenye mfumo huu wa ajira, nitaomba tu tutakapokuwa tayari kutekeleza agizo hilo, tutaleta ndani ya Bunge lako ni nini ambacho tunaona kwamba sasa ni muafaka ili kiweze kuwa ni utekelezaji wa agizo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Naamini katika yale ambayo tulikuwa tumeazimia kule mwanzo, maelezo ambayo nilitoa mwanzoni kabisa ambayo tutawasikia upande wa Serikali Mwezi Febuari, 2023, hili pengine litakuwa ni mojawapo ya kuleta hiyo suluhu na Mheshimiwa Rais wetu na yeye anaitwa Suluhu, kwa hiyo tunaamini matatizo yote haya yatapata suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kenneth Nollo ulikuwa umesimama.

**MHE KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Waziri wakati anachangia, amekuwa anaji-*restrict* sana kwenye *wage bill* na namna ya kuajiri na *wage bill* inaenda kwenye *mass employment* kama hizi za Walimu, kwenye Afya lakini kwenye Mashirika yanayojiendesha kibiashara kwanza huwezi ukai-*connect* na *wage bill* kwa sababu wengi wanakuwa na mikataba, *let say* wa *five years* halafu baadae wanapewa ile *gratuity* yao, ndivyo inavyofanyika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo awali tulikuwa na utaratibu kama *TANAPA* inaajiri watumishi wake tulichokuja kukosea, sijui kukosea au kuweka *bureaucracy* ni kuiweka tena sasa Tume ya Ajira kwenye Mashirika haya, walikuwa na utaratibu wao wa kuajiri watu wao wanaowataka kwa vigezo na ufanisi uwakawa unaendelea zaidi. Kwa hiyo, kama ni utaratibu tunaoutaka kwamba wapewe mamlaka ya kuajiri watu wanaotakiwa kwenye nafasi ambazo wanaona zitaleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, katika maazimio ambayo yamesomwa hapa na Mwenyekiti wa *PIC*. Maazimio mawili moja ni azimio Na. 08 ambalo linahusu fidia ya wanunuzi wa pamba ambao Serikali iliji-*commit* na wao wakaingia kwenye manunuzi hayo wakiwa wamelipa bei zaidi na sasa wanadai Bilioni 21. Bahati mbaya sana lile azimio halijaweka sasa kwa sababu tunajua hawa watu ni kweli baada ya kukubali ombi hilo waliingia gharama na wengine wanadaiwa na wanayo madeni makubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa haijawekwa tumesema tu Serikali ilipe lakini hatujasema ni muda gani? Mi nafikiri kwamba tuliboreshe hili azimio, tuweke kabisa muda ili kwenda kutoa ahueni ya maisha ya hawa watu ambao wanayo madai kwa Serikali. Mfano, tunaweza tukasema

hata Miezi Mitatu Serikali itekeleze jambo hilo ili kuweza kunusuru hii hali ambayo ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni agizo la ujenzi wa Bandari ya Bagayomo.

**SPIKA:** Namba ngapi?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, namba sikuikamata vizuri. Lakini ni azimio la ujenzi...

**SPIKA:** Mheshimiwa, hebu ngoja kwanza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ni azimio Namba Tatu la ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, naomba tusiagize Serikali katika hili kupitia hii hatua ya taarifa ya Kamati na badala yake kwa sababu tunaanza mchakato wa kujadili mpango wa mwaka mmoja, jambo hili linatakiwa tulijadili tukiwa tayari tuna-*information* nyingi za kutosha za kiuchumi, kifedha, *capacity* ya nchi yetu kuingia kuutekeleza mradi huo na *position* yetu katika kipindi hiki tulichonacho.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tutakapoingia kwenye mpango wa maendeleo kwa mfano tunaotegea kuanza kuujadili wiki ijayo, tutapewa na Serikali uwezo wetu wa sasa hivi kama Taifa, kama tunaweza tukauanza mradi huo, *capacity* yetu tuliyonayo na *parameter* zingine za kiuchumi zitatu-*drive* kufika kule.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hili jambo ni la kibajeti zaidi ninalishauri Bunge lako lisitoe agizo hilo

badala yake kama nchi tunautaka huu mradi, tutakuwa na nafasi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, ngoja ngoja. Waheshimiwa Wabunge, tofauti ya hii taarifa na zile taarifa nyingine, ni kwamba hii taarifa kwanza haina uhusiano na *CAG*, jambo la pili hii ndiyo Kamati ambayo inashughulikia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kwa hivyo, ikisema kwamba Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ni kwamba wao kama Kamati labda itabidi Mwenyekiti ndiyo akujibu hapo, hayo unayouliza kwamba tumejiridhisha kwenye mpango na nini? Kwa sababu mpango kwa ujumla wake kwa kweli tunataka hii *SGR* ifanye kazi vizuri. Itafanya kazi vipi? Hapa naona mapendekezo yapo mawili, moja ni hiyo Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi wa ujenzi ya Bandari ya Bagamoyo. Pili Serikali iharakishe zoezi la kuongeza ufanisi wa Bandari ya Dar-es-Salaam. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpina unataka tubaki na moja la Dar-es-Salaam na azimio la Bagamoyo liondoke?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza….

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, Hapana! usianze tena na maelezo marefu, nijibu tu swali langu. Kwa hiyo unataka Bagamoyo hapa iondoke.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kifupi mno, Bagamoyo iondoke kwa sababu kwanza mradi wa Bagamoyo hatunao, utatekelezaje mradi ambao haupo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, mradi wa Dar-es-salaam uko nao?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, tunao kwa sababu si upanuzi tunaendelea nao kila leo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, aaaah! Na yenyewe lazima inakuja tofauti huu utekelezaji si ni wa moja, mbili, tatu na hatujawahi kupitisha zote kwa wakati mmoja na wao wanaendelea, sasa nilitaka tu hilo, kwa kuwa hilo nalo hatuna ngoja tumsikilize Mwenyekiti.

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Spika, labda nianzie hapo alipoishia Kaka yangu. Ni kweli mradi wa Bagamoyo ule wa *Port* na *Industrial Park* hatunao. Kwenye ule mradi wa Bagamoyo ukichukua *element* ya Bandari peke yake siyo mradi wa thamani kubwa, tumeeleza kwenye taarifa hii na inawezekana labda tumeandika kifupi, ukichukua ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ukikamilika, maana yake uwezo wa reli ile kusafirisha mzigo kutoka Bandarini kwenda kwenye nchi *land locked* na kutoka kwenye nchi hizo kuja Bandarini hautaweza kubebwa na Bandari ya sasa. Kwa hiyo, ukiona pale tumeandika kuongeza ufanisi moja, kuna suala la kujenga gati mpya, Gati ya 12, 13,14 na 15. Gati zile za kisasa zenye urefu wa mita 300.

Mheshimiwa Spika, kuna ufanisi wa Bandari pale kuna Kontena *terminal* nadhani mmeona kwenye Vyombo vya Habari wiki iliyopita ambao kwa sasa mkataba wa *TICTS* umeisha Septemba. Utendaji wa Wakala ule umezidi kuzorota na juzi madereva waligoma.

Kwa hiyo, Bandari na Serikali ifike mwisho kwenye majadiliano ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, jambo la Tatu, ukishapata *container terminal* mwendeshaji mzuri ama bandari ikiendesha yenyewe na hizi gati mpya bado ikiwa SGR iko kwenye *full fledge* haitoweza kupata mzigo wa kutosha na ndiyo maana kuna azimio la kuitaka sasa Serikali kipande kile cha Bandari ya Bagamoyo ambacho kwa hesabu zake Serikali inaweza kugharamia iharakishe ujenzi wa Bandari ile.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hayo ni mapendekezo. Sasa kwa namna Kanuni zetu zilivyo halafu hapa nimepokea pia maandishi ya Mheshimiwa Kigwangalla. Sasa tuanze kwanza na hoja ya Mheshimiwa Mpina, ifanyiwe maamuzi. Mheshimiwa Mbunge ametoa hoja kwamba, yeye kwa pendekezo lake anataka sehemu (a) ama sehemu ya kwanza, ama sehemu ambayo inazungumzia kwamba Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, anaona hiyo sehemu tungeiondoa. Sasa niwahoji ili tuweze kusonga mbele. Wabunge wanaoafikiana na hoja yake kwamba hiyo iondolewe waseme ndiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, waliosema siyo wameshinda. Mheshimiwa Kingwangalla aliteta mapendekezo ya marekebisho hapa sasa nimpe fursa ya

kuwasilisha. Mheshimiwa Kingwangalla kwa sababu Wabunge hawana hii sehemu ambayo unataka kupendekeza marekebisho, tusomee hilo azimio lako unalotaka liingie humu.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii. Mengine kwa kiasi fulani naona yameguswa na maazimio yaliyotangulia ya Kamati ya *PAC,* haya ningependa yaingie kwenye hii sehemu ya *PIC*.

Mheshimiwa Spika, Moja, Bunge linaazimia kuitaka Serikali kuhamishia umiliki, uendeshaji na biashara yote ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ya *Internet* kwa Shirika la *TTCL* ili kukuza mtaji wake na kujiendesha kibiashara zaidi. Pili, Bunge linaazimia kuielekeza Serikali kuanzisha mazungumzo na makampuni binafsi yaliyopewa vibali vya kujenga mikongo yake ya mawasiliano ya *Internet* juu ya namna ya kuinunua mikongo hiyo kwa sababu ya kiulinzi na kiusalama.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hapa tutapata wakati mgumu kidogo kwa sababu hatuna, lakini hili ulilolisema la kwanza la kuhusu *TTCL* nadhani Serikali tayari, hivi Naibu yuko hapa? Nadhani hili liko tayari kwenye mpango wa kupeleka huu mkongo *TTCL,* nadhani lilizungumzwa hap ana Mheshimiwa Waziri, kama mimi nakumbuka sawasawa?

Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuongelea hili

suala, lakini tayari Serikali inalishughulikia suala hili; na Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha bajeti hapa alisema kwamba, tayari mpango wa kupeleka *TTCL* upo kamili, lakini kuna taratibu ambazo ni lazima zifuatwe ili kuhakikisha kwamba linaenda kisheria zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Sawa. Jambo lingine ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Kigwangalla ni hili la, Bunge linaazimia kuitaka Serikali kuanzisha mazungumzo na hatimaye kununua mikongo yote ya mawasiliano ya *internet* kutoka kwa kampuni zote binafsi zilizopewa vibali vya kujenga mikongo yake ya mawasiliano ya *internet* kwa sababu za kiulinzi na kiusalama. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe ndio utakuwa unalisikia hapa, sijui kama una maelezo yoyote; maana mimi mwenyewe sielewi, kwa hiyo nitahitaji maelezo ya ziada ili nielewe hili kama azimio. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza labda niongee jambo moja. Tuna mkono wa Taifa ambao ndio barabara kuu ya mawasiliano, lakini hapo kabla tulikuwa na *consortium of operators* ambao walikuwa wanajenga katika *metro,* katika maeneo ya majiji, lakini watoa huduma wa mawasiliano kwa mfano *tiGO, Vodacom* na *Airtel,* n.k. wanaruhusiwa zaidi kuunganisha kwenye *last mile*. Maana yake ni kwamba, baada ya mkongo wa Taifa ulipofikishwa basi wao wanaweza wakajiunganishia kufikisha kwa wateja; hicho ndicho ambacho tunakiruhusu watoa huduma kuendelea nacho.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa mkongo kama kuunganisha Mkoa na Mkoa, kuunganisha Wilaya na

Wilaya na hatimaye badae Serikali inafikiria kuhakikisha kwamba, tunaunganisha kwenye kata. Lengo ni kuhakikisha kwamba, huduma ya *internet* inapatikana nchini kote. Nakushukuru.

**SPIKA:** Kwa hivyo, hili azimio linafananaje? Yaani hili azimio umelisikia? Kwa sababu mimi nisipoelewa ni kulikataa tu hapa mbele. Maana siwezi kulikubali kama mimi mwenyewe sijaelewa, Mheshimiwa Naibu Waziri, au nikuletee hapa hili ulisome ndipo tuelewane vizuri?

Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka nikusaidie kidogo katika hili suala. Suala la mkongo kwa mujibu wa sheria ni mali ya Serikali. Na kama alivyosema Naibu Waziri, mtu mwingine anaweza kuendeleza kutoka katika hii njia kuu ambayo ni Mkongo wa Taifa. Kwa hiyo mtu yeyote kujenga Mkongo wa Taifa kwanza hilo ni kosa la kisheria. Kwa hiyo Serikali haiwezi ikaenda ikanunua mkongo ambao umejengwa nje ya utaratibu.

Mheshimiwa Spika, na kulikuwa kuna maongezi yaliyoanza ku…

**SPIKA:** Sawa, sasa hapa nchini tunazo hizo kampuni zenye mikongo?

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Kwa hiyo, yamefanya makosa kisheria.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Yapo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ninachoelewa Serikali ina mikataba na hizi kampuni kwa kujenga Mkongo wa Taifa. Airtel, Zantel, tiGO na Vodacom*,* wana mkataba. Vilevile kuna mkataba mwingine na *Vietel.* Kwa hiyo hii mikataba iko *at execution stage,* inaendelea, na bado kuna migogoro iliyojitokeza katika utekelezaji wa kazi hii ya ujenzi ambayo nayo inaendelea hatua ya majadiliano.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Haya, Taarifa inatokea upande gani?

Haya, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

**T A A R I F A**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya makosa, iliruhusu kampuni za *Vietel* na *Vodacom* kujenga mtandao huo wa mkongo kwa kujitegemea. Na Kamati ya Bunge ya Miundombinu iliishauri Serikali kuhakikisha mkongo huu umilikiwe na Serikali yenyewe badala ya kampuni. Na walienda mbali, Kampuni ya *Halotel* walitengeneza mkongo mpaka kupeleka nchi jirani ya Burundi na sisi tulishauri na Kamati

iliilekeza Serikali wahakikishe wanatekeleza haraka kuhakikisha mkongo huu unamilikiwa na Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme hivi; ujenzi wa Mkongo wa Taifa ulijengwa kwa hatua; na ujenzi wenyewe ulijengwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Lakini fursa inapotokea wawekezaji wanapokuja Serikali iliingianao mikataba ya ujenzi katika maeneo ambapo mkongo wetu haujafika, au katika maeneo ambayo tunasema *missing links;* na ndipo sasa Serikali inapoingia mkataba. Mkongo unapojengwa tayari ule unakuwa ni mali ya Serikali moja kwa moja kwa sababu, wanaingia mkataba na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano *Halotel* walipewa kazi ya kujenga pale ambapo Mkongo wa Taifa ulikuwa umekomea. Tunafahamu kabisa kwamba, kulikuwa na changamoto, lakini Serikali tayari ilishachukua hatua katika changamoto ambazo zilijitokeza. Hata hivyo, bado Mkongo wa Taifa unabaki kuwa mali ya Serikali na kampuni zote ambazo zilijenga kwa mkataba wa makubaliano rasmi na Serikali. kwa hiyo baada ya kukamilisha mkongo ule unakuwa mali ya Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mkongo baada ya kujengwa na hizo kampuni binafsi unakuwa mali ya Serikali?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mikataba iliyopo ni mkataba wa kampuni hizo kujenga na ni kwa *segments,* kila *segment* wanayomaliza wanatakiwa kuikabidhi Serikalini. Kwa hiyo mwenye shughuli ni Serikali, makubaliano ni hawa kujenga ingawa vilevile ni *operators.* Kwa hiyo, wanapomaliza kwa mujibu wa ile mikataba lazima yanakuwepo makabidhiano halafu na utaratibu wa wao sasa kuruhusiwa kutumia.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ngoja, kwa hiyo, nikizungumza kwa kifupi nitasema hivi, hapa nchini pamoja na kwamba hizo kampuni ndizo zilizojenga, mikongo ile iliyojengwa kwa sasa ni ya Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo, kwa ufahamu wangu mimi. Na migogoro iliyopo…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Jamani, huyu ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, ngoja tusikilizane. Labda kama kuna mmiliki wa mkongo humu ndani, kama hakuna tusikilizane. *(Kicheko)*

Enhee, Mheshimiwa, niko sahihi siyo? Kwamba, hizi kampuni sawa zilijenga, lakini kwa sasa hiyo mikongo waliyojenga ni ya Serikali, niko sahihi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, labda niseme hivi, niliposema kuna migogoro, migogoro ni ya utekelezaji wa mikataba hiyo, lakini ni kati ya kampuni hizo na Serikali kwenye kukinzana kwa utekelezaji wa masharti. Kama ninavyosema wanapojenga wanakabidhi Serikalini halafu habari ya wao ili waendelee kutumia lazima Serikali iwakabidhi.

**SPIKA:** Sawa, Waheshimiwa Wabunge nimeelewa hoja yenu na nimeelewa namna ambavyo hamjamuelewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey Mwambe.

**T A A R I F A**

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nitoe taarifa kidogo ili kuweka sawa. Serikali tunakumbuka kwamba ilikopa fedha zaidi ya Dola za Mimarekani milioni 200 kutoka Serikali ya China ili kujenga Mkongo wa Taifa kwenye Serikali ya Awamu ya Nne. Lengo kubwa ni kusafirisha masafa na kuuza *band width* kwa kampuni binafsi za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, ilitokea hapo katikati kwamba kampuni zilizotajwa zinaitwa *consortium* za *MNOs (Mobile Network Operators)* hao *tiGO, Vodacom, Airtel…*

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Mwambe elimu hiyo ni ya muhimu sana na tunaihitaji, ila sasa kwa muda tulionao tunataka kufika sehemu ya kutoa maamuzi. Wewe tusaidie, hapa nchini haya maswali ninayouliza mimi ili nielewe, hapa nchini ziko kampuni zinamiliki mkongo? Au mkongo unamilikiwa na Serikali ila zenyewe ndizo zilizojenga? Ndilo swali lililopo mbele yetu.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kuna mikongo inayomilikiwa na tasisi au makundi matatu tofauti. Uko Mkongo wa Taifa unamilikiwa na Serikali, uko mkongo ambao unamilikiwa na *consortium* ambao ni kwenye *metropolitan* na kwenda Da-es-salaam – Arusha…

**SPIKA:** Ni kinanani hao? Yaani *ok,* ya kwanza inamilikiwa na Serikali, hiyo ya pili ni binafsi au ni Serikali?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni binafsi.

**SPIKA:** Ya tatu?

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni binafsi pia *Halotel* ambao ndio wana mtandao mrefu kuliko wote.

**SPIKA:** Haya ahsante, hapo tumeshaelewana. Kwa hiyo kuna mikongo ya aina tatu, miwili inamilikiwa na binafsi, Naibu Waziri! Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kuna jambo kidogo hapa linachanganya, lakini naomba niliweke

sawa. Ni kwamba, Serikali inaingia makubaliano na mkandarasi; mkandarasi akishakamilisha kazi anatakiwa akukabidhi. Maana yake ni kwamba kuna hatua za kukagua ile kazi ambayo umemkabidhi. Lakini baada ya kugundua kwamba ile kazi uliyomkabidhi hajaikamilisha vizuri Serikali haiwezi kuipokea hiyo kazi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tusikilizane. Malizia Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, sasa kilichopo ni nini; ni kwamba, Serikali iliingia mkataba na watoa huduma kujenga mkongo, lakini ule mkongo akishaukamilisha anatakiwa afanye makabidhiano na Serikali. Sasa, kinachosababisha makabidhiano yafanyike ni kwamba, vile vigezo ambavyo tumevitoa katika ujenzi wa huu mkongo lazima viwe vimezingatiwa. Na ndio maana kunakuwa na changamoto ya watoa huduma wengine hawakuwa wamekabidhi mkongo kwa Serikali kwa sababu, walikuwa hawajakamilisha vizuri, lakini mkongo ukishakamilika ni mali ya Serikali.

**SPIKA:** Sawa. Haya, Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwenda sana. Mheshimiwa Kigwangalla wewe ndiye mwenye hoja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Siwezi kupewa mimi taarifa sasa maana ndiye ninayezungumza.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ufafanuzi kidogo. Ufafanuzi tu kidogo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ngoja tuelewane vizuri. Hii hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla imeeleweka. Sasa ili tusirejee kule ambako tulikuwa tunajadili hapa kwa nguvu sana hoja za *KADCO* alipewa nani mkataba ukapita wapi, sijui nini, ili kule tusifike jambo hili badala ya kuweka kwenye maazimio litaelekea kwenye Kamati ya Miundombinu. Kule kwenye Kamati ya Miundombinu watapata fursa sasa ya kujifunza haya yote tunayoyazungumza halafu kwa sababu, kamati ile haijaleta Taarifa bado, italeta tarifa Januari, Februari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kule sasa ndio tutashughulikanalo hili jambo. Kwa hiyo, wao wapate nafasi ya kulishughulikia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kigwangalla hili linapelekwa kwenye kamati inayohusika na halitakuwa sehemu ya maazimio ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, wakati amesimama, Mheshimiwa Kigwangalla naona umesimama bado?

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kulifikisha hili jambo hapo. Nilikuwa naomba tuyatenge haya mambo mawili, lile la pili liende kwenye Kamati ya Miundombinu, lile la kwanza tuongeze tu *time frame*. Kwamba ni lini Serikali itakabidhi mkongo huu kwa *TTCL,* kwa sababu maelekezo ya Serikali kufanya hivyo yana zaidi ya miaka mitatu na hawajawahi kufanya hivyo.

**SPIKA:** Yatafanyikia yote upande ule kwa sababu, yote yanahusika huko.

Haya, wakati amesimama Mheshimiwa Mpina alileta hoja mbili, ile ya kwanza ya Bagamoyo imeshakataliwa, nyingine alileta ya kuhusu kwamba hapa ingewekwa labda miezi mitatu. Sasa hapa zinazungumziwa bilioni 21 na kuzipata hizi na bajeti huwa tunapitisha sisi humu Bungeni, kama hatukupitisha hiyo bajeti maana yake Serikali itapata wakati mgumu wa kuzipata ndani ya miezi mitatu. Ila hoja ya msingi ni kwamba, kamati imelileta hili jambo na Waziri hapa amezungumza kwamba walishalipa bilioni 12 na kitu, kwa hiyo wanaendelea na huu ulipaji.

Sasa kwa sababu tumeshasema tangu mwanzo, kwamba tutapata taarifa ya haya tunayoazimia mwezi wa pili mwakani, tutasikia hiyo mwakani kwamba, kwa upande wa Bodi ya Pamba Serikali inasema nini. Sawa jamani eeh. Nadhani hilo limeeleweka.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa niwahoji ili tufanye maamuzi juu ya haya maazimio 13. Sasa hii kama nilivyosema hii ni tofauti na zile Kamati nyingine ambazo wameleta hapa maazimio, lakini tunachukua yale pamoja na yaliyoko kwenye taarifa za Mkaguzi na Mdibiti Mkuu wa Serikali; hawa ni tofauti kidogo, kwa hiyo ni haya maazimio 13 ndio tunayopitisha, sasa wao hawawezi kwenda kusema yalikuwepo na mengine huku.

Waheshimiwa Wabunge sasa niwahoji, eeh, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha; au zipo fedha za pamba? Karibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa hii fursa.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka kwenda kushauri tu kwenye Azimio Namba Saba. Azimio hili ni azimio zuri, lakini ningeshauri kwamba tuweke hapa au nilisome?

Mheshimiwa Spika, *"Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze ahadi yake (Commitment) waliyotoa kwa Benki ya Kilimo ya kuiongezea mtaji kwa kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa kila mwaka wa fedha."*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ushauri wangu hapa; tusiweke kiwango cha bilioni 100, tuseme kadiri ya hali ya uchumi itakavyowezekana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, inawezekana tukaweka zaidi ya hiyo inawezekana tukashuka hapo. Huo ushauri wangu.

**SPIKA:** Hili nadhani sina haja ya kuwahoji Wabunge ni kama wameshakataa.

Wabunge mnaokubali hoja ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, hapa tusiweke kiwango mseme Ndiyo. Msioafiki mseme Siyo.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**SPIKA:** Haya, limekataliwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa, Mheshimiwa Tabasam?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, kuna Azimio Namba 3(b) ambalo mimi niliomba kidogo liongezwe, liboreshwe, hapa ambapo inasema Serikali iharakishe zoezi la kuongeza ufanisi katika bandari.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, katika maelekezo ni kwamba, tunalo eneo liko Kwala palepale tu, eneo hilohilo la hukohuko Kibaha, Pwani. Eneo la Kwala ambalo Serikali ililinunua hekta 500 pale na wametengeneza kasehemu kadogo, kuna barabara inatoka Visiga kwenda kule na kuna barabara inatoka Ruvu pale kwenye *SGR* kwenda katika lile eneo. Lile eneo linajengwa kutoka mwaka 2017 mkandarasi hajamaliza na sisi tunakosa mahali pa kutunza makasha.

Mheshimiwa Spika, naomba azimio hilo liingie. Kwamba, Serikali ikahakikishe wanamaliza hiyo kazi ili tupate mahali pa kushushia haya makasha. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hilo eneo Spika wenu hajafika kwa hivyo, mtihani kidogo na taarifa sinazo nyingi hizo, ukiacha ya kwenye taarifa ya habari niliona timu kubwa imeenda kule kutembelea hilo eneo, kwa hiyo naamini kwamba kuna jambo linaendelea huko. Kwa hiyo hilo kuingia kwenye maazimio itakuwa mtihani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge ni muhimu, kwa sababu ukiwa unasimamia kikao lazima wewe ndio uwe umeelewa kuliko watu wengine. Sasa kama wewe hukuwa umeelewa tena itakuwa balaa. Naona Wabunge wanafurahi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa mnipe fursa niwahoji kuhusu hoja hii.

Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki. Asanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wetu na Makamu Wenyeviti wa Kamati hizi tatu kwa kazi kubwa sana waliyoifanya ya kupitia Taariffa za *CAG,* lakini pia kwa upande wa Kamati yetu ya *PIC* kupitia taarifa za *Treasury Registrar.* Tunawashukuru sana na tunawapongeza sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia, niwashukuru ninyi na kuwapongeza kwa sababu, michango namna ilivyotoka haikutoka kwenye taarifa tu za Kamati, lakini mmeibua na mambo mengine kabisa ambayo yapo lakini kwenye taarifa ya *CAG* kuashiria kwamba mmezisoma zile taarifa za *CAG* na michango yenu kwa kweli, ilikuwa yenye tija

sana. Kwa hiyo, ninawapongeza sana Wabunge wote kwa kufanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, safari hii tulifanya tofauti kama mlivyosema na sitazungumza kwa kirefu, lakini lengo hasa lilikuwa la kufanya hiki ambacho kimefanyika, ili watu wapate picha ya kwanza uwekezaji wa mitaji ya umma, lakini pia wapate picha ya fedha za umma zinasimamiwa namna gani? Kwa sababu, Katiba ya nchi yetu imelipa Bunge mamlaka ya kuisimamia Serikali, kwa hiyo wananchi lazima wajue kwamba, Bunge lao linaisimamia Serikali kwenye hoja zipi. *(Makofi)*

Sasa wengine watakuwa wanashangaa kwamba, jamani mbona mambo mazuri mengi sana yamefanywa? Mbona walikuwa wanasema mabaya tu?

Eeh, safari hii tulikuwa tunaangalia taarifa za ukaguzi. Kwa hiyo, tunaangalia yale mambo ambayo hayako vizuri, yale yaliyo vizuri tutakutana wakati wa Bunge lile la bajeti, tutakuwa tunaambiana yaliyo mazuri, ambayo hayakukaa sawa na tunatoa ushauri. Kwa hiyo, kwa Bunge hili lazima tueleze yale ambayo hayako sawasawa ili yarekebishwe na tufike mahali ambapo Bunge hili kwa ajili ya kuisimamia Serikali tutafika hapa wote tukiwa tunafurahi, kwamba kila mahali Serikali imekaa vizuri; kwa hiyo, tunataka tufike hiyo sehemu. Itatuchukua muda na tusiwe na wasiwasi, mambo haya huwa yanachukua muda, lakini ni hatua kwa hatua, na hii ni mojawapo ya hizo hatua. Kwa hiyo, niwashukuru sana Wabunge kwa sababu tungeweza kutoa hizo siku nyingi halafu Wabunge mkawa hamna michango na hamjasoma. Kwa hiyo, ndio maana nimeanza kwa kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia niwashukuru Mawaziri kwa ushiriki wao kwenye hoja hii ya Kamati. Kwanza kwa ufafanuzi, lakini pia kwa kutoa mchango wa mawazo yenu kwenye haya ambayo Kamati na pia Wabunge wameyaelekeza Serikalini. Pia, niwashukuru kwa utayari kwa sababu kukaa kwenu hap ana kuweza kujibu hoja mbalimbali ni kuonesha utayari, kwamba yale ambayo mnaagizwa sasa na Bunge, na kwa sababu Serikali ipo humu Bungeni tunaamini mtaenda kuyafanyia kazi kwa sababu mmeyasikia wenyewe na mmewasikia Wabunge wakiyazungumzia.

Yako baadhi ya mambo ambayo hayajaingia kwenye maazimio kwa sababu ya pengine aina ya mambo yenyewe, kwamba hayakuwa sehemu ya hesabu, lakini ni michango mizuri sana ambayo itasaidia tunapoenda wiki ijayo kwenye kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Ajili ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kwa hiyo, kwa yale ambayo wamweshayachangia na Wabunge hawa huenda wasiyarejee tena, naamini yatawasaidia katika kujipanga kwenye bajeti zenu za kisekta huko mbele tutakapokuwa tumehitimisha zoezi la kujadili mapendekezo ya mpango na badaye mtakapotuletea mpango utakuwa na mambo mengine ambayo yameshazungumzwa hapa. Na tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Na hapa nisisitize, Maazimio haya ya Bunge, kama ambavyo tumeona mabadiliko, hatutarajii kwamba tutakutana hapa mwakani, inshallah Mungu atuweke mwezi wa kumi na moja, halafu tuwe tunazungumzia taasisi zilezile, jambo lilelile na tuwe hatujapiga hatua.

Tutakapokuwa tunajadili tunatamani tuwe tunajadili hatua zilizopigwa katika maeneo mbalimbali ambayo Bunge limetoa maamuzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia, niwashukuru sana kwa siku ya leo, maana siku ya leo ni Jumamosi, na sasa ni karibia Saa 11:00, na wote tumekaa hapa kuanzia Saa 3:00 asubuhi. Kwa hiyo, ninawashukuru sana Wabunge kwa uvumilivu wenu maana mngetoka humu ndani sijui ningekuwa nimebaki na nani, kwa hiyo ninawashukuru sana kwa uvumilivu wenu. Hii inaonesha namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge kwanza mnao utayari wa kuwawakilisha wananchi katika hali yoyote. Na kwa kweli, sijaona idadi ya watu ikipungua humu ndani, kuashiria kwamba wote tumekaa hapa kama ni njaa tunayo, kama ni vipi tuko wote hapa ndani. Kwa hiyo ninawapongeza sana kwa uwakilishi mzuri sana na unaonesha uzalendo kwa kweli kwa nchi yetu. Kila mtu alitaka kusikia na alitaka kuwa sehemu ya maamuzi ya Bunge. *(Makofi)*

Kwa kweli, kwa wale Wabunge ambao hawakuwepo nadhani tutaendelea kukumbushana, lakini hili Bunge la kuisimamia Serikali ndilo Bunge hasa kila Mbunge anapaswa awepo, kwa sababu ndizo hoja zetu hizi. Bunge hili la mwezi wa 11 na Bunge la Januari, kwa sababu ndipo tunazungumza yale mambo ambayo sisi ndio tunaosema halafu Serikali inatusikiliza, kwa hiyo ni muhimu sana sote kushiriki kwa pamoja.

Kwa hiyo, baada ya shukrani hizo Waheshimiwa Wabunge, tangazo moja, linahusu kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Mmemuona hapa Mheshimiwa Mkuchika ameshakaa, mkishamuona pale

basi mjue amepewa heshima na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye hayupo Dodoma, kwa hivyo yeye ndiye anayekaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu ya hiyo nafasi, unajua anakuwa anakaimu humu ndani, tukishatoka pale mlangoni tena ndiyo basi. Hata hivyo, ni heshima kubwa sana kukalia kile kiti. Kwa hiyo kila la heri Mheshimiwa Mkuchika, japokuwa ndiyo tumefika mwisho wa siku lakini tunashukuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na shukrani hizo na pomgezi hizo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 10:27 Jioni Bunge Liliahirishwa Hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 7 Novemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*